Tunawezaje kudhihirisha msingi wa Kibiblia wa tumaini letu na kulithibitisha kwa Wakristo na kwa wasioamini walioshirikishwa? Tunawezaje kutamka matumaini yetu kwa Wabunge, kwa wafanya biashara au kwa akina mama? Tunawezaje kupeperusha bendera ya tumaini katika dunia inayozama kwenye ukosefu wa matumaini na utazamiaji mabaya tu?

Hivyo, tunayo furaha kubwa kuwasilisha hoja za Dk. Thomas Schirrmacher. Matamko haya hujumuisha nia yetu ya kufungua hazina ya tumaini la Kibiblia kwa wengi, yaani wanatheolojia na watu wa kawaida; na kuwatia moyo kufikiri juu ya somo hili.

Schirrmacher ni Profesa wa Theolojia (katika Ethics, missions, world religions), Rais wa Martin Bucer Theological Seminary na wa Giving Hands (Mikono itoayo), ambalo ni shirika hai la kimataifa la misaada; na mmiliki wa shirika la uchapaji (Publishing House). Ameandika na kuhariri vitabu 40 na anatajwa kwenye Marquis "Who's Who in the World", katika "International Who is Who of Professionals", katika "Who is Who in der Bundesrepublik Deutschland" na katika "International Who's Who in Distance Learning". Anazo shahada zifuatazo: M.Th. (STH Basel, Switzerland), Drs. Theol. (Theologische Hogeschool, Kampen, Netherlands), Drs.Theol. (Missiology, Johannes Calvin Stichting, Kampen, Netherlands), Ph.D (Cultural Anthropology, Pacific Western University, Los Angeles), Th.D (Ethics, Whitefield Theological Seminary, Lake-land, D.D. (Honorary doctorate, Cranmer Theological House, Shreveport).

ISBN 978-9987-718-02-3 (TASCM)
ISBN 978-3-928936-20-0 (RVB)

TASCM | RVB INTERNATIONAL

TRANS-AFRICA SWAHILI CHRISTIAN MINISTRIES
TANZANIA

Thomas Schirrmacher Tumaini Kwa Afrika

TASCM | RVB

Thomas Schirrmacher

Tumaini Kwa Afrika

Hoja 66

Dibaji na
Prof. Mchungaji Dk. Thomas K. Johnson

TASCM | RVB

Thomas Schirrmacher

Tumaini Kwa Afrika

RVB International

Volume 20

1	Thomas Schirrmacher:	GOD Wants You to Learn Labor and Love
2	Thomas Schirrmacher:	Legends About the Galileo-Affair
3	Thomas Schirrmacher:	World Mission – Heart of Christianity
4	Thomas Schirrmacher:	Law or Spirit – an alternative View of Galatians
5	Thomas Schirrmacher:	Human Rights Threatened in Europe
6	Thomas Schirrmacher:	Be keen to get going – William Carey's Theology
7	Thomas Schirrmacher:	Love is the Fulfillment of the Law
8	Thomas Schirrmacher:	Studies in Church Leadership
9	Monte Wilson:	The Most Important Rule for Living
10	Monte Wilson:	Principles of Success in Business
11	Th. Schirrmacher (Ed.):	A Life of Transformation – From Politician to Good Samaritan – A Festschrift for Colonel Doner
12	Thomas Schirrmacher:	DIOS Quiere Que tu Aprendas, Trabajes y Ames
13	Christine Schirrmacher:	La Vision Islamica de Importantes Enseñanzas Cristianas
14	Thomas Schirrmacher:	Sheria au Roho?
15	Thomas Schirrmacher:	Upendo ni Utimilifu wa Sheria
16	Thomas Schirrmacher:	Mateso ya Wakristo Yanatuhusu Sisi Sote
17	Monte Wilson:	Sheria Muhimu Zaidi katika Kuishi
18	Thomas Schirrmacher:	Mungu Akutaka Ujifunze, Ufanye kazi, na Upende
19	Christine Schirrmacher:	Mtazamo wa Kiislamu juu ya Mafundisho Makuu ya Kikristo
20	Thomas Schirrmacher:	Tumaini kwa Afrika
21	Thomas Schirrmacher:	Mafunzo Yahusuyo Uongozi wa Kanisa

Thomas Schirrmacher

Tumaini Kwa Afrika

Hoja 66

Kimetafsiriwa na Yohana Noah Bwire

Kimehaririwa na Emmanuel Buganga

TASCM | RVB International

Bibliographic information published by the Deutsche Nationalbibliothek

The Deutsche Nationalbibliothek lists this publication in the Deutsche Nationalbibliografie; detailed bibliographic data are available in the Internet at http://dnb.d-nb.de

ISBN 978-3-928936-20-0

© Copyright 2002, 2011 by
Reformatorischer Verlag Beese
www.rvbeese.de / info@rvbeese.de
Printed in Germany

ISBN 978-9987-718-02-3

© Kwa Toleo la Kiswahili, 2011
Trans-Africa Swahili Christian Ministries
P.O. Box 772,
Mwanza, Tanzania

Toleo la Kwanza, 2011 Nakala 2,000

Maandiko Matakatifu:
The Holy Bible in Kiswahili
Union Version, 1994

Mistari ya Biblia iliyokolezwa ni tafsiri ya mwandishi mwenyewe kutoka katika Maandiko Matakatifu asilia ya Kigriki.

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri, kupiga chapa, kurudufu au kutoa kitabu hiki kwa njia yoyote ile bila idhini ya Trans-Africa Swahili Christian Ministries, Idara ya Maandiko.

Kimepigwa Chapa na: Inland Press, P.O. Box 125, Mwanza, Tanzania (East Africa) TEL. +255 28 2560175 inlandpress@yahoo.com

Tabaruku kwa

Rudolf Diezel

Mfano wa kuigwa na rafiki aliye baba

"**Na sasa haya matatu yanadumu: imani, tumaini na upendo.**
Lakini lililo kuu kati ya haya ni upendo."
(1 Wakorintho 13:13)

"**Bali mtakaseni Bwana Mungu katika mioyo yenu:**
na mwe tayari daima kumjibu kila mtu awaulizaye
sababu za tumaini lililo ndani yenu kwa unyenyekevu
na kwa hofu."
(1 Petro 3:15)

"**Kwa kuwa najua mipango niliyonayo kwa ajili yako," asema BWANA,**
"mipango ya kufanikiwa na si ya kukudhuru,
mipango ya kukupa tumaini na siku zijazo."
(Yeremia 29:11)

"Tumaini ni kwa ajili ya uwepo wa mwanadamu
kama oksijeni ilivyo kwa ajili ya mapafu.
Pasipo oksijeni, mgonjwa hufa kwa
Ukosefu wa hewa. Pasipo tumaini, mtu husumbuliwa
na msongo wa kukata tamaa, kupooza kwa bidii
ya mtu kiroho kunakotokana na hisia za kukosa maana,
na za ubatili wa maisha."
(Emil Brunner)

YALIYOMO

DIBAJI: TUMAINI HUTAFUTA UELEWA 11

TUMAINI KWA AFRIKA HOJA 66 13

TUNAHITAJI TUMAINI 13
1. Tumaini Huhusisha Akili 14
2. Tumaini ni Halisi kwa Wakristo – Imani na Tumaini Huwa Pamoja 15
3. Tumaini Hujenga Umoja 15
4. Upendo Hujenga Tumaini – Tumaini Hujenga Upendo 16
5. Mwanadamu Hawezi Kuishi bila Tumaini 16
6. Kesho Hutegemea Leo 18
7. Tumaini Hujenga Siku Zijazo zilizo Halisi 19
8. Tumaini si Ukokotoaji Tulivu, kwa kuwa Hushughulika na Mambo Ambayo Bado Hayajaonekana 19

TUMAINI KATIKA MUNGU PEKEE HALIPATIKANI KWA JITIHADA ZETU 21
9. Tumaini Hutegemea Neema na siyo Mafanikio 21
10. Tumaini Haliwezi Kupatikana kwa Kufanyiwa Kazi 21
11. Mungu Hatoi Tumaini tu; Yeye ni Sababu ya Tumaini Letu 22
12. Waovu Hawana Tumaini 22
13. Tumaini bila Mungu lina Udanganyifu 24
14. Tumaini bila Mungu ni lazima Litafute Mbadala katika Uumbaji 24
15. Hakuna Mbadala Uwezao Kuchukua Nafasi ya Mungu kama Msingi wa Tumaini, Hadharani au Faraghani, kama ilivyo katika Dini ya Mali (Mammon) 25
16. Vita dhidi ya Tumaini Bandia 27

MUNGU HUTOA TUMAINI 29
17. Mungu Mwenyewe Daima Amekuwa Mtoaji wa Tumaini – Tangu Mwanzoni Kabisa mwa Historia 29
18. Mungu Mwenyewe Huleta Tumaini – katika Yesu 29
19. Mungu Mwenyewe Hutupa Tumaini – katika Roho Mtakatifu .. 29
20. Mungu Mwenyewe Hutupatia Sisi Tumaini – katika Kanisa, yaani Mbeba Tumaini 30
21. Kristo Ndani Yetu, Tumaini la Utukufu 31

22. Tumaini kupitia Msalaba 31
23. Tumaini la Kurudi kwa Yesu Mara ya Pili na Ufufuo wa Wafu 32

MUNGU NI WA KUAMINIKA 35
24. Tumaini Letu kwa Mungu ni Thabiti, kwa sababu Mungu ni wa Kuaminiwa 35
25. Tumaini ni Jambo la Hakika kwa sababu ya Uaminifu wa Mungu na Ahadi Yake 35
26. Tumaini Letu Limejengwa juu ya Msingi wa Kiapo cha Mungu36
27. Tumaini Humaanisha Kazi 39
28. Tumaini Hujengwa kwenye Neno la Mungu 40
29. Tumaini letu lina Msingi katika Utendaji Kazi wa Mungu – si katika Mihadhara 41

TUMAINI HUBADILI MWENENDO WETU 42
30. Tumaini la Kweli Husadiki kwamba Mungu ni Mwenye Uweza Wote 42
31. Tumaini Hutupatia Usalama na Amani ya Mawazo 43
32. Tumaini Hutupatia Ujasiri 44
33. Tumaini Hutufanya Tuwe wenye Kutegemea Mema na Wahalisia – Kukata Tamaa si Jambo Mbadala 44
34. Kama Tukitarajia Kile ambacho Kibinadamu Hakiwezekani, Basi Tutafanya Yote ambayo Kibinadamu Yanawezekana 47
35. Tumaini Hutufanya Watulivu, lakini si kuwa Wazembe na Wasio Watendaji 47
36. Tumaini Hutufanya Tuwe Watendaji na Watetezi wa Haki 48
37. Tumaini Hutupatia Vipaumbele Vipya, ambavyo Hutuwezesha Kuachilia Mbali Mapendeleo Yetu 48
38. Tumaini Hutufanya Welevu na Wavumilivu kwa Wengine 48
39. Tumaini Hujenga Ustahimilivu 49
40. Kwa Sababu Tumaini Hutarajia, Basi Tumaini Hufurahia 49

TUMAINI KATIKA MATESO NA UPINZANI 51
41. Tumaini Huhitaji Mateso na Jitihada – Utambuzi wa Ukosefu wa Matumaini na wa Faraja 51
42. Maombi Hutuongoza kwenye Tumaini na Tumaini Hutuongoza kwenye Maombi 52
43. Mateso kwa ajili ya Tumaini 53
44. Tumaini Halishindwi, kwa sababu Hutoka Ndani 53
45. Tumaini Halishindwi, kwa sababu Hutoka Mbinguni 54
46. Tumaini Hutulinda dhidi ya Yule Mwovu 54

TUMAINI MBELE YA TASWIRA YA SIKU YA HUKUMU 56
47. Maandiko Huhalalisha Tumaini la Kanisa Kukua 56
48. Tumaini Mbele ya Upinzani wa Kidini na wa Kiserikali 57
49. Bado tuna Tumaini, hata Mbele ya Hukumu Ijayo..... 58
50. Mbele ya Hukumu ijayo, Mungu Hujaribu Imani yetu 59
51. Tumaini ni Zaidi ya Ubashiri 60

TUMAINI KWA AJILI YA NYANJA ZOTE ZA MAISHA 62
52. Matengenezo na Uamsho Humaanisha Tumaini kwa Kanisa na kwa Jamii..... 62
53. Tumaini kwa Wanyonge..... 64
54. Tumaini kwa Tamaduni Zote na Mataifa Yote..... 64
55. Tunahitaji Kueleza Tumaini Letu katika Hali ya Kueleweka Zaidi Kuhusu Nyanja Zote za Maisha na Uumbaji 66
56. Tumaini la Kibiblia Dhidi ya Tumaini Danganyifu la Maadili ya Kibwanyenye 71
57. Tumaini kwa ajili ya Uhifadhi wa Uumbaji 74
58. Tumaini kwa Jamii 74
59. Tumaini kwa Familia..... 76
60. Tumaini kwa ajili ya Uchumi 77
61. Tumaini kwa ajili ya Mfumo wa Kisheria..... 78
62. Tumaini kwa Wanasiasa..... 80
63. Tumaini kwa ajili ya Amani 81
64. Tumaini Huhitaji Mazungumzo na siyo Vurugu 82
65. Tumaini kwa Kanisa..... 83
66. Kuna Tumaini kwa masuala ya Kisiasa wakati Kanisa Linapotubu 84

VISAWE NA MAELEZO YA MANENO..... 87

VIFUPISHO VYA MANENO 90

DIBAJI

TUMAINI HUTAFUTA UELEWA

Wakati mwingine huwa nafungua mhadhara unaohusu imani ya Kikristo kwa maneno maarufu ya Ketekisimu ya Heidelberg (1563), “Kipi kilicho *faraja* yako pekee maishani au kifoni?” Kila wakati mtu huwa anauliza kwa haraka, “Je, *faraja* ina maana sawa na *tumaini*?” Huwa najibu, “Katika msamiati wa karne ya 16, nadhani neno ‘faraja’ hujumuisha kile tukiitacho ‘tumaini’ leo.” Hii humaanisha, kwa kutumia msemo bora wa Kikristo, “*tumaini* langu pekee maishani na kifoni ni kwamba Mimi, [katika] mwili na roho, ni mali ya Mwokozi wangu mwaminifu, Yesu Kristo.” Kwa hatua hii, tumeanza mchakato muhimu wa kuiweka katika muktadha imani ya kiinjili ya kihistoria kuhusiana na maswali na mahitaji ya karne ya 21, wakati ambapo watu wanatazamia tumaini kila mahali. Pia tunaona tunahitaji kufanya tafakuri makini.

Moja kati ya msemo muhimu wa mababu wa Kikristo ulikuwa “imani hutafuta uelewa;” kanuni hii pia iliandikwa kwa kutumia maneno mengi, “Naamini ili niweze kujua.” Misemo hii, kwa mtazamo wa kwanza, ilikuwa usihi: Wakristo hawana budi kufikiri kwa kina juu ya imani na kufikiri juu ya maisha yote kwa kupitia nuru ya imani ya Kikristo. Lakini misemo hii pia hujumuisha uchunguzi muhimu juu ya maisha ya mwanadamu kwa ujumla zaidi: kile watu wanachodai kujua kwa sehemu huibuka kutokana na imani yoyote waliyonayo. Daima watu hufikiri juu ya mambo kwa kupitia nuru ya kujitoa kwao katika imani ya awali, hata kama hawakusudii kufikiri kupitia nuru ya imani yao. Imani ya mtu au ya jamii hutumika kama seti ya imani tawala ambazo huwaambia kile wanachopaswa kufikiri. Kuna uthibitisho mzuri kuwa jambo hili ni la kweli hata kwa mkana-Mungu. Misemo yetu ya Kikristo ni njia ya kuwa waungwana juu ya kile ambacho watu wa dini zote na mitazamo-dunia yote hujaribu kufanya.

Lakini imani ni ya kipekee katika tunu tatu za kiroho. Mtakatifu Paulo alitufundisha, “**Na sasa haya matatu yanadumu: imani, tumaini na upendo.**” (1 Kor. 13:13). Ikiwa imani hutafuta kuelewa, basi tumaini na upendo pia ni lazima vitafute kuelewa. Ikiwa naamini ili niweze kujua, basi sina budi pia kutumaini na kupenda ili niweze kujua. Na Mtakatifu Petro alitufundisha, “**Daima mwe tayari kutoa jibu (*apologia* kwa Kigriki) kwa kila mmoja anayewaomba mtoe sababu kwa ajili ya tumaini mlilonalo**,” (1 Pet. 3:15), [hii ni] amri ya kufikiri kwa kutumia nuru ya

tumaini letu. Chini ya athari za utamaduni wa kisasa, wengi wetu tumejiegemeza kutenda kama kwamba tumaini (sawa na imani na upendo) halina budi kusimama kwenye msingi wa sababu moja au sababu nyingi ("utetezi" wetu), lakini inawezekana si rahisi hivyo. Inawezekana sababu moja au nyingi pia husimama kwenye msingi wa tumaini. Habari au maelezo yenye fikra yanaweza kutiririka kutoka kwenye tumaini na vilevile huongoza kwenye tumaini. Utetezi wetu wa tumaini hujumuisha matumizi kamili ya tumaini la Kikristo kwa maisha yote.

Katika Zaburi 130:7 Israeli ilipewa wosia, "**Weka tumaini lako kwa Bwana**." Kwa mazingira yao, ikiwa watu hawakuweka tumaini lao kwa Bwana, basi wangeweka tumaini lao kwa sanamu, iwe ni sanamu ya kidini au ya kisiasa. "Mtu kuweka tumaini" kwa urahisi ni sehemu ya kawaida ya maisha ya mwanadamu tusiyoweza kuiepuka, lakini mahali ambapo tumaini la mtu limewekwa linafungamanishwa kwa ukaribu na mfumo wote wa maisha na mfumo wote wa kufikiri juu ya kila kitu. Tumaini (likijumuisha tumaini la uongo) lina matokeo makubwa. Vizazi kadhaa hapo nyuma, vingi katika Ulaya vilijadili "falsafa ya kukata tamaa," lakini jambo hili ilikuwa vigumu kuendelea, kwa kuwa daima watu huweka tumaini lao kwa kitu fulani. Ni muhimu kuweka tumaini letu kwenye mahali sahihi na kisha kutafuta kuelewa juu ya kitu chochote katika nuru ya tumaini letu. Lakini ni kwa namna gani?

Swali na jibu la pili lisilofahamika sana katika Katekisimu ya Heidelberg huuliza, "Ni mambo mangapi unayopaswa kuyajua, ili uishi na kufa katika faraja hii?" Jibu ni *matatu*, likijumuisha ufahamu wa dhambi zetu, ufahamu wa Neema ya Mungu, na ufahamu wa namna tunavyopaswa kuishi. Ufahamu unaohusiana na *tumaini* pia ni tata na una sura nyingi. Na ufahamu tata unaotokana na tumaini unaweza na lazima utumike kwa mawanda yote ya matatizo na fursa tunazokabiliana leo.

Kwa Wakristo, ni jambo lenye thamani sana kuchukulia na kutamka kwa ufasaha uelewa ambao hutokana na tumaini la Kikristo. Ama sivyo tunaweza kuifikiria dunia yetu kupitia nuru ya tumaini la uongo au kujipatia tumaini kutoka kwenye vyanzo potovu. Kila mmoja hutafuta kuelewa na kuiongoza dunia kupitia tumaini lao. Kwa sababu ya lengo hili, kwa dhati nakutia moyo kujishughulisha na mafundisho ya rafiki yangu mwaminifu, Thomas Schirrmacher. Ungana naye katika mchakato wa tumaini kutafuta uelewa. Ninashawishika kwamba tumaini lipatikanalo katika Mungu Mtatu ni tumaini la kweli ambalo huongoza kwenye uelewa wa kweli.

Prof. Mchungaji Dk. Thomas K. Johnson

Tumaini kwa Afrika
Hoja 66

TUNAHITAJI TUMAINI

"Kwa maoni yangu, mwingiliano wa Ulaya
hutoa fursa nyingi kubwa kwa misheni,
vitu hivyo vyote ni karama na majukumu
yaliyotolewa kwa kizazi chetu na Mungu wa historia.
Kwa msaada wake na chini ya Ufadhili wake wenye hekima,
tunaweza kutumia fursa hizi kwa faida
kama tutafanya maamuzi sahihi leo."[1]

Somo lifuatalo limetungwa kwa ajili ya Tumaini kwa Afrika, somo hili linachunguza matumizi ya dhana ya 'tumaini' katika Agano la Kale[2] na Agano Jipya na huzingatia umuhimu wa vifungu hivi kwa ajili yetu leo (Maandiko yatanukuliwa).

Kila hoja itajadiliwa kikamilifu kutoka katika mtazamo wa Kibiblia na Kitheolojia, na inaambatana na maana ya somo kimaisha kulingana na wakati wetu.

---

[1] Bernhard Knieß. "Die Chancen der europäischen Integration für die Mission". Evangelikale Missiologie 16 (2000) 4: kr. 122-133, hapa ni uk. 122. Makala haya hujumuisha kumbukumbu za hivi karibuni kabisa na vichocheo muhimu kwa Wakristo wa Ulaya [na Afrika].

[2] Agano la Kale hutumia vitenzi vinne na nomino moja iliyochukuliwa kutoka kwenye mmojawapo wa mizizi ya maneno hayo ili kuunda dhana tunayoiita 'tumaini'.

1. Tumaini Huhusisha Akili

Hoja: Tumaini si hisia zisizo na uhakika zilizokitwa kwenye mawazo au matarajio. Mungu hutuamuru Wakristo kutoa hesabu ya matarajio yetu: Kipi tunachotumaini, kwa nini na kwa namna gani?[3]

Kwa uwazi Petro anatarajia kanisa liyafikiri matumaini yake kupitia, "**Bali mtakaseni Bwana Mungu katika mioyo yenu: na mwe tayari daima kumjibu kila mtu awaulizaye sababu za tumaini lililo ndani yenu kwa unyenyekevu na kwa hofu**" (1 Pet. 3:14-15). Kabla ya kutoa hesabu kwa wengine, ni sharti kwanza tutoe hesabu ya nafsi zetu wenyewe. Tumaini halipingani na fikra, na fikra za kina haziwezi kuharibu tumaini. Hata hivyo, mafikirio yenye utambuzi na ya dhati hutofautisha kati ya tumaini la kweli na faraja nyepesi. Matokeo yake, Petro anaweza kusema juu ya sababu za tumaini letu.[4]

Kwa sababu maisha yetu kama Wakristo yanatakiwa kugeuzwa kwa upya wa kufikiri kwetu (Rum. 12:2), tunaweza tu kupata tumaini jipya pindi tunapoandaliwa kutiisha mtindo wetu wa mawazo ya kizamani kwa kuingiza mawazo mapya. Tunatakiwa kumwomba Roho Mtakatifu mara kwa mara kutuangazia fikra zetu. "**Pia naomba kwamba macho ya mioyo**[5] **yenu yatiwe nuru ili mweze kujua tumaini ambalo kwalo amewaiteni, yaani utajiri wa urithi wake wa utukufu kwa watakatifu**" (Efe. 1:18), hii humaanisha kuuelewa Utatu, yaani Baba, Yesu Kristo, na Roho (Efe. 1:17) kama Mungu mmoja, "**ili kwamba mpate kumjua yeye zaidi**". Tunasoma Biblia ili kujipatia tumaini kwa ajili yetu wenyewe na vilevile kwa ajili ya familia zetu, makanisa yetu na jamii yetu. "Kwa kuwa yote yaliyotangulia kuandikwa yaliandikwa ili kutufundisha sisi; ili kwa saburi na faraja ya Maandiko tupate kuwa na tumaini" (Rum. 15:4).

---

[3] Katika lugha nyingi, 'tumaini' humaanisha vitu vitatu tofauti: 1. kitendo cha kutumaini, yaani yaliyomo katika matarajio yangu na mtindo wa matarajio hayo. 2. mtendwa wa tumaini, yaani kile ninachokitumainia. 3. mtu au kitu ambacho kitatimiza tumaini langu. Kwa hiyo, kwa Wakristo ni: 1. tumaini katika mioyo yetu, 2. tumaini wa ajili ya wokovo, 3. tumaini katika Mungu, aufanyaye wokovu wetu.

[4] Kigriki: 'logon peri tes elpidos'.

[5] Katika Biblia, moyo ni kiini cha mawazo.

2. Tumaini ni Halisi kwa Wakristo – Imani na Tumaini Huwa Pamoja

Hoja: Tumaini ni halisi kwa Wakristo (Ebr. 3:6; Efe. 4:4), maana "imani ni kuwa na hakika ya kile tunachokitarajia na yakini ya kile tusichokiona" (Ebr. 11:1).

Hivyo, tumaini ni ungamo la awali la kila Mkristo, kwa kuwa, "**Basi tulishike kwa uthabiti tumaini tunalolikiri, kwa kuwa aliyeahidi ni mwaminifu**" (Ebr. 10:23). Daima Biblia husisitiza uhusiano wa karibu kati ya imani na tumaini, sawasawa na mifano miwili kutoka kwa Petro na Paulo. Akizungumza juu ya Yesu, Petro anasema, "**Kwa kupitia yeye mnamwamini Mungu, aliyemfufua kutoka kwa wafu na kumtukuza, vivyo hivyo hata imani yenu na tumaini lenu liwe kwa Mungu**" (1 Pet. 1:21), na Paulo hutukumbusha kwamba kwa njia ya Kristo "**tumepata njia ya kuifikia neema hii, ambayo kwayo, sasa tunasimama kwa njia ya imani. Na tunafurahi katika tumaini la utukufu wa Mungu**" (Rum. 5:2).

Petro hatuachii mashaka kwamba kuzaliwa upya – ambayo ni kazi ya Mungu inayotufanya sisi tuwe Wakristo – huzaa tumaini hai: "**Ahimidiwe Mungu na Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo! Katika rehema zake kuu ametupatia uzao mpya katika tumaini hai kupitia ufufuko wa Yesu Kristo kutoka kwa wafu**" (1 Pet. 1:3). Je, tumaini letu lililo hai haliwezi kuonekana zaidi duniani?

Wakristo barani Afrika wanahitaji kujifunza kukiri tumaini lao katika hali zote na kuyakumbusha makanisa yetu kuhusu tumani hili; si kujiondoa, hofu au kujificha ndiko kuwe ishara ya imani yetu. Hasa, watu wa Madhehebu ya Kiinjili sharti watangaze kwamba tumaini na kuzaliwa upya ni mambo yasiyotenganishwa – si katika nadharia tu bali pia katika maisha ya kila siku.

3. Tumaini Hujenga Umoja

Hoja: Ni tumaini linalowaunganisha Wakristo wote: Kwa sababu, "**Kuna mwili mmoja na Roho mmoja, kama mlivyoitwa katika tumaini moja wakati mlipoitwa**" (Efe. 4:4), Wakristo kamwe hawataweza kuimarisha umoja wao bila kuzungumzia tumaini lao la pamoja.

Wakristo barani Afrika ni sharti waungane katika tumaini lao na kuuonesha ulimwengu kwamba siyo sisi, wala kanisa letu wala taasisi zetu zinazounda tumaini hilo, bali ni upendo na neema ya Mungu vilivyodhi-

hirishwa katika Yesu Kristo. Mtu yeyote anayeushambulia umoja wa Ukristo anaunyang'anya ulimwengu tumaini lake.

4. Upendo Hujenga Tumaini – Tumaini Hujenga Upendo

Hoja: Upendo na tumaini havitenganishwi. Kwa sababu hii, Paulo anaweza"… kuikumbuka mbele za Mungu wetu na Baba yetu kazi yenu itokanayo na imani, kujishughulisha kwenu kunakosukumwa na upendo, na saburi yenu inayochochewa na tumaini lililo katika Bwana wetu Yesu Kristo" (1 Thes. 1:3). Mara kwa mara imani, tumaini na upendo hutajwa pamoja (1 Kor. 13:13. Angalia pia Kol. 1:5 na Gal. 5:5-6). "**Bwana wetu Yesu Kristo mwenyewe … aliyetupenda na kwa neema yake akatupatia faraja ya milele na tumaini jema**" (2 Thes. 2:16), ni upendo wa Mungu unaozaa tumaini, kwa kuwa, "**tumaini halitufadhaishi, kwa sababu Mungu amemimina pendo lake mioyoni mwetu kwa njia ya Roho Mtakatifu, ambaye ametupatia sisi**" (Rum. 5:5). Upendo huu ambao Mungu anatupatia sisi huunda tumaini kwa wengine, kwa kuwa upendo "**daima huvumilia, daima huamini, daima hutumaini, daima hustahimili**" (1 Kor. 13:7).

Kama Yesu anavyotueleza, jamii isiyokuwa na tumaini na isiyokuwa na Sheria ya Mungu huwa imepoa na haina upendo. "Kwa sababu ya kuongezeka maovu, upendo wa wengi utapoa" (Mat. 24:12). Uadui dhidi ya amri za Mungu ni uadui dhidi ya upendo.

Hakuna maandiko mengine mazuri yanayoeleza tatizo la msingi la Afrika ya sasa. Hakuna mtu anayeweza kukataa sheria za Mungu za uumbaji bila kuukataa upendo. Kamwe hatutaweza kabisa kurudisha upendo katika familia zetu, makanisa yetu, mahusiano ya ajira zetu, jamii zetu au serikali yetu mpaka tutakapoigeukia sheria ya Mungu. Ukosa-sheria daima huishia kwenye ukosa-upendo – kama hali yetu ya sasa inavyojidhihirisha wazi! Tangu miaka ya tisini tunaongelea sana upendo kuliko ilivyokuwa hapo awali, wakati uhalifu na chuki vikiendelea kuongezeka katika nyanja zote za maisha. Jamii yetu imesahau upendo wa kweli ni upi hasa! Kwa namna gani Afrika inaweza kujifunza tena upendo, wakati Wakristo hawaufundishi au kuuishi?

5. Mwanadamu Hawezi Kuishi bila Tumaini

Hoja: Tumaini ni muhimu kwa Uwepo wa Mwanadamu. "Tumaini ni kwa ajili ya uwepo wa mwanadamu kama oksijeni ilivyo kwa ajili ya mapafu. Pasipo oksijeni, mgonjwa hufa kwa ukosefu wa hewa. Pasipo tumaini, mtu husumbuliwa na msongo wa kukata tamaa, kupooza kwa bidii

ya mtu kiroho kunakotokana na hisia za kukosa maana, na za ubatili wa maisha" (Emil Brunner)[6].

Ustaarabu wa Afrika haujawahi kuwa na shaka juu ya ukweli huu, ingawa wengi wametafuta tumaini lao mahali pengine kuliko katika Baba wa Yesu Kristo. Plato anatoa maana ya tumaini kama, "matarajio ya kitu kizuri,"[7] hii ni maana halisi ya uwepo wa mwanadamu. Vipi kuhusu mwanafalsafa wa mlengo wa kushoto Ernst Bloch, aliyeandika kitabu maarufu kiitwacho, 'The Principle Hope' ('Tumaini Kuu')?[8]

Athari za tumaini zinaweza kuonekana katika aideolojia mbalimbali za Ulaya kama vile Umaksi[9] au Ujamaa wa Kitaifa[10]. Tumaini katika mafanikio ya baadaye ya mitazamo-dunia hiyo ya kidunia [yaani Umaksi na Ujamaa wa Kitaifa] huwapa ushawishi mkubwa sana na huwachochea watu kuyatoa maisha yao ili kufuata mitazamo hiyo. Zama Mpya, Uislamu, makundi ya vijana, na mipango ya vyama vya kisiasa, vyote huchota nguvu zao kutoka katika maono yao ya baadaye. Bila shaka yoyote kwa Biblia, ufunuo wake ni kweli, kwa kuwa Yeye aliyevuvia Maandiko ndiye Yule atengenezaye siku zijazo.

Tumaini, jambo ambalo ni sehemu ya heshima ya mwanadamu – yaani taswira [mfano] wa Mungu – ni haki ya binadamu na pia ni haki ya kuzaliwa ambayo watu wote tunawiwa kwa watu wengine wote. Haki hiyo hutupiliwa mbali tu endapo mtu atakataa kumwamini Mungu. Kila mtu ana dhana fulani kuhusu siku za usoni – Kwa ukweli, kulingana na kitivo cha Ulinganifu wa Masomo ya Kidini, kila dini ina maelezo fulani kuhusu historia ya dunia ya siku zijazo.

Mtu yeyote aishiye anaweza kuwa na tumaini na lazima afanye hivyo (Mhu. 9:4), lakini wafu hawawezi kabisa kuwa na tumaini (Mhu. 9:5-6) isipokuwa imani yao kwa Mungu huwaruhusu kutumainia ufufuo kutoka kwa wafu.[11]

---

6 Emil Brunner. op. cit., uk. 7.

7 Plato. Definitiones 416.

8 Ernst Bloch. Das Prinzip Hoffnung. 3 Vols. Suhrkamp: Frankfurt, 1982 (Toleo asilia 1954 1959, limechapwa mara kadhaa); The Principle Hope. Blackwell: Oxford, 1986.

9 Tazama Thomas and Christine Schirrmacher "Der Kommunismus als Lehre vom Tausendjährigen Reich". Factum 11+12/1986: kr. 12-19 and Thomas Schirrmacher. Marxismus – Opium für das Volk?. Schwengeler: Berneck, 1990[1]; VKW: Bonn, 1997[2].

10 Tazama Thomas Schirrmacher. "Die Religion des Nationalsozialismus: 14 Dokumente". Factum 11/1989: pp. 506-510; ders. "Adolf Hitler und kein Ende: Ausgewählte neuere Literatur zur Geschichte und Vorgeschichte des Nationalsozialismus". Factum 6/1989: pp. 252-255; ders. 'Das göttliche Volkstum' und der 'Glaube an Deutschlands Größe und heilige Sendung': Hans Naumann im Nationalsozialismus". 2 Vols. VKW: Bonn, 1992[1]; 2000[2].

11 Tazama hoja kuhusu ufufuo.

6. Kesho Hutegemea Leo

Hoja: Matarajio yetu au matumaini yetu ya baadaye huamua jinsi tufanyavyo leo. Wakati wa sasa wa kila mwanadamu hutegemea matarajio yake kwa siku zijazo.

Biblia hutupatia mifano ya kutosha ya maonyo, faraja na amri halisi kwa wakati wa sasa zinazochotwa kutoka katika ahadi za siku za usoni. Kama tukidai kuweza kufanya mambo bila matarajio ya siku za usoni, twajidanganya wenyewe, kwa kuwa moja kwa moja tunakubali mawazo ya jamii yetu. Pasipo kutarajia, waumini wengi hutafakari mitazamo ya wanasiasa na ya kwenye luninga zaidi kuliko mafundisho ya kibiblia. Mitazamo yetu wenyewe ya kutarajia mambo mabaya katika siku zetu za usoni, siku za usoni za kanisa letu au za ulimwengu wetu pia hutegemea mitazamo fulani kuhusu siku zijazo, ingawa hatuwezi kila wakati kufasili maana ya mawazo haya.

Kwa kuwa mitazamo yetu ya siku zijazo hushiriki jukumu muhimu katika mienendo yetu kuelekea muda kitambo ujao, ni muhimu kuuliza ni mtazamo wa nani, kuhusu ukweli, ulio sahihi zaidi. Tunaposhindwa kutengeneza mawazo thabiti, tunauacha uwanja kwa makundi ya kimadhehebu kama Mashahidi wa Yehova, ambao hutegemea sana mifumo yao maalumu ya mambo ya siku zijazo [mifumo ya kieskatolojia]. Kwa kweli, pindi uelewapo eskatolojia [mafundisho ya mambo yajayo au siku za mwisho], utakuwa umeelewa mafundisho ya dini yao. Jambo hili linaweza kusemwa pia kwa makundi mengi mapya yaliyogawanyika ambayo pia yapo katika kambi za Madhehebu ya Kiinjili. Ni lazima tutafute majibu ya uhakika kwa mavuguvugu hayo, ingawa tunahitaji kuvumilia kiwango fulani cha tofauti.

Maswali kuhusu siku za usoni hutegemea masuala makuu ya imani ya Kikristo, kama vile Kurudi kwa Kristo mara ya pili, Hukumu ya Mwisho na Ufufuo wa wafu; masuala yasiyotenganishwa kutoka kwenye asili na ofisi [huduma] ya Yesu. Kwa sababu hii, ni muhimu kutofautisha kati ya masuala ambayo Biblia inayajibu kwa ufasaha (kwamba Yesu anarudi tena kuwahukumu wanadamu wote), maswali ambayo Biblia inayajibu kwa sehemu tu, na masuala ambayo Maandiko hayajishughulishi nayo kabisa na ambayo huibuka tu wakati wanatheolojia wasisitizapo ili kukamilisha mfumo waliokwisha uanzisha. Uwazi huo pekee katika mafundisho yetu ndio utaweza kuzima mafuriko ya unabii wa uongo katika jamii ya madhehebu ya Kiinjili.

7. Tumaini Hujenga Siku Zijazo zilizo Halisi

Hoja: Kama Mungu asingetupatia siku zijazo, tusingekuwa na chochote. Kwa sababu tu Mungu hutuahidi siku zijazo, basi tuna siku zijazo. "Tena liko tumaini kwa siku zako za mwisho, asema BWANA" (Yer. 31:17).

Siku hizi zijazo siyo tu mwendelezo wa muda, bali ni kimo na kina cha historia ambayo huongoza kuelekea katika siku njema za mwisho. "**Maana naijua mipango niliyonayo kwa ajili yenu, asema BWANA, mipango ya kuwafanikisha na si ya kuwadhuru, mipango ya kuwapatia tumaini na kuwapatia siku za usoni**" (Yer. 29:11). Kila mtu anayechukua lengo la historia kama chanzo chake cha kuanzia na anayejumuisha hukumu ya mwisho ya Mungu atazingatia uhalisi wa siku za usoni katika ubora na vile vile katika wingi, "**kwa hakika hapa lipo tumaini la siku za usoni kwa ajili yako, na tumaini lako halitatupiliwa mbali**" (Mit. 23:18).

8. Tumaini si Ukokotoaji Tulivu, kwa kuwa Hushughulika na Mambo Ambayo Bado Hayajaonekana

Hoja: Nguvu ya tumaini la Kikristo ni imani na utegemezi wake kwa ulimwengu usioonekana. "Tumaini halina maana nyingine zaidi ya kutegemea na kusubiri mambo ambayo mtu hawezi kuyaona" (Martin Luther).

Luther alichota tamko hili kutoka kwenye maana ya imani katika Waraka kwa Waebrania. "**Basi imani ni kuwa na hakika ya kile tunachokitarajia na yakini ya kile tusichokiona**" (Ebr. 11:1). Paulo anaongezea, "**Kwa kuwa katika tumaini hili tuliokolewa. Lakini tumaini ambalo linaonekana si tumaini kabisa. Ni nani atumainiye kile ambacho anacho tayari? Lakini ikiwa twatumainia kile ambacho hatuna, twakitumainia kwa saburi**" (Rum. 8:24-25).

Ni ubora huu hasa unaolipa tumaini nguvu ya ukombozi ya mabadiliko ya kiroho ambayo wasio Wakristo hawawezi kuifahamu.

Mfumo wa tamaa ya vitu ambao umeanza kuota mizizi barani Afrika katika miongo iliyopita unaweza kujidhihirisha wenyewe katika muundo tofauti kuliko ule wa maeneo mengine, ingawa mizizi yake inafanana. Katika bara linaloghushiwa zaidi na mfumo wa tamaa ya vitu, ambapo wengi huamini yale tu wanayoweza kuyaona, kwa kiasi kikubwa watu huhitaji ujumbe kuwa tumaini la kweli linapatikana katika Mungu asiyeonekana, na kwamba maadili ya kweli hutoka ndani. Wakristo wa Afrika wanaweza kujifunza mengi kutoka kwa ndugu zao wa Ulaya ambao

tamaa ya vitu imewafanya kupoteza matumaini kabisa na imani kwa Mungu Mwumbaji.

TUMAINI KATIKA MUNGU PEKEE HALIPATIKANI KWA JITIHADA ZETU

9. Tumaini Hutegemea Neema na siyo Mafanikio

Hoja: Msingi wa Imani yetu hudhihirisha wazi kwamba mambo yote hutegemea neema ya Mungu na siyo mafanikio yetu, kwa kuwa mafanikio yetu ni chanzo cha yote tunayoweza kuyashughulikia na kuyafikia, na haya kwa urahisi hayatoshelezi kabisa kuleta mabadiliko ya kweli.

Kama Martin Luther alivyotamka, "Tumaini halitokani na matendo yetu mema. Matendo yetu mema hutokana na tumaini". Mafundisho ya kuhesabiwa haki kwa imani, ambayo Luther aliyafunua tena, ni msingi wa tumaini lisilotegemea matendo mema, "**ili, tukiisha hesabiwa haki kwa neema yake, tupate kuwa warithi tukiwa na tumaini la uzima wa milele**" (Tit. 3:7). Petro anashauri, "**mkiweka kikamilifu tumaini lenu juu ya neema mtakayopewa wakati Yesu Kristo afunuliwapo**" (1 Pet. 1:13) na waandishi wengine mara nyingi hutaja tumaini wakiliunganisha na neema (kwa mfano, 2 Thes. 2:6; Zab. 13:6, 130:7). Isaya anaomba, "**Ee BWANA, uwe mwenye rehema kwetu; twakungojea wewe. Uwe nguvu yetu kila asubuhi, na wokovu wetu wakati wa taabu**" (Isa. 32:2).

10. Tumaini Haliwezi Kupatikana kwa Kufanyiwa Kazi

Hoja: Tumaini hutegemea neema na siyo utauwa wetu au theolojia sahihi na bora kabisa, vilevile kwa kadri tunavyojitahidi kuishi na kufikiri katika njia ya kitauwa.

Rafiki wa Ayubu aitwaye Elifazi, anauliza, "Je, utauwa wako usiwe ujasiri wako na njia zako zisizo na lawama tumaini lako?" (Ayu. 4:6), lakini Ayubu, katika hali ya kukosa matumaini (Ayu. 17:13, 15), amejifunza kuweka tumaini lake kwa Mungu pekee.

Wakati Waraka kwa Waebrania unapozungumzia "**tumaini ambalo kwalo twajivuna**" (Ebr. 3:6), na wakati Paulo asemapo "**twafurahi katika tumaini la utukufu wa Mungu**" (Rum. 5:2), hawajisifu kwa ajili ya mafanikio yao wenyewe bali wanampa Mungu utukufu, na 'kujisifu' kwa kitu ambacho hawajakifanyia kazi kwa njia yoyote, na ambacho vilevile kinapatikana kwa wengine.

Hivyo, kwa namna yoyote tumaini ni zawadi ya Mungu ambayo ni kusudi la wokovu wetu. Mtu hawezi 'kujichumia [kufanya kazi ili

kujipatia]' tumaini, kwa kuwa, "Tumaini hutokea tu wakati Mungu awapo na huruma juu yetu na kuimimina mioyoni mwetu" (Martin Luther). "Tumaini lina msingi katika wema wa Mungu ulio safi na usioweza kupatikana kwa kuufanyia kazi, ambao uliahidiwa kwa neema, na unaoombwa na wale wasioustahili" (Martin Luther). Mtazamo wenye siha wa kutarajia mema katika ulimwengu wenye mateso, udhalimu, majanga angamizi, na kuanguka kwa maadili ni zawadi ya Mungu, ambayo sisi sote hatuna budi kuiomba [kwa Mungu].

11. Mungu Hatoi Tumaini tu; Yeye ni Sababu ya Tumaini Letu

Hoja: Mungu hatupi tu kitu cha kutumainia. Yeye mwenyewe ni kiini cha tumaini letu. "**Lakini sasa, Bwana, kipi ninachokitazamia? Matumaini yangu yako kwako**" (Zab. 39:7). Zaburi inalieleza jambo hili kwa uwazi zaidi. "**Maana umekuwa tumaini langu, Ee BWANA Mkuu, uliye ujasiri wangu tangu ujana wangu**" (Zab. 71:5); "**Ee nafsi yangu, tafuta mahali pa pumziko katika Mungu pekee, tumaini langu hutoka kwake**" (Zab. 62:5); "**Amebarikiwa yeye ambaye msaada wake ni Mungu wa Yakobo, ambaye tumaini lake liko katika BWANA Mungu wake**" (Zab. 146:5). Mara kwa mara Mtunga Zaburi anahusisha tumaini na uchaji wa Mungu (Zab. 33:18; 147:11; 62:6).

Kwa kuwa tu, sisi ni wa Mungu; na kwa sababu Yeye 'ni wa' kwetu, twaweza kutumaini kabisa. "**Naiambia nafsi yangu, 'BWANA ni sehemu yangu; kwa hiyo nitamngoja**'" (Omb. 3:24). Tunapaswa kutambua kwamba tumaini letu halitutegemei sisi, halitegemei mawazo yetu mazuri au mipango yetu au jitihada zetu na mapendeleo yetu, bali humtegemea Mungu, aliye Mtoaji wa mawazo hayo na mapendeleo hayo. Yeye ndiye msingi, lengo na yote yaliyomo katika tumaini letu; tumaini letu huendelea hata katika wakati wa utimilizaji wa ahadi zote za mbinguni, kwa kuwa Paulo anasema, "**Na sasa haya matatu yanadumu: imani, tumaini na upendo. Lakini lililo kuu kati ya haya ni upendo**" (2 Kor. 13:13), na hata katika wakati tutakapomwona Yesu uso kwa uso (1 Kor. 13:12).

12. Waovu Hawana Tumaini

Hoja: Moja ya matamko ya Biblia yanayotajwa sana kuhusu tumaini ni kwamba waovu hawana tumaini la kweli; isipokuwa ni tumaini la kufikirika tu na danganyifu.

Paulo anawakumbusha Waefeso juu ya maisha yao kabla ya kumjua Kristo, "**Zamani zile mlitengwa na Kristo, mkiwekwa kando mbali na uraia wa Israeli na wageni wa maagano ya ahadi, hamna tumaini na hamna Mungu duniani**" (Efe. 2:12). Wasioamini ni "wengine wasio na matumaini" (1 Thes. 4:13). Hitimisho lenye mantiki kwa waamini siyo kiburi, bali ni ushauri wa haraka wa kumtumaini Mungu peke yake, kwa kuwa "**Amelaaniwa mtu yule amtegemeaye mwanadamu, autegemeaye mwili kuwa nguvu zake na ambaye moyo wake umegeukia mbali kutoka kwa BWANA**" (Yer. 17:5).

Maandiko Zaidi ya Agano la Kale

1 Nya. 29:15 **Sisi tu wageni na wasafiri machoni pako, kama walivyokuwa baba zetu wote. Siku zetu duniani ni kama kivuli, pasipo tumaini.**

Ayu. 8:13 **Kama ilivyo hatima ya wote wamsahauo Mungu; ndivyo lipoteavyo tumaini la asiyemcha Mungu.**

Ayu. 7:6 **Siku zangu hupita upesi kuliko chombo cha kufumia, nazo zafika mwisho bila tumaini.**

Ayu. 11:20 **Lakini macho ya waovu yatashindwa, …**

Ayu. 19:10 **Hunibomoa pande zote mpaka ninapotoweka; na anang'oa tumaini langu kama mti.**

Ayu. 27:8 **Kwani ana tumaini gani mwovu pindi akatiliwapo mbali, wakati Mungu achukuapo uhai wake?**

Zab. 37:9 **Maana watu waovu watakatiliwa mbali, lakini wale wamtumainio BWANA watairithi nchi.**

Mith. 11:7 **Mtu mwovu afapo, tumaini lake hupotea; na yote aliyoyatarajia kutoka katika uwezo wake huwa kitu bure.**

Mith. 10:28 **Matarajio ya mwenye haki ni furaha, lakini matumaini ya mwovu huwa kitu bure.**

Mith. 11:23 **Matamanio ya mwenye haki huishia katika mema tu, lakini tumaini la mwovu huishia tu katika ghadhabu.**

13. Tumaini bila Mungu lina Udanganyifu

Hoja: Mwana mpotevu alijidanganya mwenyewe wakati alipoweka matumaini yake kwa rafiki zake. Pindi pesa zake zilipokwisha, na rafiki zake vilevile walipotea. Tumaini alililoliweka kwa Baba yake lilithibitisha kuwa ni lenye kutegemewa, kwa kuwa lilitegemea upendo badala ya utajiri (Luk. 15:11). Ni kwa jinsi gani twaweza kushukuru ya kwamba Baba yetu wa kweli aliyeko Mbinguni "**alitupenda na kwa neema yake akatupatia faraja ya milele na tumaini jema**" (2 Thes. 2:16).

Kwa sababu "**Mtu mwovu afapo, tumaini lake hupotea; na yote aliyoyatarajia kutoka katika uwezo wake huwa kitu bure**" (Mith. 11:7), mtu yeyote anaweza kufedheheshwa na kudhalilishwa endapo atawategemea wanadamu (Ayu. 41:1). Wakati mtu ategemeapo mataifa mengine, atagundua kuwa hayawezi kumsaidia (Omb. 4:17). Wakati jamii inapoharibika, "**twatazamia haki, lakini hakuna hata moja**" (Isa. 59:11) na "**tulitumainia amani lakini hakuna jema lililokuja**" (Yer. 14:19; Angalia pia Yer. 2:37).

14. Tumaini bila Mungu ni lazima Litafute Mbadala katika Uumbaji

Hoja: Tumaini katika Mungu na imani na kuamini katika Yeye kunaweza kuharibiwa tu kama mbadala utapatikana. Kwa kuwa hakuna Mwumbaji mwingine nje ya Uumbaji, basi mbadala huu unaweza kuwa ni sehemu ya Uumbaji, yaani waweza kuwa sanamu, wanadamu, malaika, asili au fedha.

Anguko linadhihirisha jambo hili kwa uwazi (Mwa. 3:1, 7). Katika wakati wetu wa sasa wa fikra za kutoegemea upande wowote, Hawa angeweza kumwambia nyoka, "Inawezekana, kwamba Mungu si wa kutegemewa, na hajatuambia ukweli. Vipi kuhusu wewe? Kama natilia mashaka neno la Mungu, ni lazima pia uniruhusu nawe nikulitilie mashaka. Siwezi kumwamini yeyote kwa wakati huu, lakini hebu subiri!" Hata hivyo, mazungumzo haya hayakufanyika, na hakufanya hivyo. Hawa angeweza tu kulitelekeza tumaini lake kwa Mungu kwa kumwamini Shetani. Asingeweza kumtilia mashaka Mungu bila kuamini kitu kingine chochote. Kutoegemea upande wowote hakuwezi kuwepo[12], iwe ni katika

[12] Ufupisho wa Heinrich Berger juu ya mtazamo wa Historia wa Calvin katika ; HeinrichBerger Studien zur Dogmengeschichte und Systematischen Theologie 6. Zwingli Verlag: Zürich, 1956, uk. 138 (Tazama pia kr. 138-139).

masomo ya ki-uhakiki au katika maamuzi ya kimaadili. Hawa asingeweza kusikiliza kwa urahisi pande zote mbili na kisha kusubiri matokeo, kwa kuwa alihitaji kuendelea kuishi, kufanya kazi na kuamua. Asingeweza kuamini au kutii pande zote mbili.

15. Hakuna Mbadala Uwezao Kuchukua Nafasi ya Mungu kama Msingi wa Tumaini, Hadharani au Faraghani, kama ilivyo katika Dini ya Mali (Mammon)

Hoja: Tumaini lolote ambalo hatimaye halina msingi kwa Mungu ni lazima lijithibitishe kuwa ni danganyifu, kwa kuwa linasimama juu ya kitu ambacho hakiwezi kutoa hakikisho na ambacho siku moja ki-tashindwa.

Hebu tuangalie jinsi Afrika inavyopenda fedha sasa na tuzingatie matokeo ya matumaini ya uongo iliyonayo kwa maisha ya kila siku. Katika Hotuba Mlimani, Yesu alisema, "Hakuna mtu awezaye kutumikia mabwana wawili; kwa maana atamchukia huyu, na kumpenda huyu; ama atashikamana na huyu, na kumdharau huyu. Hamwezi kumtumikia Mungu na Mali" (Mat. 6:24; Tazama pia Luk. 16:13). Muda mfupi kabla ya hili, alionya juu ya utumiaji wa maisha yetu kujilimbikizia hazina duniani, "kwa kuwa hazina yako ilipo ndipo utakapokuwepo na moyo wako" (Mat. 6:21; Tazama pia Luk. 12:34). Hii haikuwa sheria mpya, kwa kuwa Agano la Kale na Agano Jipya, yote yanapinga 'Mali ya udhalimu' (Luk. 16:9; neno la Kigriki humaanisha ama 'isiyo ya haki' au 'ovu'). Biblia hulinda mali za watu binafsi (kwa mfano, katika Amri Kumi), hutuambia tufanye kazi, na wakati mwingine huelezea amani na utajiri kama zawadi zitokazo kwa Mungu, lakini inaposisitiza kwamba "**mfanyakazi hustahili ujira wake**" (Luk. 10:7; Tazama pia 1 Tim. 5:18), si kwamba huruhusu tu mfanyakazi kufurahia mapato yake aliyoyapata kihalali, lakini pia huwapinga wale wanaoshindwa kumlipa [mfanyakazi] kwa kazi yake. Yakobo, nduguye Yesu, anaafiki kuwa: "**Angalieni, ujira mlioshindwa kuwalipa wafanyakazi waliovuna mashamba yenu unapiga kelele dhidi yenu. Vilio vya wavunaji vimefika masikioni mwa Bwana Mwenye uweza wote**" (Yak. 5:4. Tazama pia Yak. 5:1-6 na Kumb. 24:15)[13].

---

[13] Madai ya Karl Marx kuhusu Biblia ni ya kipumbavu. Kamwe Biblia haikukusudiwa kutumika kama, 'bangi kwa ajili ya watu' ili kuwazuia wasiweze kupinga mamlaka zitakazokuwepo. Sijapata kuona kitabu kitakatifu kingine kiwacho chote ambacho kwa ukali kabisa kinawapinga viongozi wajipatiao utajiri kwa njia zisizo za haki na kwa fujo [kama Biblia]. Kusema ukweli, Maandiko humhukumu kupita wengine wote mwumini asiye haki. Ili kuwa na hakika, maaskofu na viongozi wengi wa Kikristo wametiwa hatiani,

Yesu anatuambia, hakuna mtu atumikiaye mali, akaweza kumtumikia na Mungu kwa wakati mmoja. Biblia huchukulia kupenda fedha kama shina la maovu yote (1 Tim. 6:10). Zingatia kwamba siyo fedha, bali kupenda fedha ndicho chanzo cha dhambi nyingine. Maonyo ya Yesu kuhusu mali, muda wote yameshiriki jukumu muhimu katika maadili ya Kikristo. "Kwa msingi wa Amri ya Kwanza, ukinzani kati ya Mungu na mali hubainisha mawazo ya kiuchumi ya Luther."[14] Uchunguzi makini wa matamko ya Yesu katika Hotuba Mlimani hudhihirisha kwamba hayawalaumu wale waishio kwa ajili ya mali peke yake (au kama Marx angesema, waishio kwa ajili ya mtaji). Mali imeinuliwa kuwa dini, yaani imekuwa mpinzani dhidi ya imani ya Biblia juu ya Mungu. Kama Yesu asingetumia jina la mungu wa kipagani, tungelielewa jambo hili vizuri. Angeweza kusema, kwamba tunapaswa kuwa na Mungu mmoja tu. Ama tunaomba kwa Mungu wa Biblia au kwa 'Mammon' ('Mali'), lakini kama tujuavyo, 'Mammon' hairejei kwa mungu, bali kwa utajiri, fedha na mtaji. Katika Luk. 16:13, Yesu anarudia, "**Hamwezi kumtumikia Mungu na Fedha**" (Kwa Kigriki: "Mammon'), lakini mistari michache iliyotangulia (Luk. 16:9, 11) anatumia neno linaloelezea fedha zinazotumika katika biashara. Hivyo Dini ya Mali inaweza kuchukua mahali pa imani katika Mungu wa Biblia. Hii ndiyo sababu iliyomzuia kijana tajiri aliye kiongozi kumfuata Yesu, kwa kuwa alipenda sana utajiri wake kuliko Mungu (Mat. 19:16-30; Mk. 10:17-31; Luk. 18:18-30). Kijana huyu alikuwa amezishika amri zote isipokuwa ya Kwanza; "Usiwe na miungu mingine ila mimi". Ingawa dini ya fedha haina miungu, haina makuhani, wala haina hekalu (hakuna tunayoweza kuyaita mahekalu), ni dini inayomkana Mungu (a-theistic religion), dini isiyo na Mungu (Katika Kigriki: 'a'= 'bila, isiyo'; 'theos' = 'Mungu'). Je, Yesu analinganisha vitu viwili ambavyo havilinganishiki? Je, siyo kwamba Mungu ni suala la kidini na "Mammon" ("Mali") ni jambo la kiuchumi, kibiashara na la mtindo wa maisha?

Kamwe dini si jambo la kinadharia katika Biblia. Suala si kama vugu-vugu, falsafa, au mtindo wa maisha hujichukulia wenyewe kama dini au la, bali lile tukio la mwisho ambalo huamua tunu za maisha yetu ya kila siku katika uhalisia, na si tu katika nadharia. Zaidi ya yote, Maandiko hujihu-

---

na tena upingaji wa kijamii wa Biblia mara nyingi ulielekezwa kwa uongozi wa kidini ambao unawagandamiza watu wake wenyewe na kudharau msingi wa dini yao.

[14] Hans-Jürgen Prien. Luthers Wirtschaftsethik. Vandenhoeck & Ruprecht: Göttingen, 1992, p. 221 (Tazama kitabu kizima kuhusu umuhimu wa Mahubiri Mlimani kwa ajili ya maadili ya kiuchumi ya Luther). Pia tazama rejea mbalimbali kuhusu Mammon katika maandiko ya Luther. Martin Luthers Sämtliche Schriften, ed. by Joh. Georg Walch. Vol. 23. Verlag der Lutherischen Buchhandlung H. Harms: Groß Oesingen, 1986 (Kimerudiwa kuchapwa tangu 1910[2]), Col 1130-1132.

sisha na tumaini na imani katika Mungu wa Biblia. Suala si kama tunashawishika kwamba Mungu yupo, bali kama tunamtumaini Yeye katika maisha yetu. "**Waamini kwamba kuna Mungu mmoja. Vema! Hata mapepo huamini hivyo – na kutetemeka**" (Yak. 2:19). Katika Maagano yote, Agano la Kale na Jipya, neno 'amini' humaanisha 'kutumaini, kutegemea, kuchukulia kuwa ni cha uhakika', jambo ambalo hujumuisha tumaini. Kama tunamwamini Mungu, tunamchukulia kuwa ni wa uhakika kabisa, tunayachukulia kwa dhati mambo yote aliyoyasema na kuyafanya kama Mwumbaji na Mwokozi, na hupangilia maisha yetu sawasawa na uwepo wake na Sheria yake.

Dini ni kitu chochote kinachoshindana na tumaini hili la Biblia na imani hii. Ni kipi ninachokitegemea kabisa? Ni kipi kinachoyapa maisha yangu maana ya msingi? Ni kipi kinachotawala moyo wangu? Ni kipi kinachoamua maamuzi yangu? Ni nani mwenye neno la mwisho maishani mwangu? Lengo langu la mwisho ni lipi? Ni kipi nipendacho zaidi? Ni kwa namna gani ninahalalisha matamanio yangu?

Wakati fulani Ayubu alitambua haki ya Mungu ya kumhukumu yeye, "**Ikiwa nimeweka tumaini langu kwenye dhahabu au kuiambia dhahabu safi, 'Wewe ni usalama wangu**'" (Ayu. 31:24). Ingawa 'tumaini' na 'tegemeo'ni maneno ambayo yanaweza kutumiwa kwa Mungu tu, mara nyingi tunayatumia kurejea dini zilizofichika kama kukiri kwa Ayubu kunavyoonesha. Mithali hurudia wazo hili: "**Yeyote ategemeaye utajiri wake ataanguka**" (Mith. 11:28). Pia tungeweza kusema, "**Yeyote ategemeaye mali…**" Zaburi 49:6 huzungumzia "**wale wanaotumaini mali zao na kujisifia wingi wa utajiri wao**" (Tazama pia Zab. 52:7). Mara nyingi Biblia huielezea dini ya fedha kwa maneno yaleyale inayoyatumia kuelezea mahusiano ya mtu na Mungu.

Katika 1 Timotheo 6:17, Paulo anawasihi matajiri kutokuweka matumaini yao kwenye utajiri, "usio yakini" bali wayaweke kwa Mungu. Katika Waefeso 5:3-5, anaonya juu ya tamaa, na katika kukubaliana na Agano la Kale, anaongeza, "**kwa maana ni uabudu sanamu.**"

16. Vita dhidi ya Tumaini Bandia

Hoja: Mungu atafedhehesha matumaini ya uongo na anatutaka sisi tuyaweke wazi kiunabii.

Akiongea na Mungu, Ayubu anasema "**waangamiza tumaini la mwanadamu**" (Ayu. 14:19). Hata Wakristo wakati mwingine huongozwa na Mungu kuelekea hali zisizo na matumaini kabisa, ili wajifunze kusalimisha matumaini yao yoyote yale isipokuwa Mungu mwenyewe.

Yeremia, mwandishi wa kitabu cha Maombolezo, analia kwa sauti, "**Kwa nini umetutesa kiasi kwamba hatuwezi kuponywa? Tulitumaini amani lakini hakuna jema lililokuja, tulitumaini wakati wa uponyaji lakini kuna hofu tu**" (Yer. 14:19; Tazama pia Yer. 8:15).

Kwa sababu hii, moja ya wajibu muhimu wa manabii wa Agano la Kale ilikuwa ni kukataa matumaini bandia, iwe katika muundo wa miungu wa uongo, mashirikiano danganyifu ya kisiasa, ahadi za uongo za wafalme, au utabiri wa mambo mema yajayo wa manabii wa uongo. Hatupaswi kuwategemea wanadamu (Yer. 17:5; 48:13), kutegemea haki yetu wenyewe (Eze. 33:13), kutegemea alama za kidini kama vile Hekalu (Yer. 7:4), wala kutegemea sanamu (Hab. 2:18), bali kumtegemea Mungu pekee.

[Historia ya Ulaya imekuwa ikitengenezwa na nabii wa uongo kama Hitler na Stalin, na waongo wengine wengi wasiojulikana sana. Unabii unaofichua matumaini hayo ya uongo ni mojawapo ya wajibu muhimu sana wa makanisa ya Ulaya na waumini wa Ulaya; wajibu ambao tumekuwa tukishindwa kuutekeleza mara kwa mara].Ulimwenguni mwote na hata barani Afrika kuna manabii wengi sawa na Hitler na Stalin, na wengine wasiojulikana. Ni wajibu muhimu kabisa wa kanisa barani Afrika kutoa unabii unaofichua matumaini ya uongo ya manabii hawa. Cha kusikitisha ni kwamba mara nyingi, kanisa pote barani Afrika, limekuwa likishindwa kutekeleza wajibu huu ulio muhimu kabisa.

MUNGU HUTOA TUMAINI

17. Mungu Mwenyewe Daima Amekuwa Mtoaji wa Tumaini – Tangu Mwanzoni Kabisa mwa Historia

Hoja: Tumaini la dunia huanza kwa ukweli kwamba Mungu ndiye mmishenari wa kwanza.

Wakati wote Mungu amekuwa mmishenari wa kwanza. Muda mfupi tu baada ya Anguko, historia ya mwanadamu ilionekana kufika ukingoni kabla hata haijaanza kikamilifu, lakini Mungu hakuachilia mbali. Kwa neema, aliitembelea bustani ya Edeni (Mwa. 3:8-9), akiwatafuta Adamu na Hawa, na kuita, "Mko wapi? (Mwa. 3:9). Katika kutangaza hukumu inayokuja na ukombozi unaokuja (Mwa. 3:14-21), Yeye mwenyewe alitoa tumaini jipya kwa Uumbaji.

18. Mungu Mwenyewe Huleta Tumaini – katika Yesu

Hoja: Yesu ni kielelezo halisi cha mmishenari na mleta tumaini.

Yesu alitumwa duniani na Mungu. Kama mwanadamu alitakiwa kubeba adhabu yetu juu Msalaba ili kutengeneza na kutangaza wokovu wetu na hivyo kurudisha tumaini na siku za usoni kwa ulimwengu. Hata kabla ya Uumbaji Mungu alikuwa amekusudia (Efe. 1:4), sio kutuacha mpaka tuyafikie maangamizi ya dhambi, ambayo sisi wenyewe tumeyaleta juu yetu; bali kujituma yeye mwenyewe katika Kristo kama mmishenari kuja duniani ili kufanya siku za usoni zilizo halisi ziwezekane (Yoh. 3:16).

19. Mungu Mwenyewe Hutupa Tumaini – katika Roho Mtakatifu

Hoja: Pentekoste hutuonesha kwamba umishenari wa kiulimwengu katika nguvu ya Roho Mtakatifu ni alama iliyo muhimu zaidi ya kanisa la Agano Jipya, na kwamba Wakristo hawawezi kamwe kutumaini au kutangaza tumaini pasipo Yeye.

Mara zote Yesu aliwaamuru wanafunzi wake kusubiri ujio wa Roho Mtakatifu kabla ya kuanza kuyahubiri mataifa (Mk. 16:15-20; Mdo. 1:4-11). Roho alitakiwa kuja kama mrithi wa Yesu ili kuushawishi ulimwengu kwa Injili (Yoh. 16:7-11). Kwa ujio wake kwa Kanisa, Kanisa la Agano Jipya na umishenari wa kiulimwengu vilianza kwa pamoja. Bila yeye hakuna muundo wa misheni au mkakati wa kimishenari ambao ungekuwa na

matarajio ya mafanikio, kwa kuwa ni yeye pekee awezaye kuhakikisha hatia ya dhambi (Yoh. 16:7-10), awezaye kuongoza katika kumkubali Mungu na kazi ya wokovu ya Yesu Kristo, awezaye kuwapa uhai mpya wenye dhambi au kuwapa tumaini (Yoh. 3:5). Ni hakika Mungu amechagua kuwatumia wanadamu katika umisheni na anakusudia watumie akili zao kuwafikia wengine,[15] lakini mikakati hiyo yote ni ya kimasharti tu, kwa kuwa ni Mungu pekee anayeamua kama watafanikiwa au la (1 Kor. 12:4-6; Rum. 1:13).

Kipekee, Paulo anaendelea kusisitiza kwamba ni Roho Mtakatifu anayemimina tumaini katika mioyo yetu na ya kwamba tumaini letu hutegemea kabisa nguvu yake ya kushangaza. Ngoja nikupatie mifano mitatu. "**Na tumaini halitufadhaishi, kwa sababu Mungu amemimina pendo lake mioyoni mwetu kwa njia ya Roho Mtakatifu, ambaye ametupatia sisi**" (Rum. 5:5). "**Mungu wa tumaini awajaze ninyi furaha na amani yote kwa kuwa mnamtumaini yeye, ili mpate kufurikwa na tumaini kwa nguvu za Roho Mtakatifu**" (Rum. 15:13). "**Lakini kwa imani tunasubiri kwa hamu kupitia kwa Roho haki ambayo twaitumainia**" (Gal. 5:5).

20. Mungu Mwenyewe Hutupatia Sisi Tumaini – katika Kanisa, yaani Mbeba Tumaini

Hoja: Umishenari wa Kanisa umejengwa katika ukweli kwamba Mungu alijituma yeye mwenyewe kwanza ulimwenguni kama mmishenari ('Missio Dei').

Yesu aliwatuma wanafunzi wake ulimwenguni kuendeleza utume ambao yeye aliupokea kwa Baba yake (Mat. 10:40; Mk. 9: 37; Luk. 10:16; Mdo. 3:20, 26, takribani mara 50 katika Injili ya Yohana, tukianzia na Yoh. 3:17. Angalia pia Isa. 48:16), na ambao Roho Mtakatifu ameupokea kutoka kwa Baba na kwa Mwana (Yoh. 14:26; 15:26; Luk. 24:49). Katika Yohana 17:18 Yesu anamwomba Baba yake: "Kama vile ulivyonituma mimi ulimwenguni, nami vivyo hivyo naliwatuma hao ulimwenguni". Katika Yohana 20:21 anabadilisha tamko hilo kuwa lake na kulielekeza kwa wanafunzi wake, "**Yesu akawaambia tena, 'Amani iwe kwenu! Kama baba alivyonituma mimi, mimi nami nawatuma ninyi**" (Yoh. 20:21). Mungu Baba anamtuma Mwanawe na Roho wake kama wamishenari wa kwanza; Kanisa huendelea kuchukua huduma yao [yaani Yesu na Roho Mtakatifu] kwa njia ya umishenari wa kiulimwengu. Hivyo, jitihada za

[15] Kwa mfano Paulo anafanya mipango mingi ya kina na kuunda mbinu ya kijumla. Tazama Warumi 1 na 15 kwa mifano.

umishenari wa Kikristo umejengwa juu ya Mungu Mtatu. Kanisa la Kristo, kwa fasili, ni Mbeba tumaini, kwa kuwa utangazaji wake wa tumaini katika Injili ni mwendelezo wa moja kwa moja wa utume wa Mungu.

21. Kristo Ndani Yetu, Tumaini la Utukufu

Hoja: Kwa kuwa Mungu ni tumaini letu pekee, Kristo na kazi yake ya wokovu msalabani ndilo tumaini letu pekee. Akiwafikiria Wathesalonike, Paulo anaikumbuka "**mbele za Mungu wetu na Baba yetu kazi yenu itokanayo na imani, kujishughulisha kwenu kunakosukumwa na upendo, na saburi yenu inayochochewa na tumaini lililo katika Bwana wetu Yesu Kristo**" (1 Thes. 1:3).

Wakristo ni wa "**Kristo Yesu aliye tumaini letu**" (1 Tim. 1:1) na Kristo yu ndani yetu, kwa kuwa Paulo anaandika, "**Kwao hao Mungu amechagua kuujulisha utajiri wa utukufu wa siri hii katikati ya mataifa, ambayo ni Kristo ndani yenu, tumaini la utukufu**" (Kol. 1:27).

Tumaini katika Kristo haliko tu ndani yetu; tunasubiria utimilifu wake halisi, wa kihistoria na wa kibinafsi "**wakati tukisubiria tumaini lenye baraka – yaani mwonekano wenye utukufu wa Mungu wetu Mkuu na Mwokozi, Yesu Kristo**" (Tit. 2:13).

22. Tumaini kupitia Msalaba

Hoja: Tendo la Mungu la ajabu zaidi, lililo msingi wa matumaini yote ya kweli, lilikuwa ni kifo cha Kristo msalabani pale Gorigotha, pale alipokufa kwa niaba yetu ili kushinda mauti, dhambi na Shetani, ambao ni maadui wa kudumu wa matumaini yote. Kwa sababu hii, hakuna uwezekano wa kuwepo kwa tumaini la mwanzo mpya pasipo msamaha.

Ukweli wa kiulimwengu kuwa tumaini la siku zijazo hutegemea msamaha ni la kweli katika hali mahususi. Ni katika kusameheana sisi kwa sisi tu, twaweza kuutumaini mwanzo mpya.

Kwa mfano, Waislamu hawana mafundisho ya dhambi ya asili au dhambi ambayo ni uharibifu wa mahusiano ya mwanadamu na Mungu; hawana mafundisho ya upatanisho au msamaha. Kwa Waislamu upatanisho katika maisha binafsi au kati ya mataifa ni vigumu kufikiwa, kwa kuwa makosa ya nyuma bado yanaweza kuendelea kuibuliwa katika karne zijazo.

Iwe walimwamini Mungu mpatanishi katika maisha yao binafsi au la, Konrad Adenauer na Charles de Gaulle, kama wawakilishi wa mataifa yao, walitenda katika roho ya ustaarabu iliyoathiriwa sana na imani ya

Kikristo, wakati walipozipatanisha Ujerumani na Ufaransa na wakaamua kuanza mahusiano mapya kinyume cha udhalimu mbaya uliokuwepo hapo nyuma.

Askofu Desmond Tutu alishiriki sana katika kupigania haki za Waafrika barani Afrika, na hata haki za Waafrika nchini kwake wakati wa ubaguzi wa rangi. Pamoja na madhara makubwa ya ubaguzi wa rangi yaliyoleta chuki mbaya miongoni mwa raia wa nchi hiyo, alishiriki sana katika kuleta upatanishi na msamaha miongoni mwa raia wa nchi hiyo baada ya uhuru. Ni roho ya msamaha na upatanishi iliyoathiriwa kabisa na Ukristo iliyokuwa ndani yake. Uislamu hauna kitu cha kulinganishwa na hilo.

Kama Afrika inahitaji kutafuta tumaini jipya, Makanisa ulimwenguni na waumini wao ni lazima kusameheana kila mmoja na mwenzake na kupatana. Kama Afrika inahitaji kutafuta tumaini jipya, familia ulimwenguni ni lazima kusameheana na kupatana. Kama Afrika inahitaji kutafuta tumaini jipya na siku njema zijazo, 'jamii' na mataifa barani Afrika ni lazima kusameheana na kupatana. Zaidi ya yote, tunatakiwa kivitendo kuonesha msamaha kwa Waislamu. Sababu ni kuwa imani yao na utamaduni wao haujui lolote kuhusu msamaha, kuhusu kusahau majeraha yaliyopita ili kuingia katika kipindi kipya cha mapatano na kustahimiliana. Ushuhuda wetu hauna thamani kwao kwa kadri tutakavyoendelea kutoonesha msamaha kivitendo, na kuwaonesha kwamba msamaha humaanisha kuachilia mikononi mwa Mungu makosa na dhambi zilizopita. Je, ndoa za Kikristo zina tumaini lililokitwa katika msamaha na mapatano? Je, roho ya upatanisho na msamaha inaweza kuonekana katika makanisa yetu ili tuwe na mamlaka na mguso, au tunaongozwa tu na wasiwasi, tetesi, uhasama mkubwa wa zamani, ghasia za makundi ya watu na makwaruzano, kama taasisi nyingine zilivyo?

23. Tumaini la Kurudi kwa Yesu Mara ya Pili na Ufufuo wa Wafu

Hoja: Tumaini la Kikristo limeelekezwa katika Ujio wa Yesu Mara ya Pili na Ufufuo wa Wafu. Si kwa bahati, Imani ya Mitume inamalizikia na maelezo mengi kuhusu siku zijazo. Imani ya Kikristo si kuamini tu juu ya Mwumbaji mwenye Uweza Wote, bali pia ni imani katika kazi zake za wokovu katika historia ya mwanadamu iliyopita na ijayo.

Wakati Ujao katika Imani ya Mitume
(Umechapwa katika herufi za mlazo)

Namwamini Mungu Baba Mwenyezi,
Muumba wa Mbingu na Nchi,
na Yesu Kristo
Mwana wake pekee Bwana wetu;
aliyechukuliwa mimba kwa uweza wa Roho Mtakatifu,
akazaliwa na bikra Mariamu,
akateswa zamani za Pontio Pilato
akasulubiwa, akafa, akazikwa,
akashuka mahali pa wafu,
siku ya tatu akafufuka ***(kutoka kwa wafu)****;*
akapaa mbinguni;
ameketi mkono wa kuume
wa Mungu Baba Mwenyezi;
kutoka huko atakuja
kuwahukumu walio hai na wafu.
Namwamini Roho Mtakatifu;
na Kanisa takatifu ya waamini wote;
na ushirika wa watakatifu;
na ondoleo la dhambi;
na kiyama ya mwili
na uzima wa milele. Amina.

Kutokana na msimamo huu wa wakati mkuu ujao, umuhimu wa wakati wetu mdogo ujao unaongezeka.

Paulo na Tumaini la Ufufuo

Mdo. 24:15 **na mimi nina tumaini hilohilo kwa Mungu sawa na watu hawa, kwamba kutakuwa na ufufuo wa wenye haki na waovu.**

Mdo. 26:6 **Na sasa ni kwa sababu ya tumaini langu katika kile ambacho Mungu amewaahidia baba zetu niko mbele ya hukumu leo.**

Mdo. 26:7 **Hii ni ahadi ambayo makabila yetu kumi na mawili yanatumainia kuiona ikitimilika kadri wanavyoendelea kumtumikia Mungu kwa uaminifu mchana na usiku. Ee Mfalme, ni kwa sababu ya tumaini hili Wayahudi wananishtaki mimi.**

Mdo. 28:20 **Kwa sababu hii, nimeomba kuwaona na kuongea nanyi. Ni kwa sababu ya tumaini la Israeli kwamba ninafungwa kwa mnyororo huu.**

1 Thes. 4:13 **Ndugu, hatutaki mwe wajinga juu ya wale waliolala mauti, au mhuzunike kama hao watu wengine wasio na tumaini.**

MUNGU NI WA KUAMINIKA

24. Tumaini Letu kwa Mungu ni Thabiti, kwa sababu Mungu ni wa Kuaminiwa

Hoja: Tumaini katika Mungu ndilo lenye uhakika wa kweli, kwa sababu ni Mungu pekee aliye wa milele, asiyebadilika, mwenye uweza wote, mwenye haki, mwenye hekima na mwenye upendo.

Kama Baba wa Kanisa aitwaye Chrysostomos alivyowahi kusema, Imani ya Kikristo ni yenye uhakika kamili, kwa kuwa mwanzilishi wake huishi milele.[16] Yeremia aliweka tumaini lake katika Uumbaji wa Mungu, "**Je, kuna yeyote miongoni mwa sanamu za mataifa huleta mvua? Je, mawingu yenyewe huishusha mvua? La hasha, ni wewe, Ee BWANA Mungu wetu. Kwa hiyo tumaini letu liko kwako, kwa kuwa wewe ni yule afanyaye vitu vyote**" (Yer. 14:22).

25. Tumaini ni Jambo la Hakika kwa sababu ya Uaminifu wa Mungu na Ahadi Yake

Hoja: Tumaini ni jambo la hakika kwa sababu lina msingi katika ahadi za Mungu ambazo ni za kuaminiwa, kwa sababu Mungu mwenyewe amejifunga kuzitunza.

Martin Luther aliandika, "Rehema ya Mungu, ambayo huahidi kupitia Neema, na katika Kweli, ambavyo hutimiza ahadi, ni vyanzo vya tumaini."

Katika ulimwengu wa Kigriki wa kisekyula, familia ya neno 'tumaini' hujumuisha aina zote za matarajio kama vile woga, hofu, tumaini, matakwa na mahitaji. (Kwa mfano: 'Ninatumaini kwamba hali ya hewa itakuwa nzuri kesho!') Maneno haya yana maana sawa katika maisha ya kila siku katika baadhi ya maandiko, kwa mfano, wakati Paulo anapopanga kutembelea baadhi ya makanisa (kwa mfano, Rum. 15:24; 1 Kor. 16:7; Flp. 2:23; 1 Tim. 3:14).

Hata hivyo, tumaini la imani si hisia zisizo wazi kuhusu siku zijazo. Ni hakikisho lililokitwa juu ya uaminifu wa Mungu wa kutumainiwa kabisa. "**Basi tulishike kwa uthabiti tumaini tunalolikiri, kwa kuwa aliyeahidi ni mwaminifu**" (Ebr. 10:23). Kinyume na methali ya Kijerumani, "Kutumainia na kungojea huunda wapumbavu wavumilivu,"[17] Paulo anatuambia,

---

[16] Homilie, Ch. 5.

[17] 'Hoffen und Harren hält manchen zum Narren'.

"**Na tumaini halitufedheheshi**" (Rum. 5:5). "**Kisha utajua kuwa mimi ni BWANA; wale wanaonitumaini mimi hawatafedheheshwa**" (Isa. 49:23).

Ni jambo lisilokubalika kiakili wala lisilowezekana kwa Mungu kusema uongo. Imani yetu na ufahamu wetu huwekwa "**kwenye tumaini la uzima wa milele, ambalo Mungu, asiyeweza kusema uongo, aliliahidi tangu kuanza kwa wakati**" (Tit. 1:2).

26. Tumaini Letu Limejengwa juu ya Msingi wa Kiapo cha Mungu

Hoja: Tunaweza tu kumtegemea Mungu kikamilifu, kwa sababu amejifunga mwenyewe kwa kiapo katika Agano lake.

Tofauti na Mungu wa Uislamu, Mungu ameapa: "**Mungu alifanya hivyo ili, kwa vitu viwili visivyoweza kubadilika, ambavyo katika hivyo haiwezekani Mungu kusema uongo, sisi tuliokimbilia kushika tumaini lililotolewa kwetu tuweze kufarijiwa sana**" (Ebr. 6:18).

Baadhi husema, kuapa ni muhimu tu pale mtu anapohitaji kukwepa kusema ukweli! Lakini kama tukisisitiza kwamba kuapa si muhimu, kwa kuwa twapaswa kusema ukweli kila siku; basi ni lazima tueleze kwa nini Mungu, ambaye kamwe hasemi uongo, mara kwa mara anaapa viapo (kwa mfano, Mwa. 22:16; Mik. 7:20; Kut. 6:8; Eze. 20:5; Zab. 95:11). George Giesen[18] amehesabu viapo themanini na mbili vilivyofanywa na Mungu katika Agano la Kale, ambayo ni 38% ya viapo vyote vilivyotajwa. Mbali na hivyo, Mungu alifanya viapo kadhaa vilivyobuniwa kwa maneno mengine. Mungu hutunza amri zake mwenyewe kwamba viapo vyote lazima viapwe kwa jina lake kwa kuwa "**Mungu alipompa ahadi yake Ibrahimu, kwa kuwa hakukuwa na yeyote aliye mkuu kuliko yeye wa kumwapia, alijiapia kwa nafsi yake mwenyewe**" (Ebr. 6:13).

Mungu anaapa kwa nafsi yake mwenyewe

Mwa. 22:16 akasema, Nimeapa kwa nafsi yangu asema BWANA, kwa kuwa umetenda neno hili, wala hukunizuilia mwanao, mwanao wa pekee.

Ebr. 6:13 **Kwa maana Mungu alipompa ahadi yake Ibrahimu, kwa kuwa hakukuwa na yeyote aliye mkuu kuliko yeye wa kumwapia, alijiapia kwa nafsi yake mwenyewe.**

[18] Georg Giesen. Die Wurzel sb' „schwören": Eine semasiologische Studie zum Eid im Alten Testament. Bonner Biblische Beiträge 56. Peter Hanstein: Königstein, 1981.

Yer. 44:26 **Basi, sikia neno la BWANA, enyi Wayahudi wote muishio Misri: 'Naapa kwa jina langu lililo kuu,' asema BWANA, 'kwamba hakuna hata mmoja kutoka katika Yuda aishiye mahali popote humu Misri atakayeliitia jina langu au kuliapia,' kwa hakika kadri BWANA aliye Mkuu aishivyo.**

Amo. 6:8 **BWANA aliye Mkuu ameapa kwa nafsi yake - Mungu wa Uweza Wote asema: "Nachukia fahari ya Yakobo, nachukizwa na ngome zake; nitautoa mji huo, pamoja na vyote vilivyomo ndani yake.**

Kut. 32:13 Mkumbuke Ibrahimu, na Isaka, na Israeli, watumishi wako, ambao uliwaapia kwa nafsi yako, na kuwaambia, Nitazidisha kizazi chenu mfano wa nyota za mbinguni; tena nchi hii yote niliyoinena nitakipa kizazi chenu, nao watairithi milele.

Amo. 4:2 Bwana Mungu ameapa kwa utakatifu wake, ya kuwa, tazama, siku zitawajilia, watakapowaondoa ninyi kwa kulabu, na mabaki yenu kwa ndoana.

Kumb. 32:40 Maana, nainua mkono wangu mbinguni, Na kusema, Kama mimi niishivyo milele.

1 Sam. 2:30 **Kwa hiyo, BWANA, Mungu wa Israeli asema, 'Niliahidi kuwa nyumba yako na nyumba ya baba yako zitahudumu mbele yangu milele.' Lakini sasa BWANA asema: 'Jambo hili liwe mbali nami! Wale wanaoniheshimu nitawaheshimu, lakini wale wanaonidharau watadharauliwa'.**

Rum. 14:11 **Imeandikwa: "'Kwa hakika kadri niishivyo,' asema Bwana, 'kila goti litapigwa mbele zangu, na kila ulimi utamkiri Mungu'.**

"Kwa nafsi yangu nimeapa" (Isa 45:23; Yer 22:5; 49:13).

"Kama niishivyo (=Kwa hakika kadri niishivyo)" (Hes. 14:21, 28; Kumb. 32:40; Isa. 49:18; Yer. 22:24; 46:18; Eze. 5:11; 14:16,18,20; 16:48; 17:16,19; 18:3; 20:3,31,33; 33:11,27; 34:8; 35:1,6; Zef. 2:9; Rum. 14:11

Kiapo cha Mungu, ambacho kwa hicho Yeye hujifunga mwenyewe katika Agano lake, ni muhimu katika imani ya Kikristo. Huwa tunashindwa kulitambua hili, kwa sababu hatufahamu kabisa maana ya kiapo, au kwa sababu hatuko makini na tofauti muhimu iliyopo kati ya Mungu wa Biblia na miungu wa dini nyingine. Katika Uislamu Mungu ni mkamilifu

sana, mwenye enzi na mwenye kujitegemea, kiasi kwamba asingeweza kujitoa mwenyewe kikamilifu kwa mwanadamu yeyote, kwa kuwa jambo hili lingemfanya kuwa chini ya uamuzi wa mwanadamu. Hata anapoahidi, Allah anabaki na haki ya kubadilisha mawazo yake, bila mtu yeyote kuweza au kuwa na ujasiri wa kumhukumu.

Mungu wa utamaduni wa Kiyahudi na Kikristo kwa usawa uleule ni mkamilifu sana, mwenye enzi na mwenye kujitegemea. Hakuna mtu yeyote wa kumkataza kubadilisha mipango yake au kumlazimisha kutunza ahadi zake. Kamwe si Mwanadamu au Uumbaji unaoweza kumwekea Mungu mipaka, bali yeye mwenyewe amejifungamanisha na neno lake na ameapa kwa Jina lake mwenyewe kulitunza. Mungu ni mwaminifu na wa kuaminiwa kabisa. Tofauti na Allah, enzi yake inajieleza yenyewe katika ukweli kwamba hakuna mtu wa kumlazimisha kutimiza mipango yake, kuheshimu viapo vyake au kutunza ahadi zake. Ni kweli, anatuamuru tumpime kulingana na maneno yake mwenyewe na 'kumpeleka mahakamani' (Isa. 1:18; 41:1; 43:26; Mal. 3:10), lakini mwanadamu kamwe hatapata kosa lolote kwake.

Uaminifu wa Mungu hutuongoza kwenye tumaini, au kama ambavyo huwa tunaeleza, hutuongoza kwenye imani, ambayo ni mojawapo ya maelekezo matatu muhimu yanayojulikana (imani, upendo na tumaini; Tazama Hoja ya 2) ya mahusiano yetu na Mungu – si jambo la bahati.

Kama Mungu mwenyewe na Yesu mwenyewe wanaapa zaidi ya mtu mwingine yeyote, basi kusudi la kuapa haliwezi kuwa ni kutofautisha kati ya ukweli na kile kisicho kweli. Mungu anaapa zaidi ya mtu awaye yote, na watu mashuhuri wa imani katika Biblia wanafuata mfano wake. Inawezekanaje ukweli wa tamko utiliwe mashaka, wakati Mungu anapokuwa kasema?[19] Mwandishi wa Waraka kwa Waebrania anaelezea kiapo cha Mungu kwa Ibrahimu kwa maneno yafuatayo: "**Wanadamu huapa kwa yeye aliye mkuu kuliko wao, na kiapo huthibitisha kile kilichosemwa na huyafikisha mwisho mabishano yote. Kwa sababu Mungu alitaka ku-**

[19] Tukifikiri kwamba Yesu alikuwa akitetea mtazamo wa kiapo wa Agano la Kale dhidi ya utendaji wa Waandishi na Mafarisayo, ambao waliapa kwa kutumia kila kitu isipokuwa Mungu, basi Hotuba Mlimani haihukumu viapo vyote, bali vile tu vilivyozuiliwa katika Agano la Kale. Katika Mathayo 5:34-35, Yesu anasema, "**Msiape kabisa kwa Mbingu … au kwa dunia.**" Yakobo 5:12 huelezea wazo hili hili: "**Kamwe msiape kwa mbingu wala kwa dunia.**" Kikitafsiriwa vema, kifungu kinapaswa kusomeka: "**Lakini nawaambieni ninyi: Msiape kabisa kwa mbingu, kwa kuwa ni kiti cha enzi cha Mungu, wala kwa dunia, kwa sababu ni mahali pa kuwekea miguu yake, wala kwa Yerusalemu, kwa kuwa huo ni mji wa Mfalme mkuu, wala ninyi msiape kwa kichwa, kwa kuwa hamwezi kuufanya hata unywele mmoja kuwa mweupe au mweusi. Acheni maneno yenu yawe Ndiyo, ndiyo! au Hapana, hapana! Chochote zaidi hutoka kwa yule Mwovu**" (Mat. 5:34-37).

liweka wazi kwa warithi kusudi lake la asili lisilobadilika juu ya kile kilichoahidiwa, akalithibitisha kwa kiapo. Mungu alifanya hivyo ili, kwa vitu viwili visivyoweza kubadilika, ambavyo katika hivyo haiwezekani Mungu kusema uongo, sisi tuliokimbilia kushika tumaini lililotolewa kwetu tuweze kufarijiwa sana." (Ebr. 6:16-18). Hivyo, tegemeo la milele la uamuzi wa Mungu hutegemea kiapo chake, kwa kuwa hulifanya agano kuwa hitimisho na lisilobadilika. Si kila tamko lililofanywa na Mungu halibadiliki: mara ngapi amebatilisha hukumu aliyoitangaza, kwa sababu ya mwenye dhambi kutubu! Hukumu hazikuweza kukwepeka tu, endapo Mungu alizitangaza chini ya kiapo. Viapo vya kibinadamu vina maana ile ile: tofauti kati ya ahadi na kiapo ni kwamba, ahadi inaweza kubadilishwa kulingana na mazingira. Kiapo huweka utofauti kati ya mapenzi na ndoa, kwa kuwa ndoa ni agano linalofanywa kwa kiapo.

Hebu turudi kwenye kuaminiwa kwa tumaini la Mungu. Kulingana na Waebrania 7:20-21, ukuhani wa Walawi wa Agano la Kale haukukitwa kwenye kiapo, wakati ambapo ukuhani wa milele wa Yesu ulio kwenye mfumo wa Melkizedeki ulikitwa kwenye kiapo kilichofanywa na Mungu katika Zaburi 110:4: "**Bwana ameapa na wala hatabadili mtazamo wake: "Wewe ndiwe kuhani milele, kwa mfumo wa Melkizedeki.**" Waebrania 7:20-22 hutuambia, "**Na haikuwa pasipo kiapo! Wengine walikuwa makuhani pasipo kiapo, bali yeye alikuwa kuhani kwa kiapo wakati Mungu alipomwambia: "Bwana ameapa na wala hatabadili mawazo yake: 'Wewe ndiwe kuhani milele.'" Kwa sababu ya kiapo hiki, Yesu amekuwa mdhamini wa agano lililo bora zaidi**" (Ebr. 7:20-22). Ukuhani wa Walawi ungeweza kufikia mwisho, kwa sababu Mungu alikuwa hajatoa hakikisho la uwepo wake wa milele kwa kiapo, lakini ukuhani wa Yesu kamwe hautakwisha, kwa kuwa uhalali wake wa milele umetiwa muhuri kwa kiapo.

27. Tumaini Humaanisha Kazi

Hoja: Usalama wa tumaini letu hauturuhusu kupumzika katika ndoto za wakati ujao, bali hututaka tujitahidi kuthibitisha imani yetu.

"**Twataka kila mmoja wenu kuonesha jitihada ileile hadi mwisho, ili kulifanya tumaini lenu kuwa la hakika**" (Ebr. 6:11). Paulo anawasihi waumini "**… kuendelea katika imani yao, iliyoimarishwa na iliyo thabiti, kwa kutoyumbishwa mbali na tumaini lililo katika injili**" (Kol. 1:23).

28. Tumaini Hujengwa kwenye Neno la Mungu

Hoja: Kwa sababu Mungu, ambaye ni mwaminifu kabisa, kajifunga mwenyewe – katika maandiko[20] – Neno lake ni msingi wa kutegemewa wa tumaini letu.

Mtunga Zaburi anakiri mbele ya watu, "**Ninamngoja BWANA, nafsi yangu yamngoja, na katika neno lake nitaweka tumaini langu**" (Zab. 130:5), na mbele za Mungu, "**Wale wote wakuchao wafurahi wanionapo, kwa kuwa nimeweka tumaini langu katika neno lako**" (Zab. 119:74); "**Usiliondoe neno la kweli kinywani mwangu, maana nimeweka tumaini langu katika sheria zako**" (Zab. 119:43); "**Wewe ni kimbilio langu na ngao yangu; nimeweka tumaini langu katika neno lako**" (Zab. 119:114). Baada ya Yesu kuupata uzima wa milele kwa ajili yetu, Paulo anaurudia ukweli huu wa Agano la Kale kwa kuzungumza juu ya imani na ukweli "**… ambao huchipuka kutoka kwenye tumaini ambalo limehifadhiwa kwa ajili yenu huko mbinguni na ambalo mmekwishalisikia tayari katika neno la kweli, yaani injili**" (Kol. 1:5).

Ngoja nirudie: Wakristo husoma Biblia ili kutafuta tumaini kwa ajili yao wenyewe, kwa ajili ya familia zao, kwa ajili ya makanisa yao, na kwa ajili ya jamii yao. "**Kwa kuwa kila kitu kilichoandikwa hapo zamani kiliandikwa kutufundisha, ili kupitia uvumilivu na utiaji moyo wa Maandiko tuweze kuwa na tumaini**" (Rum. 15:4).

Wakristo barani Afrika ni lazima watangaze kwamba makanisa na waumini wanaokataa neno la Mungu kuwa si la kuaminiwa au halilingani na mazingira yetu hawaziibii tu nafsi zao tumaini pekee la kuaminiwa kabisa bali pia huliibia bara hili tumaini hilo. Mungu hapendi tutegemee matarajio yasiyo dhahiri, bali ametupatia ahadi thabiti katika neno lake lililoandikwa. Matumaini danganyifu ya wanatheolojia kinzani ni lazima yawekwe wazi (hususani katika bara la Afrika, zaidi ya sehemu nyingine yoyote duniani). Makanisa mengi ya Afrika hukata tamaa, kwa sababu hayawezi kujua nini cha kukitumainia! Bila Biblia, hayatajua kamwe!

---

[20] Ibara ya 1.1 ya Ukiri wa Westminster (Westminster Confession): "kwa hiyo ilimpendeza Bwana, kwa nyakati mbalimbali, na katika mitindo mbalimbali, kujifunua mwenyewe, na kutangaza kuwa makusudi yake kwa Kanisa lake; na baadaye, kwa ajili ya uhifadhi na usambazaji bora wa ukweli na kwa uhakika zaidi uimarishaji na faraja ya Kanisa … kuyaweka hayo yote katika maandishi." G. I. Williamson. The Westminster Confession of Faith for Study Classes. Philadelphia, Pennsylvania: Presbyterian and Reformed Publishing Company, 1964.

29. Tumaini letu lina Msingi katika Utendaji Kazi wa Mungu – si katika Mihadhara

Hoja: Tumaini letu halitegemei nadharia au makusudio ya kiungu, bali katika utendaji kazi wa Mungu. Katika Biblia tumaini na upendo haviwezi kamwe kufafanuliwa hadi mwisho kwa maneno au hisia, bali huelezwa kwa vitendo daima. Paulo anazungumza juu ya "**imani inayojieleza yenyewe kupitia upendo**" (Gal. 5:5-6). 1 Yohana 3:17 inatuonya, "**Lakini mtu yeyote akiwa na umiliki wa mali na anamwona nduguye akiwa katika uhitaji lakini hamwonei huruma, yawezekanaje upendo wa Mungu kuwa ndani yake? Watoto wapendwa, tusipende kwa maneno au kwa ulimi bali kwa matendo na katika kweli.**"

Yohana ameweka msingi wa amri yake katika huduma ya Yesu, "**Hivi ndivyo tuwezavyo kujua upendo ni nini: Yesu Kristo aliyatoa maisha yake kwa ajili yetu. Nasi twapaswa kuyatoa maisha yetu kwa ajili ya ndugu zetu**" (1 Yoh. 3:16). Upendo wa Yesu unaweza kuonekana katika mwenendo wake. Kifo hiki ni uthibitisho wa upendo wa Mungu (Rum. 5:8; Yoh. 3:16; Efe. 5:25). Waume wanapaswa kudhihirisha upendo wao kwa wake zao katika vitendo na kujitoa kibinafsi, kama Kristo alivyodhihirisha upendo wake kwa kanisa. "Enyi waume, wapendeni wake zenu, kama Kristo naye alivyolipenda Kanisa, akajitoa kwa ajili yake" (Efe. 5:25).

Katika kitabu cha Ufunuo, Yohana anatofautisha kati ya upendo na kukosekana kwa upendo, si kwa maneno bali kwa mwenendo. "**Lakini nina neno dhidi yako: Umeuacha upendo wako wa kwanza. … Tubu na ufanye mambo uliyoyafanya hapo mwanzo. … Nayajua matendo yako, upendo wako na imani yako, huduma yako na uvumilivu wako, na ya kwamba sasa unafanya zaidi kuliko ulivyofanya hapo mwanzo**" (Ufu. 2:4-5, 19). Kuurudia upendo wa kwanza humaanisha mtu kutenda kama alivyokuwa akifanya hapo mwanzo. Upendo wa kwanza haukumalizwa kwa hisia, bali ulijionesha wenyewe kwa vitendo. Kama Manifesto ya Manila ya Vuguvugu la Lausanne, inavyotukumbusha, Injili isiyobadilika inaweza kuonekana wazi katika maisha yaliyobadilishwa ya waumini. Utangazaji wa upendo wa Mungu ni lazima uendane na huduma ya upendo. Kuhubiri Injili ya Ufalme wa Mungu humaanisha kujitoa kwa matarajio yake ya haki na amani."[21]

Afrika haiwezi kuurudia upendo wake wa kwanza au tumaini lake mpaka Wakristo walitangaze Neno la Mungu na kutenda kama lilivyo.

---

[21] Das Manifest von Manila. Lausanner Bewegung - Deutscher Zweig: Stuttgart, 1996. uk. 14.

TUMAINI HUBADILI MWENENDO WETU

30. Tumaini la Kweli Husadiki kwamba Mungu ni Mwenye Uweza Wote

Hoja: Hatuna sababu ya kweli kutumaini, isipokuwa twaamini na kujua kwamba kila kitu kiko chini ya umiliki wa Mungu. Tumaini la kweli limejengwa kwenye ukiri huu: "Namwamini Mungu Baba Mwenyezi, Muumba wa mbingu na nchi" (=Naamini katika Mungu mmoja, Baba wa Uweza Wote, Mwumba wa Mbingu na Dunia.").

Mungu ni Mwenye Uweza Wote

Ayu. 42:2: "**Najua ya kuwa waweza kufanya mambo yote, na ya kuwa mipango yako haiwezi kuzuilika.**"

Yer. 32:17: "**Aa! BWANA uliye Mkuu, umefanya mbingu na dunia kwa uweza wako mkuu na kwa mkono wako ulionyooshwa. Hakuna jambo lililo gumu kwako.**"

Mwa. 18:14: "**Kuna jambo lililo gumu sana kwa BWANA?**"

Mat. 28:18: "Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani"

Isa. 55:11: "**Ndivyo lilivyo neno langu litokalo kinywani mwangu: Halitanirudia bure, bali litakamilisha kile nilichokusudia na kutimiza kusudi ambalo kwalo nililituma.**"

Ayu. 36:22-23 "**Mungu ameinuliwa katika uweza wake. Ni nani aliye mwalimu kama yeye? Ni nani aliyemwelekeza njia zake, au aliyemwambia, 'Umefanya makosa'?**"

2 Nya. 14:11: "**BWANA, hakuna mwingie aliye mfano wako katika kumsaidia asiyejiweza dhidi ya mwenye uwezo. Tusaidie , Ee BWANA Mungu wetu, kwa kuwa twakutegemea wewe.**"

Zab. 33:10-11: "**BWANA hukwamisha mipango ya mataifa, huzuia malengo ya wanadamu. Bali mipango ya BWANA husimama imara milele.**"

Mungu huitwa, "Mwenye Uweza Wote": Mwa. 17:1; 28:3; 43:14; 48:3; 49:25; Kut. 6:3; Hes. 24:4; Rum. 1:20-21; Ayu. 40:2 (kama mara 30 hivi katika kitabu cha Ayubu); Zab. 68:15; Zab. 91:1; Isa. 13:6; Eze. 1:24; Ufu. 1:8; 4:8; 11:17; 15:3; 16:7,14; 19:6,15; 21:22

Ni pale tu tunapoyaamini haya, ndipo tunaweza kusadiki kwamba Mungu atayaleta yote na katika mwisho ulio mwema. Mfano mmoja kutoka Agano Jipya na mmoja kutoka Agano la Kale inatosha. Daudi anatangaza: "Umkabidhi BWANA njia yako, pia umtumaini, naye atafanya" (Zab. 37:5). Paulo anafurahia, "Nasi twajua ya kuwa katika mambo yote Mungu hufanya kazi pamoja na wale wampendao katika kuwapatia mema, yaani, wale walioitwa kwa kusudi lake… Kwa maana nimekwisha kujua hakika ya kwamba, wala mauti, wala uzima, wala malaika, wala wenye mamlaka, wala yaliyopo, wala yatakayokuwepo, wala wenye uwezo, wala yaliyo juu, wala yaliyo chini, wala kiumbe kinginecho chote hakitaweza kututenga na upendo wa Mungu ulio katika Kristo Yesu Bwana wetu" (Rum. 8:28, 38-39).

31. Tumaini Hutupatia Usalama na Amani ya Mawazo

Hoja: Tumaini hutupa amani ya mawazo, ingawa matatizo yetu wenyewe na mateso duniani pote yaweza kutufanya tuchanganyikiwe.

"**Utakuwa salama, kwa sababu kuna tumaini; utajichunguza na kupata pumziko lako katika usalama**" (Ayu. 11:18). Mtunga Zaburi aliomba, "**Nafsi yangu, tafuta mahali pa pumziko katika Mungu pekee; tumaini langu hutoka kwake**" (Zab. 62:5). Baba wa Kanisa aitwaye Chrysostomos alilielezea tumaini kama kamba ngumu inayoning'inia kutoka mbinguni na inayoshikiria nafsi zetu.[22]

Hakuna mwanadamu awezaye kubeba matatizo yote ya dunia, wala matatizo yote katika maisha yake mwenyewe. Matatizo ya siku moja yanatosha (Mat. 6:34). Mtu yeyote anayeisoma dunia kwa umakini sana kama mwandishi wa kitabu cha Mhubiri (tazama hoja ya 56) anaweza kuchanganyikiwa akifikiria matendo yote ya ukosefu wa haki, ubatili (ukosefu wa maana ya maisha), mateso, na kuharibika kwa dunia yetu; bali mtu awekaye tumaini lake kwa yule ambaye "ameiweka dunia katika mikono yake", kama watumwa wa Marekani walivyowahi kuimba, anaweza kuendelea kuishi kwa ujasiri.

[22] To Theodore, Ch. 2.

32. Tumaini Hutupatia Ujasiri

Hoja: Tumaini la Kikristo hutupatia ujasiri wa kutenda, "Kwa hiyo, kwa kuwa tuna tumaini la namna hii, tuna ushupavu mwingi" (2 Kor. 3:12). 'Ujasiri' na 'ushupavu' viko karibu sana na tumaini (Heb. 3:6). Tumaini na taraja huitupa nje hofu (Isa. 12:2; Zab. 46:3; Mith. 28:1), hata hofu ya kushindwa.

Wakristo barani Afrika sharti wajifunze kwamba tutahitaji tumaini katika siku zijazo katika sura ya mateso yanayoongezeka na hadhi ya walio wachache, hata katika nchi zenye utamaduni wa Kikristo wa zamani sana na uhuru wa kidini. Tunahitaji ujasiri kukabiliana na waumini na wanafiki, wanaofuata desturi peke yake.

33. Tumaini Hutufanya Tuwe wenye Kutegemea Mema na Wahalisia – Kukata Tamaa si Jambo Mbadala

Hoja: Pindi tujifunzapo kutofautisha kati ya matumaini danganyifu na tumaini la kweli, twaweza kuwa watu wenye kutegemea mema na wahalisia. Petro aliandika, "**mwe na kiasi; mkiweka kikamilifu tumaini lenu juu ya neema mtakayopewa wakati Yesu Kristo afunuliwapo**" (1 Pet. 1:13).

Uhalisia huu wa kutegemea mema utaweza kuonekana wazi duniani. Vinginevyo Petro asingetupatia changamoto ya kuhalalisha tumaini letu kwa wale wanaotuzunguka (1 Pet. 3:15). Mitume wanasadiki kwamba wengine watatambua tumaini lililo 'ndani yetu'.

Tumaini la Kibiblia liko katika mkamilishano wa tabia ya kutarajia mabaya kuelekea asili ya mwanadamu na ujasiri wa kutarajia mema katika fursa za Mungu, katika mvutano kati ya 'yaliyokwishafanyika' na ambayo 'hayajafanyika', kama ambavyo wanatheolojia walivyounda. Hakuna upande wowote wa mfumo wa mkamilishano unaoweza kuondolewa.

Afrika inahitaji Wakristo wenye kutarajia mema – siyo waota ndoto, washikiliao jambo sana bila akili, viongozi wa kisiasa wenye hotuba zenye mvuto bila mantiki au manabii wasio wahalisia wenye maangamizi, bali wahalisia wanaoshughulikia matatizo kikamilifu, tena kwa kuwa wanamwamini Mungu kikamilifu na kutegemea uingiliaji kati wake, wanaangaza tumaini na matarajio ya mema. Kizazi cha vijana wa Kikristo barani Afrika hawawezi kumudu vikwazo vipya vya kutarajia mabaya; wanahitaji watu walio vielelezo vya kuigwa ambao ni majasiri na waonao mbele.

Mapitio: Juu ya Mkamilishano wa Fikra za Kibiblia

Wanafizikia wamegundua mambo mengi ambayo yanaweza kuelezwa kama mkamilishano (Kwa Kilatini, 'Complementum': 'Ukamilisho'). Baadhi ya mambo haya yako katika mikamilishano ya vitu viwili viwili, mengine katika mkamilishano wa vitu vitatu vitatu. Tunazungumza juu ya mkamilishano wa rangi, kama vile nyekundu na kijani, ambazo huchanganywa na kuwa nyeupe. Elektroni inaweza tu kuonekana kama chembe au kama wimbi, lakini haiwezi kuonekana katika hali zote mbili wakati wa jaribio moja. Haya ni sawasawa pia hata katika jaribio la mwanga.

Hapo awali, Nadharia ya mkamilishano ilikuwa yenye kuleta mkanganyiko. Dane Niels Bohr (1885 – 1962), aliyepokea Tuzo ya Nobeli mnamo mwaka 1922, alitambulisha dhana hii mnamo mwaka 1927[23] na kujihakikishia ushindi wa wazo la mkamilishano katika Fizikia ya Karne ya Ishirini.[24]

> *"Mkamilishano [kwa maana ya Kilatini], ni jambo lililochunguzwa kwanza na N. Bohr, hutambua kwamba chembe chembe za atomu zina jozi mbili, zilizoungana lakini zinazoonekana kuwa na tabia kinzani, kwa mfano, chembe na wimbi. Hata hivyo ni vigumu kuchunguza tabia zote mbili kwa wakati mmoja, kwa kuwa vigezo vyote viwili huhitaji hatua za upimaji ambazo moja huingilia nyingine."*[25]

Wazo la mkamilishano humaanisha kwamba, mitazamo miwili, mitatu au zaidi ya jambo moja inaweza kuchunguzwa na kuelezewa kila mmoja peke yake, ingawa matokeo na matamko ya mtazamo mmoja mmoja kwa usawa ni halali, na ingawa mwanafunzi anaweza tu kuthibitisha matokeo yaliyo sahihi wakati elementi zote zihusishwapo vema kila moja na nyingine. Kwa mfano, rangi za mkamilishano, hutengeneza tu rangi nyeupe wakati zichanganywapo kwa usahihi.

Carl Friedrich von Weizsäcker anafasili mkamilishano kama ifuatavyo:

---

[23] Carl Friedrich von Weizsäcker. "Komplementarität und Logik", kr. 281-331 katika: Carl Friedrich von Weizsäcker. Zum Weltbild der Physik. S. Hirzel: Stuttgart, 1958[7], uk. 281.

[24] Tazama Wolfgang Buchheim. Komplementarität nach Niels Bohr. Sitzungsberichte der Sächsischen Akademie der Wissenschaften zu Leipzig, Mathematisch-Naturwissenschaftliche Klasse 117, 6. Akademie-Verlag: Berlin, 1984 and Wolfgang Buchheim (Ed.). Beiträge zur Komplementarität, katika mlolongo wa toleo lilelile, 55,5. Ibid. 1983.

[25] Bertelsmann Neues Lexikon in 10 Vols. Vol 5. Bertelsmann Lexikon Verlag: Gütersloh, 1995, uk. 323.

> *"Mkamilishano hujumuisha ukweli kwamba elementi haziwezi kuchukuliwa kutenda kazi kwa pamoja ingawa zote hazina budi kutumika."*[26]

Kwa sasa, mawazo ya aina hii yameenea kutoka kwenye fizikia kwenda kwenye sayansi nyingine za asili na katika nyanja mbalimbali za maisha.[27]

Mtazamo huu si kwamba hauna mantiki: mipaka ya kibinadamu hutufanya tutegemee maelezo ya mkamilishano ya ukweli wa Kibiblia. Kanisa la Kwanza kwa kukusudia walitengeneza mfumo wa mafundisho ya kidogma ulio muhimu sana wa imani ya Kikristo katika muundo wa mkamilishano, kama ulivyotetea ukweli kwamba Mungu ni Mtatu au kwamba kwa wakati mmoja Yesu ni Mungu halisi na Mwanadamu halisi.

Asili ya mkamilishano wa ukweli wa Kibiblia unaweza kushiriki jukumu muhimu katika kuyashinda mabishano yasiyo ya lazima miongoni mwa Wakristo.[28] Tunapenda kusisitiza upande mmoja wa ukweli wa mkamilishano na kutokujali uthamani wa upande mwingine, kama ambavyo baadhi ya wanatheolojia walivyozoea kusisitiza asili ya ubinadamu wa Yesu ili kukanusha asili yake kama Mungu, au kuonesha juu ya utii wake ili kukanusha mafundisho ya usawa wake na Baba yake katika Uungu na wadhifa wake.

Ukweli wa Kibiblia hujumuisha mafundisho ya mikamilishano mingi zaidi ya Utatu na Asili Mbili za Kristo:

- Majaliwa na Uwajibikaji
- Imani na Ufahamu
- Sheria na Neema
- Hukumu na Msamaha
- Upendo wa Mungu na Hasira Yake
- Mafundisho na Maisha
- Ubatizo kama Tendo la Mungu na Tendo la Mwanadamu
- Umuhimu wa Vyeo vya Kanisa na Ukuhani wa Waumini Ulimwenguni[29]
- au Tofauti na Usawa wa Mwanamume na Mwanamke[30]

---

[26] Carl Friedrich von Weizsäcker. „Komplementarität und Logik". op. cit., uk. 284, akifafanua mtazamo wa kale wa mkamilishano. Maoni yake binafsi kwa namna fulani ni tofauti.

[27] Kwa mfano tazama, Helmut K. Reich. Der Begriff der Komplementarität in Wissenschaft und Alltag. Berichte zur Erziehungswissenschaft 105. Pädagogisches Institut Freiburg (CH), 1994.

[28] Tazama Winfried Amelung. In IHM ist die Fülle: Wider die falschen Alternativen. Weinmann-Stiftung: Dornstetten, 1988.

[29] Rud., uk. 33-50 (Church office) und pp. 51-69 (baptism).

Maandiko hutambulisha mada hizi zote kwa mitazamo miwili au zaidi inayoonekana kukinzana, ambayo hata hivyo, haiwezi kutenganisha kila moja na nyenzake, lakini inayoweza tu kufikiriwa kwa njia ya mtazamo mmoja kwa wakati mmoja.

34. Kama Tukitarajia Kile ambacho Kibinadamu Hakiwezekani, Basi Tutafanya Yote ambayo Kibinadamu Yanawezekana

Hoja: Iwapo tutategemea kile ambacho kibinadamu hakiwezekani, basi tufanya yote tuwezayo ili kukipata, kwa kuwa, "Umtumaini BWANA ukatende mema" (Zab. 37:3). Tumaini hutufanya tuwe watendaji! Ni kukoswa tumaini kunakotufanya tusiwe watendaji, tuwe dhaifu na waoga.

35. Tumaini Hutufanya Watulivu, lakini si kuwa Wazembe na Wasio Watendaji

Hoja: "Kutumaini ni kusonga mbele kuelekea lengo,"[31] kwa kuwa tumaini ni nguvu ya imani ya kihistoria iliyo hai.

Oskar Cullmann anaandika, "eskatolojia ya Kikristo ya kweli haiwezi kukuza ukosefu wa utendaji, kutofanya kazi au kutojishughulisha."[32] Kama tumaini hutuongoza kwenye utulivu wenye sifa ya kutofanya kazi na uzembe, kwa nini mara kwa mara Biblia hutukumbusha kwamba tumaini hutupatia nguvu (Isa. 40:31; 30:15) na hutokana na nguvu ya Roho Mtakatifu peke yake (Rum. 15:13)?

La hasha, tumaini hutupatia ushwari ulio makini na ulio na utendaji. Tumaini halichochei utendaji wenye wazimu, bali ufanyaji kazi wa kimantiki kwa ajili ya wengine. Utendaji ni sehemu ya tumaini: "**Shika upendo na haki, na umngojee Mungu wako daima**" (Hos. 12:6), kwa kuwa, "Matamanio ya mwenye haki huishia katika mema tu, lakini tumaini la mtu mwovu huishia katika ghadhabu" (Mith. 11:23).

Bara la Afrika katika baadhi ya maeneo limeshawahi kuwa bara la Kikristo kwa sababu tu Wakristo wengi katika vizazi vilivyotangulia walichochewa na tumaini. Hatutairudisha Afrika kwa Yesu, tusipotarajia kila kitu

---

[30] Tazama John Stott. Christsein in den Brennpunkten unserer Zeit ... 4 ... im sexuellen Bereich. Francke: Marburg, 1988 [Engl. 1984]. kr. 21-24 (Abschnitt "Komplementarität").

[31] Ernst G. Hoffmann katika Theologisches Wörterbuch zum Neuen Testament, II, 726.

[32] Oskar Cullmann. Jesus und die Revolutionäre seiner Zeit. Mohr Siebeck: Tübingen, 1970, uk. 29.

kutoka kwa Mungu na kuanza kutenda. Hatutaweza pia kuuvuta ulimwengu kwa Yesu, tusipotarajia kila kitu kutoka kwa Mungu na kuanza kutenda!

36. Tumaini Hutufanya Tuwe Watendaji na Watetezi wa Haki

Hoja: Tumaini hutufanya tuwe tayari kutenda [na] kuthubutu, badala ya kuongea tu! "Na kwa jambo hili twajishughulisha na kujitahidi, kwamba tumeweka tumaini letu kwa Mungu aliye hai, ambaye ni Mwokozi wa watu wote, na hususani wa wale waaminio" (1 Tim. 4:10).

Wakristo wengi sana barani Afrika wamekaa tu kwa muda mrefu, wakati ambapo tumaini letu lingetusukuma kufanya kazi. Ni pale tu tunapotafuta kuwasaidia wengine, hata kama wote wako kinyume nasi, ndipo tumaini letu linapokuwa halisi kwa wengine.

37. Tumaini Hutupatia Vipaumbele Vipya, ambavyo Hutuwezesha Kuachilia Mbali Mapendeleo Yetu

Hoja: Tumaini hubadilisha vipaumbele vyetu, ambavyo hudhihirishwa katika utayari wa kufanya, bila kujitoa dhabihu na kukubali hasara. Wale wanaoshindana, wako tayari kuacha raha ili washinde (1 Kor. 9:25).

Akiongea juu ya wanawake, Petro anaonesha kwamba, tunaweza kuachilia vitu muhimu kwa wengine (hapa anazungumzia, mavazi na vito vya thamani), kwa sababu tumaini letu limebadilisha maadili yetu. 'Wanawake watakatifu wa zamani waliomtumaini Mungu', walijipamba vizuri kwa maadili bora ya ndani (1 Pet. 3:5). Tunaposhikilia maadili yetu katika hali ya shinikizo, tunapata uzoefu wa nguvu itokanayo na tumaini letu, kwa kuwa, "**mateso huzaa uvumilivu; uvumilivu huzaa tabia; na tabia huzaa tumaini**" (Rum. 5:3-4). Kila aina ya tumaini kwa ajili ya wakati ujao huathiri utendaji wetu wa sasa. Wakristo hawana udhuru: tumaini letu katika uhalisia ambao Mungu ametuahidi, ni lazima litubadilishe kuelekea kwenye ubora zaidi. "**Kila mmoja mwenye tumaini hili ndani yake hujitakasa, kama yeye alivyo mtakatifu**" (1 Yoh. 3:3).

38. Tumaini Hutufanya Welevu na Wavumilivu kwa Wengine

Hoja: Uvumilivu ni maadili ya hali ya juu ya Kikristo yanayokua kutokana na tumaini. Tunapokuwa na tumaini kwa ajili ya wengine, tu-

takuwa pia watu wenye ufahamu zaidi. "**Lakini ikiwa twatumainia kile ambacho hatuna, twakitumainia kwa saburi**" (Rum. 8:25). Uvumilivu huu huathiri mahusiano yetu na wengine (Gal. 5:22; Efe. 4:2; Kol. 3:12-13; 1 Tim. 6:11; 2 Tim. 3:10). Paulo hutuambia kwamba upendo, "**daima huvumilia, daima huamini, daima hutumaini, daima hustahimili**" (1 Kor. 13:7).

39. Tumaini Hujenga Ustahimilivu

Hoja: Tumaini hutusaidia kustahimili, wakati ambapo tungechagua kukata tamaa. "**Bali wale wawekao tumaini lao kwa BWANA watapata nguvu mpya; wataruka juu kwa mbawa kama tai; watakimbia, wala hawatachoka; watatembea, wala hawatazimia**" (Isa. 40:31). Jambo hili ni kweli katika maisha yetu binafsi, vile vile kwa Kanisa na kwa jamii.

Kama tukitarajia kutimilika kwa tumaini letu katika 'muda mfupi ujao', tutaweza kusubiri. Dunia itajua tabia yetu hii katika wakati huu tulionao.

Wakristo wengi ulimwenguni hulalamika kwamba hapo mwanzo maeneo kadhaa ya maisha ya jamii yaliyotawaliwa na maadili ya Kikristo kwa sasa yanatawaliwa na maadili mengine. Katika kulalamika tunapuuza ukweli kwamba ushawishi wa Kikristo mara zote umetegemea kipindi kirefu cha jitihada za waumini ambao kwa muda wote hawajawahi kujionea uhalisia wa ndoto zao. Tunaposhughulikia mabadiliko ya kisheria, tunapojenga vyuo au tunapofanya kazi na vijana wasio na ajira, tunaathiri muda mfupi ujao, na yawezekana tusione mavuno kwa miaka mingi. Tunahitaji miradi ya Kikristo ya muda mrefu na uwezo wa kuanzisha mambo katika nyanja zote za uumbaji na maisha ya Kanisa.

40. Kwa Sababu Tumaini Hutarajia, Basi Tumaini Hufurahia

Hoja: Kwa kadri tunavyokuwa na tumaini, tuna sababu ya kufurahi. Mbali na matatizo sugu, nabii Isaya aliandika, "**Katika siku hiyo watasema, 'Hakika huyu ndiye Mungu wetu; tuliyemtumaini, na ametuokoa. Huyu ndiye BWANA tuliyemwamini; basi tufurahi na kufanya shangwe katika wokovu wake**'" (Isa. 25:9).

Na furaha yetu ni lazima ijae tumaini. "**Katika tumaini iweni wenye furaha, katika mateso iweni wavumilivu, na katika maombi iweni waaminifu**" (Rum. 12:12).

Kwa sababu hii, mara zote Maandiko huzungumza juu ya furaha na tumaini kwa wakati mmoja. Paulo anaandika, "**Mungu wa tumaini awajaze ninyi furaha yote na amani yote kadri mnavyomtumaini, ili mfu-**

rike kwa tumaini, kwa nguvu za Roho Mtakatifu" (Rum. 15:13; Angalia pia 1 Thes. 2:19). Na katika Mithali 10:28 tunaona kwamba, "**Matarajio ya mwenye haki ni furaha; lakini matumaini ya waovu huwa kitu bure**".

Mahali palipo na tumaini, pana furaha. Mahali ambapo tumaini kuu linaweza kupatikana – katika imani ya Kikristo – ni lazima patakuwa na furaha kuu. Cha kushangaza, hizi ni habari kwa watu wengi wa Afrika, ambao uzoefu wao wa kiutendaji kwa Wakristo na kwa Kanisa huzungumza lugha nyingine wakiamini Wakristo si watu wenye tumaini na furaha. Ni lazima tujifunze kufurahi, kusherehekea furaha yetu kama ilivyo katika Biblia, na kutumia sanaa, kama vile muziki na uchoraji wa picha, kwa kulingana na mapenzi ya Mungu.

TUMAINI KATIKA MATESO NA UPINZANI

41. Tumaini Huhitaji Mateso na Jitihada – Utambuzi wa Ukosefu wa Matumaini na wa Faraja

Hoja: Hata wale wanaomwamini Mungu wanaweza kuwa katika hali ya kukosa matumaini.

Biblia huizungumzia hali hii kwa uaminifu kabisa. Zaburi za maombolezo, kitabu cha Ayubu (hasa Ayubu 17:13-15), na Maombolezo ya Yeremia kwa uaminifu huelezea kukata tamaa na hisia za kuachwa na Mungu, pasipo kukana maungamo ya waziwazi kama yale yaliyofanywa na marafiki wa Ayubu. Mfadhaiko mkubwa unaweza kutufanya tupoteze hata tumaini letu kwa Mungu. "**Hivyo nasema, 'Ufahari wangu umepotea na yote niliyoyatumainia kutoka kwa BWANA**" (Omb. 3:18).

Katika hali hii, si vizuri kupuuza maumivu, bali kuyavumilia kwa msaada wa Mungu na marafiki, na kumngojea Bwana. "**Ni vema kumngojea Bwana kwa utulivu kwa ajili ya wokovu wa BWANA**" (Omb. 3:26); "**Lakini kwangu mimi, ninamtazamia BWANA kwa matumaini, namngojea Mungu Mwokozi wangu; Mungu wangu atanisikia**" (Mik. 7:7). Wakati mwingine mtu anaweza kuvurugwa katikati ya tumaini na mashaka ya tumaini hilo, kama Ibrahimu alivyokuwa: "**Kinyume cha matumaini yote, katika tumaini Abrahamu aliamini**" (Rum. 4:18). Hivyo twaweza kuomba tu namna hii, "**Naamini, nisaidie kukushinda kutokuamini kwangu**" (Mk. 9:24).

Kwa sababu hii, hatutaweza kamwe kujifunza tumaini la kweli kama mambo yote yanakwenda sawa sawa, isipokuwa katika magumu, mateso, magonjwa na dhambi, na hata katika kifo. Paulo anaandika, "**Natarajia kwa hamu na kutumaini kuwa kwa namna iwayo yote sitaaibika, bali nitakuwa na ujasiri wa kutosha ili, sasa kama ilivyo daima, Kristo atainuliwa katika mwili wangu, iwe kwa kuishi au kwa kifo**" (Flp. 1:20).

Wale ambao kwa mara chache wamepitia mateso binafsi wanaweza kujifunza maana ya tumaini kwa kubeba mizigo ya wengine, kwa kuwaonea huruma (Ebr. 4:15; Kwa Kigriki: sumpaqe, kihalisia, 'kuteseka pamoja na'). Kwa kuwa, kama Paulo anavyoandika, "**Ikiwa kiungo kimoja kinaumia, kila kiungo huumia pamoja nacho; ikiwa kiungo kimoja kinaheshimiwa, kila kiungo hufurahi pamoja nacho**" (1 Kor. 12:26).

Wakati Biblia inapotuambia kwamba wale wawekao tumaini lao kwa Mungu wamebarikiwa, mara zote huzungumza juu ya watu ambao wame-

pitia mateso makali na kukata tamaa (kwa mfano: Zab. 146:5; 84:12; Yer. 17:7). Kristo hajatuahidi mafanikio katika maisha haya na tumaini letu haliwekewi mpaka na wale waliofanikiwa. Mfadhaiko na kukata tamaa ni lazima vivumiliwe na kwamba vinaweza kuchukua muda, lakini hatimaye, tumaini la Mungu hushinda, "**Mungu alifanya hivyo ili, kwa vitu viwili visivyoweza kubadilika, ambavyo katika hivyo haiwezekani Mungu kusema uongo, sisi tuliokimbilia kushika tumaini lililotolewa kwetu tuweze kufarijiwa sana**" (Ebr. 6:18, Tazama pia Zab. 119:49-50). Tunaweza kuwa wenye shukrani kwamba Baba yetu wa mbinguni, "**alitupenda, na kwa neema yake akatupa faraja ya milele na tumaini jema**" (2 Thes. 2:16). Hata katika mateso mazito, Ayubu anaweza kulia, "**Najua kuwa Mkombozi wangu yu hai**" (Ayu. 19:25). Sote twaweza kuomba, "**Ee nafsi yangu, kwa nini kuhuzunika? Kwa nini kuhangaika ndani yangu? Weka tumaini lako kwa Mungu, kwa kuwa bado nitamtukuza**" (Zab. 42:5; Tazama pia Zab. 42:11 na Zab. 43:5).

42. Maombi Hutuongoza kwenye Tumaini na Tumaini Hutuongoza kwenye Maombi

Hoja: Kwa sababu maombi ni udhihirisho wa tumaini letu kwa Mungu, katika wakati wa kukata tamaa na kukosa tumaini, maombi huwa faraja yetu iliyo muhimu sana. "**Katika tumaini iweni wenye furaha, katika mateso iweni wavumilivu, na katika maombi iweni waaminifu**" (Rum. 12:12).

Hoja zangu nyingi huonesha mahusiano ya karibu kati ya maombi na tumaini, kwa kuwa mengi ya Maandiko yaliyonukuliwa yametoka kwenye kitabu cha maombi cha Biblia, yaani Zaburi, ambacho si kwamba kina usihi mwingi wa kumtumaini Mungu pekee, bali pia kina maombolezo mengi, ambayo huanza wakati wa kukata tamaa, mateso, kukosa tumaini, na kwamba jambo hili taratibu huanza katika kukata tamaa na kuelekea kwenye tumaini.

Tunahitaji jambo hili sio tu katika maisha yetu binafsi, bali pia katika jamii yetu kwani maangamizi yake ni maangamizi yetu. Si Mungu awaamuruye Waisraeli kutafuta ustawi wa Babeli, ingawa mji huu ni wa kipagani, [kwa kuwa] maangamizi yake ni maangamizi ya watu wa Mungu? "**Pia, tafuteni amani na mafanikio ya mji ule ambao nimewachukua utumwani. Ombeni kwa BWANA kwa ajili yake, kwa sababu ikiwa utafanikiwa, nanyi mtafanikiwa pia**" (Yer. 29:7). Katika Agano Jipya, Paulo analiambia kanisa kuiombea serikali, "**Basi, nawasihi, kwanza kabisa, maombi, sala, dua na utoaji shukrani vifanywe kwa ajili ya**

kila mmoja – kwa ajili ya wafalme na wale wote walio katika mamlaka, kwamba tuweze kuishi kwa amani na katika maisha matulivu katika utauwa wote na utakatifu. Jambo hili ni zuri, na humpendeza Mungu Mwokozi wetu" (1 Tim. 2:1-3), kwa kuwa sera za kisiasa na hali ya jamii vilevile huamua juu ya maisha wa Kanisa.

Kwa maoni yangu, mojawapo ya alama muhimu za matumaini ya Afrika ni shauku ya Wakristo wa Afrika kuomba na ushiriki wao katika aina zote za mavuguvugu ya maombi, kama vile Operation World [Opareshen i ya Kiulimwengu], the Alliance Week of Prayer [Wiki ya Maombi ya Ushirikiano], Siku ya Kiulimwengu ya Maombi kwa Wakristo Wanaoteswa, Siku 30 za Maombi kwa ajili ya Ulimwengu wa Kiislamu. Wakristo barani Afrika hawana budi kushiriki kwa hali zote – katika maombi na kivitendo kwa ajili ya wenzao na hata wale wasio Wakristo ulimwenguni kote! [Changamoto kubwa kwa Wakristo barani Afrika pote ni kuhakikisha kuwa wanaishi kivitendo katika tumaini jema walilonalo ili kuupa ulimwengu matumaini ya kweli].

43. Mateso kwa ajili ya Tumaini

Hoja: Siyo muhimu tu kujitahidi kutumaini wakati wa mateso, bali ni muhimu pia kuteseka daima kwa ajili ya tumaini letu. Historia huonesha kwamba hakuna kitu kinachoweza kupatikana pasipo utayari wa kuteseka kwa ajili ya tumaini.

Paulo anasisitiza kwa wahukumu wake kwamba anahukumiwa, "**kwa sababu ya tumaini langu katika ufufuo wa wafu**" (Mdo. 23:6; Tazama pia Mdo. 26:6-7; 28:20; kwa mistari mingine ya ufufuo tazama hoja ya 23).

Badala ya kulihubiri tumaini letu katika hali ya kustarehe tukiwa kwenye sofa [makochi] ya sebuleni, hatuna budi kukubali umuhimu wa hasara na mateso halisi kwa ajili ya tumaini letu. Siyo kwa sababu mateso yana thamani yoyote ndani yake, bali ni kwa sababu dunia yetu hutufanya tuteseke na kwa sababu maumivu yetu huonesha wazi uzito wa hali ilivyo.

44. Tumaini Halishindwi, kwa sababu Hutoka Ndani

Hoja: Tumaini la kweli huishi ndani ya mioyo wa wanadamu na hivyo haliwezi kushindwa na nguvu zitokazo nje. "**Na tumaini halitufadhaishi, kwa sababu Mungu amemimina pendo lake mioyoni mwetu kwa njia ya Roho Mtakatifu, ambaye ametupatia sisi**" (Rum. 5:5).

Kwa sababu hii, tunapaswa "**kutoa sababu kwa ajili ya tumaini mlilonalo**" (1 Pet. 3:15). Si jambo la ajabu kwamba Maandiko mengi huzungumzaa juu ya tumaini lililo mioyoni mwetu (kwa mfano Efe. 1:18). Na

kwa sababu hii, tumaini la kweli humaanisha kwamba Roho wa Mungu huibadilisha mioyo yetu. "**Pia naomba kwamba macho ya mioyo yenu yatiwe nuru ili mweze kujua tumaini ambalo kwalo amewaiteni, yaani utajiri wa urithi wake wa utukufu kwa watakatifu**" (Efe. 1:18). Na kwa sababu hii, siri ya tumaini ni kwamba, Kristo anaishi 'ndani yetu'. "**Kwao hao Mungu amechagua kuujulisha utajiri wa utukufu wa siri hii katikati ya mataifa, ambayo ni Kristo ndani yenu, tumaini la utukufu**" (Kol. 1:27).

Katika Biblia, moyo ni kitovu (kiini) cha uamuzi, mawazo, dhamiri, na mwenendo, mahali ambapo tunafanyia maamuzi. Moyo huongoza maisha yetu wakati Mungu na Neno lake wanapotawala moyo wa mtu, yaani 'aaminipo katika moyo wake' katika maana ya kibiblia ya neno lenyewe (angalia Mk. 11:23; Rum. 10:9-10; Mdo. 8:37) na kumpenda Mungu 'kwa moyo wake wote' (Kumb. 6:6; Mat. 22:37). Imani na maisha ni kitu kimoja. Akizungumzia juu ya Mali, Yesu anatumia neno 'moyo' katika maana hii wakati asemapo, "Kwa kuwa hazina yako ilipo, ndipo utakapokuwepo na moyo wako" (Mat. 6:21= Luk. 12:34).

45. Tumaini Halishindwi, kwa sababu Hutoka Mbinguni

Hoja: Katika Umilele wote, tumaini hutupatia nguvu hapa tulipo na katika wakati tulionao. Paulo anazungumza juu ya "tumaini lililohifadhiwa kwa ajili yenu huko mbinguni" (Kol. 1:5).

Wasioamini hawawezi kulifahamu tumaini la kweli la Kikristo, na hali ngumu (yaani 'Dunia') haziwezi kulishinda, kwa sababu linaishi ndani yetu na kwa sababu linatoka kwa Mungu.

46. Tumaini Hutulinda dhidi ya Yule Mwovu

Hoja: Tumaini la Kikristo hutulinda dhidi ya mashambulizi ya mwovu, kwa kuwa tunavaa "imani na upendo kama deraya ya kifua, na tumaini la wokovu kama chepeo" (1 Thes. 5:8; Tazama pia Efe. 6:17). Sehemu muhimu sana ya mwili wetu, yaani kichwa, huvaa tumaini kama chepeo. Tunapopoteza ulinzi huo tunapoteza vichwa vyetu na tutajipoteza sisi wenyewe pia.

Kama Baba wa Kanisa Chrysostomos alivyoandika, "Kama vile chepeo inavyolinda sehemu yetu iheshimikayo sana, yaani kichwa chetu, kwa kukifunika pande zote, ndivyo tumaini linavyotunza ujasiri wetu usizame, na kuusimamisha, likizuia chochote kitakachotuangukia kutokea nje."[33]

[33] Homily, Ch. 5, 8

Kwa kweli, tumaini hutulinda, kwa sababu tu Mungu ndiye mlinzi wetu na kwa sababu tunaweza kumtegemea Yeye na Neno lake. "**Wewe ni kimbilio langu na ngao yangu; nimeweka tumaini langu katika neno lako**" (Zab. 119:114).

TUMAINI MBELE YA TASWIRA YA SIKU YA HUKUMU

47. Maandiko Huhalalisha Tumaini la Kanisa Kukua

Hoja: Mafanikio ya Huduma ya Umisheni Duniani yana hakikisho la mamlaka isiyoonekana na ya kiulimwengu ya Yesu Kristo.

Mafanikio ya huduma ya umisheni duniani huthibitisha ahadi ya mamlaka ya Kristo. Katika Utume Mkuu ulio katika Mathayo 28:18-20, anatangaza ushindi wa utangazaji injili ulimwenguni kwa uthibitisho kwamba: "Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani" (mst. 18) na kwamba "**hakika, mimi niko pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari**" (mst. 20) – na hayo [yalisemwa] mbele ya mashaka waliyokuwa nayo wanafunzi (mst. 17). Utume Mkuu ni ahadi na vilevile ni amri, kwa kuwa Bwana mwenyewe atawafanya mataifa [watu] yote kuwa wanafunzi: "Nitalijenga kanisa langu; wala milango ya kuzimu haitalishinda" (Mat. 16:18). Je, si Kitabu cha Ufunuo kinachoendelea daima kutangaza kwamba watu wa lugha zote na tamaduni zote watakuwa miongoni mwa kusanyiko lisilohesabika la waliokombolewa? "**Na waliimba wimbo mpya: 'Wastahili wewe kutwaa gombo na kufungua mihuri yake, kwa sababu ulichinjwa, na kwa damu yako ulimnunulia Mungu wanadamu kutoka kila kabila na lugha na watu na taifa**'" (Ufu. 5:9-10. Tazama pia 7:9; 10:11; 11:9; 13:7; 14:6; 17:15).

Ukuaji ni tabia ya Ufalme wa Mungu, kama Kitabu cha Danieli kinavyodhihirisha katika taswira nyingi za kinabii, na kama ambavyo mifano ya Yesu inavyotoa picha ya mambo ya siku za usoni. Ndoto ya Nebukadreza inaishia na jiwe linaloanguka kutoka mbinguni [na] kuiharibu sanamu ya falme za dunia (Dan. 2:34-35), na kisha linakua kuwa mlima mkubwa "likaijaza dunia yote" (Dan. 2:35, 45). Danieli anafasili, "**Katika kipindi cha wafalme hao, Mungu wa mbinguni atausimamisha ufalme ambao hautaharibiwa kamwe, wala hautaachwa kwa watu wengine. Utaharibu falme hizo zote na kuzifikisha mwisho, bali wenyewe utasimama milele**" (Dan. 2:44). Danieli anaonesha mwisho wa falme za dunia zinazowasilishwa kama wanyama kwa njia ile ile (Dan. 7:9-14, 26-27). Falme hizi zinafikia mwisho, wakati 'mwana wa mtu' (Dan. 7:13; Yesu alitumia jina hili mara nyingi kurejea kwake mwenyewe) apaapo Mbinguni (yaani Kupaa kwenda Mbinguni) na anapokea "**mamlaka, utukufu na nguvu za kifalme**", ili kwamba "watu wote, mataifa yote na wanadamu wa kila lugha wamwabudu yeye" (Dan. 7:14). Ufalme huu

hautaharibiwa (Dan. 7:14, 27). Yesu aliimarisha kwanza Ufalme wake katika kipindi cha Dola ya Kirumi, akianza na wanafunzi wake na Kanisa la Kwanza, na kutoa unabii katika mifano mingi kwamba utakua na kuijaza dunia (kwa mfano; mfano wa ngano na magugu katika Mat. 13:24-30, 36-43; mfano wa punje ya haradali katika Mat. 13:31-32; mfano wa chachu katika Mat. 13:33-35).

Katika Biblia yote, ahadi hii ya ukuaji hurejea nyanja zote za Kanisa, za ndani na za nje, za kiroho na kimwili, kila moja ikitazamwa kipekee au zote zikichukuliwa kwa pamoja. Ukuaji huu wa ndani na wa nje wa Ufalme wa Mungu na wa Kanisa la Yesu Kristo haumaanishi kwamba kila Kanisa la Kikristo, dhehebu au kundi litakua tu lenyewe – Mungu anaweza kuadhibu Kanisa lake au kuruhusu makanisa maasi kufa (Tazama Ufu. 2:5; Rum. 11:20-21).

Uhakika wa ukuaji na ushindi wa mwisho wa Ufalme wa Mungu hauondoi uwezekano wa mateso. Hususani mifano ya ukuaji, kama vile mfano wa ngano na magugu (Mat. 13:24-30; 36-43) hudhihirisha wazi kwamba uovu hukomaa sambamba na Ufalme. Hata hivyo, magugu yanaweza tu kuendelea kwa sababu Mungu anaruhusu Kanisa lake kukua na kukomaa. Ikiwa Kanisa la Kristo lingeondolewa duniani, hukumu ya mwisho ingeshuka mara moja (Tazama Mwa. 18:22-23).

48. Tumaini Mbele ya Upinzani wa Kidini na wa Kiserikali

Hoja: Ufunuo wa Yohana Mtakatifu unatoa ujumbe wenye nguvu ambao umeendelea daima kuwatia moyo Wakristo katika historia.

Vyovyote tunavyoweza kufasili yaliyomo katika Ufunuo, hatuna budi tukubaliane katika hoja hii. Kanisa haliongezeki kwa kutumia mamlaka, utajiri au nguvu, bali ni kwa mamlaka ya Kristo, Neno la Mungu na maombi peke yake. Hata wakati Mungu anaporuhusu mamlaka ya dini na serikali kuunganisha nguvu dhidi ya Kanisa, na hata wakati ambapo Kanisa huonekana kupotea, Kanisa la uongo na Serikali potovu hujichimbia makaburi yao wenyewe pindi wapingapo Kanisa la Yesu. Tena Mungu huongoza mamlaka za dunia kugombana zenyewe kwa zenyewe, hivyo basi mamlaka za kisiasa huangamiza wapinzani wa kidini wa Kanisa, kama ilivyo kwa Mnyama wa Ufunuo anavyomgeukia Kahaba wa Babeli.

Ufalme wa Mungu huendelea kukua kinyume na mamlaka zote za kidini, za kisomi, za kiuchumi na kisiasa za dunia hii. Je, hii haikuwa kanuni ya kiroho iliyo dhahiri katika Agano la Kale? Je, Yesu hakuitangaza [kanuni hii] katika Utume Mkuu na katika ahadi kwamba wala milango ya kuzimu haitaushinda Ufalme wa Mungu?

Je, kanuni hii hajathibitishwa kwa kurudiwarudiwa katika historia ya Kanisa? Iko wapi Dola ya Kirumi, uko wapi Umanikaisimu, ziko wapi dini za zamani sana zilizoenea sehemu nyingi ambazo zote ziliuchukia Ukristo, bali sasa zimebaki kuwavutia wanahistoria? Nini kilichoupata Ujamaa wa Kitaifa au Mapinduzi ya Kidunia ya Kikomunisti yaliyoanzia Ujerumani na Urusi? Je, hatuwezi kujifunza kutoka Ufunuo kuwa siku za Uislamu, za Makundi ya Siri, za Mali [Vitu] zinahesabika, hata kama hatuna wazo ni lini mpango wenye hekima wa Mungu utafunuliwa?

49. Bado tuna Tumaini, hata Mbele ya Hukumu Ijayo

Hoja: Hata wakati Mungu anapokuwa ametangaza hukumu, hususani wakati anapokuwa ametamka hukumu, twaweza kutumaini.

Yona alikuwa na hakika kwamba Ninawi ulikuwa umepotea. Tangazo la Mungu lilisikika kana kwamba uamuzi wa Mungu ulikuwa usiobadilika: “Baada ya siku arobaini Ninawi utaangamizwa” (Yona 3:4), lakini kulikuwa na sharti ambalo halikusemwa, ambalo huelezea ni kwa nini Yona alitumwa kwanza kwenda kuhubiri - “Wasipotubu na kuamini!” Wakazi wa mji ule walilisikia onyo, wakatubu na kumtukuza Mungu, ambaye baadaye aliwaonea huruma kinyume na tishio lake (Yona 3:5-10).

Pamoja na hasira yake, Yona alijua kwamba mara nyingi Mungu hutenda kwa namna hii: “Kwa maana nalijua ya kuwa wewe u Mungu mwenye neema, umejaa huruma” (Yona 4:2). Malalamiko ya Yona na kukata tamaa kwake, vyote vilikuwa na msingi wa kitauwa na wa kitheolojia. Alikuwa “amechukizwa sana” (Yona 4:1) kwamba Mungu alichagua kuwasamehe Waashuru, ingawa, kama mwanatheolojia mzuri, alipaswa kutambua kwamba Mungu pia huwahurumia wapagani. “**Hii ndiyo sababu nilifanya haraka kukimbia**” (Yona 4:2). Mungu akamfanyia Yona mtango (mzabibu), ili “**kumpunguzia adha**” na alipouacha ukakauka, Yona alijisikia vibaya sana na akataka afe. Sasa, Mungu alikuwa amemwonesha jinsi alivyojisikia juu ya waliopotea katika Ninawi (Yona 4:7-11).

Akirejea kwenye kitabu cha Yona katika mahubiri yake marefu yaliyoitwa ‘Mahubiri juu ya Toba’, Baba wa Kanisa Chrysosotomos husisitiza kwamba mahubiri ya Kikristo mara nyingi huonekana yakiharibu tumaini, lakini siyo kwa ajili ya kuliteketeza, bali ni kuelekeza tu kwenye tumaini la kweli linalopatikana kwa Mungu peke yake.

Neema ya Mungu isiyofikirika hujieleza yenyewe katika ukweli kwamba matamko ya Mungu ya mara chache huthibitishwa kwa kiapo, ambacho huyafanya yasibadilike, lakini matamko ya neema ni mengi mno.

Vilevile, Agano la Mungu kwa Nuhu, kwamba asingeweza kamwe kuuhukumu ulimwengu tena (Mwa 8:20-9:17) lilithibitishwa kwa kiapo. Katika historia ya Israeli anafanya yale yale kama Isaya 54:9 inavyoeleza: "Kwa maana jambo hili limekuwa kama maji ya Nuhu kwangu; maana kama nilivyoapa ya kwamba maji ya Nuhu hayatapita juu ya dunia tena, kadhalika nimeapa ya kwamba sitakuonea hasira, wala kukukemea."

50. Mbele ya Hukumu ijayo, Mungu Hujaribu Imani yetu

Hoja: Kanisa huhubiri hukumu tu, kwa sababu tuna tumaini. Kitisho cha hukumu hutupatia fursa za kipekee kulidhihirisha tumaini letu kwa njia ya kuomba, maneno na vitendo.

Ayubu alitumia mfano wa mti unaoonekana kuwa umekufa na usio na kitu, mfano uliotumiwa mara kwa mara na manabii wa Agano la Kale: "Kwani yako matumaini ya mti, ya kuwa ukikatwa utachipuka tena, wala machipukizi yake hayatakoma" (Ayubu 14:7).

Mithali 11:11 hufundisha kwamba Mungu anaweza hata kuihifadhi jamii kwa ajili ya watu wachache wacha Mungu: "Mji hutukuzwa kwa mbaraka wa mwenye haki; bali mji hupinduliwa kwa kinywa cha mwovu."

Maombi ya dharura ya Ibrahimu kwa ajili ya Sodoma na Gomora (Mwa. 18:6-33) hudhihirisha umuhimu kuwa watu wacha Mungu wanaweza kuishi katika jamii ya wasio wacha Mungu; na Mungu akaiacha ile miji, endapo angepata watu kumi wenye haki ndani yake (Mwa. 18:32, 25).

Mwishoni, dunia yetu ya uovu imetunzwa hadi Ujio wa Mara ya Pili wa Kristo kwa sababu ya watu wacha Mungu ambao bado wanaishi ndani yake, na kwa sababu Ufalme wa Mungu unakua, kama Yesu anavyoonesha katika mfano wa ngano na magugu (Mat. 13:24-30, 36-42). Magugu yanaruhusiwa kukua, ili kwamba ngano – Ufalme wa Mungu – uendelee kubaki. Ngano itakapokuwa imekomaa na imeijaza dunia, magugu yataharibiwa.

Kama ilivyo muhimu kuchanganua matatizo ya jamii kwa mujibu wa Sheria ya Mungu, Wakristo wana njia moja pekee ya kuitengeneza upya siasa na jamii: "Ikiwa watu wangu, walioitwa kwa jina langu, watajinyenyekesha, na kuomba, na kunitafuta uso, na kuziacha njia zao mbaya; basi, nitasikia toka mbinguni, na kuwasamehe dhambi yao, na kuiponya nchi yao" (2 Nya. 7:14). Kanisa linaweza kuomba kwa ajili ya Jamii na Serikali: Hebu tutumaini ya kwamba Mungu hatatuambia sisi: "Nami nikatafuta mtu miongoni mwao, atakayelitengeneza boma, na kusimama mbele zangu mahali palipobomoka, kwa ajili ya nchi, nisije

nikaiharibu, lakini sikuona mtu" (Eze. 22:30) kama alivyofanya kwa Ezekieli.

Hata ambapo hukumu huonekana kutokuepukika, hebu tusieneze hofu, kujiuzulu na kukata tamaa, bali tuombe kwa ajili ya watu wetu kama Ibrahimu alivyofanya.

Watu wengi wamepoteza tumaini kwa ajili ya Afrika, kwa sababu wanaona tu dalili za kuporomoka. Tumaini halitegemei ukweli unaoonekana, bali hutegemea uingiliaji kati wa Mungu. Wakati Wakriso wa kwanza walipoleta tumaini kwenye Dola ya Kirumi, hali yao haikuwa nzuri – kwa namna nyingine! Historia ya hivi karibuni ya Ulaya Mashariki pia hutukumbusha kwamba hukumu inaweza kuzishukia mamlaka za wapinga-ukristo ili kufungua njia kwa ajili ya Injili!

51. Tumaini ni Zaidi ya Ubashiri

Hoja: Kwa kuwa Yesu anasema waziwazi kwamba mwanadamu hawezi kutabiri siku ya kurudi kwake, matendo yetu lazima yaamuliwe na Amri za Mungu, na si kwa ubashiri wa mambo yajayo.

Yesu anatuonya waziwazi kubashiri juu ya siku yake ya kurudi: "Akawaambia, Si kazi yenu kujua nyakati wala majira, Baba aliyoyaweka katika mamlaka yake mwenyewe" (Mdo. 1:7); "Basi kesheni, kwa sababu hamwijui siku wala saa" (Mat. 25:13).

Hakuna kiashirio chochote kwamba amri yoyote yaweza kutenguliwa kwa kurejea matukio yajayo, hata kama tungedhani kwamba tunajua kikamilifu lini yatatokea. Mungu hututaka tuishi sawasawa na mapenzi yake yaliyofunuliwa waziwazi, siyo sawasawa na matukio ya baadaye, ambayo kwa makusudi ameyafuta kwenye fahamu zetu.

Katika sura ya tatu ya 2 Timotheo, Paulo anatuonya: "Siku za mwisho zitakuweko nyakati za hatari" (2 Tim. 3:1), ambapo "Watu watakuwa wenye kujipenda wenyewe, wenye kupenda fedha, wenye kujisifu, wenye kiburi, wenye kutukana, wasiotii wazazi wao, wasio na shukrani, **wasio watakatifu, wasio na upendo, wasiosamehe**, wasingiziaji, wasiojizuia, **wakatili**, wasiopenda mema, **walaghai**, **wenye pupa**, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu" (2 Tim. 3:2-4).

Timotheo ataishije katika nyakati hizo? Atapaswa kufuata mafundisho ya Paulo na mfano wake (2 Tim. 3:10); atapaswa kuyatii maandiko: "Lakini watu wabaya na wadanganyaji wataendelea, na kuzidi kuwa waovu, wakidanganya na **kudanganywa**. Bali wewe ukae katika mambo yale uliyofundishwa na kuhakikishwa, kwa maana unajua ni akina nani ulijifunza kwao; na ya kuwa tangu utoto umeyajua Maandiko Matakatifu, ambayo yaweza kukuhekimisha hata upate wokovu kwa imani iliyo katika

Kristo Yesu. **Andiko lote lina pumzi ya Mungu na lafaa kwa mafundisho, kwa kukaripia, kusahihisha na kufunza katika haki, ili mtu wa Mungu awe ametayarishwa vema kwa ajili ya kila kazi njema**" (2 Tim. 2:13-17).

Sheria pekee ya kibiblia kwa ajili ya nyakati za uovu ni kushika amri za kibiblia. Badala ya kutoa maelekezo ya maadili maalumu kwa ajili ya Siku za Mwisho, Maandiko hutuamuru: kulihubiri neno la Mungu na kutii amri zake "**wakati ufaao na wakati usiofaa**" (2 Tim. 4:2). Zaidi ya yote, Paulo anamsihi Timotheo: "Fanya kazi ya mhubiri wa Injili" (2 Tim. 4:5). Kuna mbinu moja tu kwa ajili ya Siku za Mwisho, Habari Njema ya Injili, kwamba Mungu hutupatia tumaini hata katika muda mgumu wa maisha yetu na hutupatia matarajio ya mwanzo mpya kwa kupitia usuluhishi na msamaha.

TUMAINI KWA AJILI YA NYANJA ZOTE ZA MAISHA

52. Matengenezo na Uamsho Humaanisha Tumaini kwa Kanisa na kwa Jamii

Hoja: Matengenezo na mavuguvugu yote ya uamsho yamekuwa yakiendeshwa kwa tumaini la uamsho na ufanywaji upya wa Kanisa na wa jamii.

Wanamatengenezo wote wa karne ya 16 walitetea utenganishi wa Kanisa na Serikali, lakini kwa wakati ule ule waliitia moyo jamii kimakusudi ijijenge juu ya tunu na juu ya maadili ya Kikristo. Waliamini kwamba Mungu anataka kulitengeneza upya na kikamilifu Kanisa na Serikali pamoja na kila mtu. Wazo kwamba Luther, Calvin au mwingine yeyote miongoni mwa wanamatengenezo hawakuvutiwa na masuala ya kijamii, au kwamba hawakuwa na matumaini kwa maisha haya, ni ubatili. Wote walitaka kujenga upya jamii pamoja na Kanisa na walifanya kazi kwa lengo hili kwa kuwafundisha watu tunu za kibiblia.

Mababa wa **Upayatisti na wa Mavuguvugu ya Uamsho**, kama vile Philip Jacob Spener, August Hermann Francke, Jonathan Edwards, John Wesley au George Whitefield sio tu kwamba walikutana na wokovu wao binafsi, lakini pia, wakichochewa na ufanywaji upya ndani yao wenyewe, walifanya kazi kuliathiri Kanisa na Jamii kwa manufaa ya maskini na wanyonge. Wote walibadilishwa kwa matumaini yao, na hivyo, kwa wakati wote walishutumiwa kama 'wanamapinduzi'

Programu ya mageuzi ya Kipayatisti ya Philipp Jacob Spener si kwamba ilichochea tu mafuriko ya kazi za kimishenari, bali pia taasisi za kijamii zisizohesabika.[34] August Hermann Francke yeye mwenyewe alianzisha au alitia moyo uanzishwaji wa vituo vingi vya watoto yatima, shule kwa ajili ya maskini, famasia na hospitali nyingi. Shule zake zilizojulikana kama 'Shule Halisi' (kwa Kijerumani 'Realschule'), ambao ni 'uvumbuzi' wa Kipayatisti uliwapatia watoto kutoka familia maskini au

[34] Tazama Helmuth Egelkraut. Die Zukunftserwartung der pietistischen Väter. Theologie und Dienst 53. Brunnen Verlag: Gießen, 1987; Philipp Jacob Spener. Umkehr in die Zukunft: Reformprogramm des Pietismus: Pia desideria. Kimehaririwa na Erich Beyreuther. Brunnen: Gießen, 1975[2]; Pia tazama Martin Schmidt. "Speners 'Pia Desideria': Versuch einer theologischen Interpretation", kr. 113-166 katika: Martin Greschat (Ed.). Zur neueren Pietismusforschung. Wege der Forschung CDXL. Wissenschaftliche Buchgesellschaft: Darmstadt, 1977.

tabaka la kati elimu 'halisi' iliyokusudiwa kuwaandaa kwa ajili ya uhalisia wa maisha. Taasisi za kitawa[35] za Kiprotestanti pamoja na uenezaji wake uliosambaa maeneo makubwa wa misaada kwa maskini, wazee, na wagonjwa, hospitali, vituo vya kulelea wazee, na kwa nyakati za hivi karibuni, vituo vya kusaidia walioathirika na madawa ya kulevya, yote haya ni sehemu muhimu ya historia ya Upayatisti! Viongozi wa Kipayatisti walianzisha programu na orodha ya matakwa kwa Serikali na jamii na walichapisha matini za kuelimisha Serikali na raia wake kuhusu maana ya tunu za Kikristo kwa jamii.

Karibu mababa wa madhehebu yote ya Kikristo – Mababa wa Kanisa, Wanamatengenezo wa Kilutheri kama vile Luther na Melanchthon, wanatheolojia wa kimageuzi kama vile Calvin, Bucer na Knox, Waanglikana kama vile Cranmer, na Mababa wa Umethodisti kama vile (Wesley, Whitefield) na Wabaptisti (hususani wa huko Amerika na Uingereza) walisadiki kwamba Wakristo wanajua vipimo vya haki kwa jamii na watajitahidi kutambua matumaini yao kupitia maombi, mafundisho, usemaji wa unabii na kwa vitendo. Wazo la kwamba Wakristo wanatakiwa wajiondoe kabisa kutoka kwenye jamii, na kwamba tumaini letu binafsi halina matokeo kwenye jamii, ni geni kabisa katika ukiri wa dhehebu lolote!

Wakristo wa Afrika sharti waanze tena kupanda [kusiha] katika tumaini, kama Wanamatengenezo, Wapayatisti, Wanauamsho na wengine wengi walivyofanya, na tufanye kwa malengo ya mbele, siyo tu kwa ajili ya matatizo ya muda mfupi ujao.

Ubinafsi ulioibuka Ulaya na nchi za Magharibi katika miaka 150 iliyopita na ule unaoibuka hapa Afrika umetupotosha kuamini kwamba imani yetu ya Kikristo ni ya kibinafsi kabisa, kwamba haina umuhimu wa kijamii, na kwamba inaweza kuendelea kuwepo bila ushirika katika Kanisa lenye utaratibu mzuri. Tabia hii husababisha kukata tamaa na huondoa tumaini la Wakristo. Tunapoona hakuna hitaji la kuwajibika wenyewe kwa ajili ya wengine, kwa haraka tutapoteza tumaini pia. Ubinafsi huu, wala si Biblia, na si Upayatisti, umesababisha waumini wengi kujiondoa kwenye maisha ya familia, kujiondoa kwenye biashara, siasa na sayansi, na kutupilia mbali ushuhudiaji wa tunu za Kikristo katika maisha ya kila siku.

---

[35] 'Diakonissenmutterhäuser': Taasisi za Kiprotestanti zenye kufanana na makazi ya watawa wa Kanisa Katoliki la Rumi, ambapo 'Wahudumu wa kike' huapa kuishi maisha ya useja na kumtumikia Mungu.

53. Tumaini kwa Wanyonge

Hoja: Tumaini la Kikristo limewalenga hasa maskini, wanyonge na mafukara, kwa kuwa "**Hivyo maskini ana matumaini**" (Ayu. 5:16), "**lakini mhitaji hatasahauliwa daima; wala matumaini ya mteswaji hayatapotea daima**" (Zab. 9:18). Wafungwa waliofungwa kwa kuonewa ni "wafungwa wa tumaini" (Zek. 9:12) na mjane mwenye ukiwa "**huweka tumaini lake kwa Mungu na hudumu usiku na mchana katika maombi na katika kumwomba Mungu msaada**" (1Tim 5:5).

Jamii ya Kiafrika imeathiriwa sana na makundi mengi kama vile Jeshi la Wokovu, Umethodisti, au Wahudumu wa Kike wa Kiprotestanti, yanayojihusisha katika kusaidia makundi mbalimbali ya kijamii. Tunatakiwa kuhuisha jitihada zetu za kumsaidia kila mtu na kumpatia tumaini kama Yesu alivyofanya, hata ikiwa sehemu nyingine ya dunia iliyobaki, au hata Makanisa na Wakristo wengine wamemtupilia mbali.

54. Tumaini kwa Tamaduni Zote na Mataifa Yote

Hoja: Tumaini la Kikristo hutoa tumaini kwa tamaduni zote na kwa mataifa yote. "**Mataifa wataweka matumaini yao katika jina lake**" (Mat. 12:21; tazama pia: Rum. 15:12) Mungu hana upendeleo wa watu (Tazama Hoja ya 61). "Kwa maana twajitaabisha na kujitahidi kwa kusudi hili, kwa sababu tunamtumaini Mungu aliye hai, aliye mwokozi wa watu wote, hasa wa waaminio" (1 Tim. 4:10).

Tangu Mungu achague watu wa Agano la Kale ili kutoa tumaini kwa watu wote, umisheni wa kiulimwengu, yaani utangazaji wa tumaini kwa wote, ni kiini cha Agano la Kale. Ibrahimu, Isaka na Yakobo waliitwa kuwa baraka kwa mataifa yote duniani (Mwa. 12:3; 18:18; 22:17; 26:4; 26:4; 28:14). Hivyo Agano Jipya hutumia ahadi iliyotolewa kwa baba zetu kufanya umisheni miongoni mwa wasio Wayahudi (Luk. 1:54-55, 72; Mdo. 3:25-26; Rum. 4:13-25; Efe. 3:3-4; Gal. 3:7-9,14; Ebr. 6:13-20; 11:12).

Aina anuwai za watu na tamaduni siyo matokeo ya Anguko, bali zilikuwa kusudi asilia la Mungu. Biblia haihukumu sehemu yoyote ya utamaduni wowote ambao haupingi kwa wazi mapenzi matakatifu ya Mungu. Wala aina mbalimbali za tamaduni si matokeo ya adhabu ya ki-Mungu kwenye Mnara wa Babeli (Mwa. 11:1-9). Kinyume chake, Mungu alichanganya lugha ili kutimiza amri yake mwenyewe, ya kumtawanya mwanadamu katika dunia yote ("mkaijaze nchi" Mwa. 1:28; 9:1), jambo ambalo moja kwa moja huongoza kwenye uanuwai wa familia na mataifa, lakini pia wa kazi, uwezo na tamaduni. Kwa kutumia Mnara wa Babeli

Shetani alikusudia kuanzisha utamaduni wa kiulimwengu, ambalo ni lengo lake la daima, kama tuonavyo katika Kitabu cha Ufunuo na kwa Mpinga Kristo. 'Mnyama', anayepokea nguvu zake kutoka kwa 'Joka' (Ufu. 13:1-10) "akapewa uwezo juu ya kila kabila na jamaa na lugha na taifa", lakini Mungu hataki mji wa kiulimwengu wala Uyumanisti wa kiulimwengu. Ni Yeye na Neno lake pekee wawezao kutoa hakikisho la umoja wa dunia, wala siyo taasisi yoyote ya kibinadamu inayoonekana. Alimtawanya mwanadamu katika uso wa dunia nzima (Mwa. 9:1), akianza na watoto wa Nuhu ili kuijaza watu dunia nzima (Mwa. 9:19) mpaka mataifa yakasambaa katika dunia yote (Mwa. 10:5), jambo linaloelezea asili ya mwanadamu kutoka uzao mmoja (Mwa. 10:1-32). Mungu mwenyewe ni mwumbaji wa Mataifa, kwa kuwa "**kutoka katika mwanadamu mmoja alifanya kila taifa la wanadamu, ili waweze kuikalia dunia yote; na aliazimia nyakati zilizowekwa kwa ajili yao na mahali halisi ambapo wanapaswa kuishi**" (Mdo. 17:26; Tazama pia Kumb. 32:8; Zab. 74:17). Hivyo Wakristo wako huru na kizuizi chochote cha kiutamaduni. Hakuna mapokeo au sheria za kibinadamu zinazotufunga mbali na Sheria ya Mungu. Marko 7:1-13 hudhihirisha hili wazi wakati Yesu anapowakosoa Mafarisayo, ambao waliuinua utamaduni wao wa kibinadamu kwa kiwango sawa na sheria ya ki-Mungu. Wakristo wanaweza kuzihukumu tamaduni nyingine kulingana na viwango vya kibiblia wanapokuwa wamejifunza kutofautisha kati ya utamaduni wao wenyewe (ikijumuisha utamaduni wa dini yao wenyewe) na Sheria halali ya Mungu iliyo juu ya utamaduni. Tena, Marko 7:1-13 ni mfano mzuri. Mafarisayo walikuwa na nia zenye kuheshimika katika kutengeneza kanuni nyingine zaidi mbali na Sheria ya Mungu na katika kuzipandikiza sheria hizi kwa sehemu yote iliyobaki ya jamii yao. Hata hivyo, Yesu anawakosoa, kwa sababu katika kufanya hivyo, walikuwa wamejitwalia jukumu la Mungu mtoa-sheria, hivyo kuwa sawa na Mungu: "**Nao waniabudu katika ubatili, mafundisho yao ni sheria zinazofundishwa na wanadamu tu**" (Mk. 7:7; Mt 15:9).

Kwa sababu sisi ni wa Kristo peke yake na tuko chini ya neno lake peke yake, tunaweza kuchunguza kwa makini utamaduni wetu wenyewe na tamaduni za wengine, na kwa upendo tunalazimika kuzitohoa [kuzichukua na kuzitumia] tamaduni za wengine. Paulo anahalalisha umuhimu wa kuishi kwa kulingana na tamaduni za wengine katika kufanya injili kwa kurejea uhuru wake kwa watu wote (1 Kor. 9:19-23). "**Ingawa niko huru na siko chini ya mtu yeyote, najifanya mwenyewe kuwa mtumwa kwa kila mtu, ili niwapate wengi kadri iwezekanavyo. Kwa Wayahudi nilikuwa kama Myahudi, ili niwapate Wayahudi. Kwa wale walio**

chini ya sheria nilikuwa kama mtu aliye chini ya sheria (ingawa mimi mwenyewe siko chini ya sheria), ili niwapate wale walio chini ya sheria. Kwa wale wasio na sheria nilikuwa kama mtu asiye na sheria (ingawa siko huru mbali na sheria ya Mungu bali niko chini ya sheria ya Kristo), ili niwapate wale wasio na sheria. Kwa walio dhaifu nilikuwa dhaifu, ili niwapate walio dhaifu. Nimekuwa katika hali zote kwa watu wote ili kwamba kwa njia zozote zinazowezekana niweze kuwaokoa baadhi yao. Ninafanya haya yote kwa ajili ya Injili, kwamba niweze kushiriki katika baraka zake."

Hivyo, Mkristo anaweza kuishi kwa msimamo mkali sana kulingana na utamaduni wake, kiasi kwamba anashindwa kutambua kwamba, kwa mtazamo mzuri, watu hawamwelewi, lakini katika mtazamo mbaya, anawazuia wengine kuifahamu Injili (1 Kor. 9:12). Hivyo, hatupaswi tu kuwajibika kuwaambia wengine juu ya wokovu katika Kristo Yesu, bali pia kuitangaza Injili katika njia ambayo wanaweza kuielewa. Kwa sababu hii, tunaweza kutafsiri Maandiko katika lugha yoyote inayofikirika, na tunaweza – na ni lazima – tuieleze Injili katika kila lahaja na katika kila muundo wa kiutamaduni.

Lipo tumaini kwa Afrika. Si kwamba watu wa Ulaya wako karibu na Mungu au ni wa maana sana kuliko watu wengine. Kinyume chake, Mungu huyapenda mataifa yote, hata Waafrika, bila kujali yote tuliyoyafanya hapo nyuma.

55. Tunahitaji Kueleza Tumaini Letu katika Hali ya Kueleweka Zaidi Kuhusu Nyanja Zote za Maisha na Uumbaji

Hoja: Tumaini la Kikristo hujumuisha Uumbaji wote, katika utimilifu wake wa milele na pia kwa ajili ya wakati wetu wa sasa. Ukombozi wa mwisho wa Uumbaji utajumuisha ulimwengu wote wa viishivyo. "**Kwa maana uumbaji uliwekwa chini ya mkanganyiko, siyo kwa uchaguzi wake wenyewe, bali kwa mapenzi ya yeye aliyeutiisha, katika tumaini**" (Rum. 8:20; Tazama pia mstari wa 24). Hivyo, taswira ya Yohana ya Mbingu mpya na Dunia mpya hujumuisha si wanadamu tu bali pia dunia yenyewe (Tutazungumzia uhifadhi katika kipengele kingine hapo baadaye).

Biblia haijihusishi tu na imani binafsi ya mtu; pia huzungumzia masuala mengi ya kijamii, kama vile masuala ya kifamilia, kiuchumi, kimahakama, kiraia na ya kitaasisi. Je, masuala kama urithi, uleaji mtoto, ustawi, madeni, kupanda kwa gharama za maisha, rushwa, mishahara,

kodi, ukahaba, ubakaji, mali isiyohamishika, fidia, mahakimu, wafalme, matumizi ya jeshi, malipo ya uzeeni, ulinzi binafsi, uhifadhi, usemaji uongo baada ya kuapa, utoaji mimba, faida, mahitaji ya walemavu, n.k. yanahusu watu binafsi *pekee*? Nasisitiza *pekee* kwa sababu, kwa kuwa mifumo yote ya kimaadili ya Kikristo na mabadiliko yoyote huanza na maisha ya mtu mmoja, jaribio lolote la kuzuia umuhimu wa Biblia kuhusu maisha binafsi limeshahalalishwa kushindwa. Maandiko yamefurika Utaratibu wa Uumbaji wa Mungu kwa ajili ya ujumla wa kuishi wa mwanadamu. Kuzipunguza sheria zake na kuzifanya kuwa zinazohusu masuala binafsi ni sawa na kuzikana Amri za Mungu. Kama John Warwick Montgomery anavyosema, mtu yeyote anayeuelewa Ukristo ulivyo hasa, moja kwa moja hujua pia maana yake kwamba unawatarajia wafuasi wake kiuhalisia kupinga maovu ya jamii na kufanya jitihada ya kurahisisha mahitaji ya binadamu.[36]

Katika kurasa zifuatazo, ningependa kujadili nyanja kadhaa za maisha: familia, uchumi, sheria, siasa na uhifadhi. Natumaini kwamba mawazo yangu yatachochea mjadala katika masuala mengine zaidi na ya kwamba wataalamu katika nyanja mbalimbali na mabingwa watatafsiri wito wetu katika istilahi yao wenyewe kwa ajili ya wenzao. Moja ya changamoto kubwa ya Afrika ni kutafuta kanuni halisi za tumaini la kibiblia kwa ajili ya maisha ya kila siku katika nyanja zote za maisha, katika taaluma zote na katika majukumu yote.

Mapitio: Vyanzo vya Maadili ya Kiinjili

Kabla ya kujadili mitazamo mbalimbali ya maisha ya kijamii, ningependa kuchunguza mahusiano kati ya tumaini la kibiblia, ufunuo wa ki-Mungu katika Maandiko na ufahamu wa kibinadamu. Alister E. McGrath anaandika: “Kwa ujumla, utamaduni wa Kikristo umevikubali vyanzo vikuu vinne: 1. Maandiko, 2. Mantiki (Akili), 3. Desturi, 4. Uzoefu.”[37] Nje ya vyanzo hivi, tunaweza kujumuisha mamlaka ya kikanisa, hali halisi na utamaduni ambao sisi tumo (yote haya yanajumuishwa kwenye orodha ya McGrath).

---

[36] John Warwick Montgomery. Christians in the Public Square. Law, Gospel and Public Policy. Canadian Institute for Law, Theology and Public Policy: Edmonton (CAN), 1996, uk. 30.

[37] Alister E. McGrath. Der Weg der christlichen Theologie. C. H. Beck: München, 1997, uk. 189; Tazama toleo lililosheheni taarifa katika Rud., kr. 189-243 (Sura 6: “Die Quellen der Theologie”). Vernunft und Erfahrung neben der Schrift diskutiert Martin Honecker. Einführung in die Theologische Ethik. Walter de Gruyter: Berlin, 1990, kr. 187-202.

Kwa Maadili ya Kiinjili, Neno la Mungu ndilo kipimo kisichoshambulika cha mwisho na cha pekee, ni kigezo kwa ajili ya mamlaka nyingine zote (Kwa Kilatini: 'norma normans', yaani kipimo kwa ajili ya vipimo vingine vyote). Lakini je, vyanzo vingine kama vile mamlaka ya kikanisa, mawazo, hekima, uzoefu au hali halisi na utamaduni vina thamani gani? Je, vyaweza kukataliwa kwa sababu Biblia ina mamlaka iliyo kuu? Au vyaweza kuhitajika katika maamuzi ya kimaadili? Desturi, uzoefu na hali (au utamaduni) siyo vyanzo pekee vya maadili, bali ni maana za kale tu kwa ustaarabu wetu, neno tunalolitumia kuelezea jinsi tunavyopokea mitazamo mizuri na sahihi ya ulimwengu.

Wazo lilililokuzwa kupita uhalisia la kitauwa zaidi kumpita Yesu au mitume hujaribu kuitupilia mitazamo hii mbali na maadili. Wakidai kujizoesha katika Biblia tu, wafuasi wa mtazamo huu hukataa vipimo au mapendekezo mengine yoyote. Kwa kawaida, jambo hili halina uhalisia. Hakuna mtu awezaye kuishi kwa kulingana na Maandiko tu, na hakuna mtu asiyeweza kutofautisha kati ya wema na ubaya katika mambo ambayo Biblia haijayaelezea kwa uwazi. Kwa mfano, twaweza kutafuta hoja dhidi ya uvutaji, ingawa Maandiko hayazungumzii tumbaku; na uvutaji hauwezi kutajwa kama 'dhambi'. Katika hali ya kawaida, ni suala lisilo la kiafya, lililo kinyume na jamii na lisilo la hekima.

Mpaka mahali hapa, ningependa kuwakumbusha wasomaji wangu kwamba wazo kama hilo ni geni kabisa katika Biblia, ambalo kwa kurudiwa rudiwa hutusihi tufuate hekima na uzoefu wa wengine kwa dhati, tutilie maanani maonyo ya viongozi wa watu wa Mungu au ya watu wengine walio katika mamlaka na tujifunze kutoka kwenye historia. Mbali na hilo, waandishi wa Biblia pia hutoa hoja zao kutokana na uzoefu au mantiki. Kama tukiichukulia Biblia kama mamlaka yetu iliyo kuu, ni lazima pia tushike usihi wake wa kukubali ushauri, hekima, uzoefu, mantiki na maelekezo yatolewayo na viongozi wa kikanisa au wa kidunia. "Hitaji hili la kupata ufahamu wa nje ya Biblia ili kuifahamu Biblia si hitaji lenye kutaabisha. Ni la kiasili, ni sehemu ya kawaida ya wajibu wetu, na Mungu anatutarajia tulifanye."[38]

Ni kweli Mungu ameweka mipaka kadhaa katika Biblia, lakini kwa kufanya hivyo, ametupatia uhuru mkubwa sana. Mawazo ya kibinadamu, yaliyopotoshwa chini ya laana ya Anguko, yanaweza kuwa silaha hatari katika mikono ya Shetani, lakini kama sehemu ya mpango bunifu wa Mungu iliyothaminishwa kwa mwanadamu kama taswira (mfano) wa Mungu, yanaendelea kusafishwa na kubadilishwa kwa ajili ya malengo ya

[38] John M. Frame. The Doctrine of the Knowledge of God: A Theology of Lordship. Presbyterian & Reformed: Phillipsburg (NJ), 1987, uk. 67; Tazama pia kr. 66-68.

Mungu wakati mtu binafsi anapotubu na kumgeukia Mungu. Kwa sababu hii, Wakristo wanaweza kuwa watu wenye utambuzi na wenye kufikiri. Maandiko hutupatia mfumo wa maadili ya amri, lakini pia mfumo wa maadili ya hekima. Pamoja na kanuni na mipaka kamilifu, tunapaswa kujifunza kutokana na uzoefu wa maisha na kutokana na hekima, mambo ambayo huamua hali halisi vema na hufanya maamuzi ambayo yangeweza kuwa si sahihi katika hali nyingine. Mungu alimwumba Mwanadamu katika uanuwai wa tamaduni, na hakutukusudia kamwe sisi sote kufikiri, kuhisi au kufanya kazi katika njia zinazofanana.

Ufunuo wa Mungu lazima uwe chanzo cha mawazo yetu, lakini siyo mbadala wa kufikiri na kupanga. “Kumcha BWANA ni mwanzo wa hekima” (Mit. 9:10; 7:1), siyo mwisho wake.

Hata hivyo, maadili ya ‘Sheria Asilia’ yana uhalali fulani kwa waumini. Kadri Neno la Mungu linavyoendelea kuamua juu ya mawazo yetu, maadili asilia au yanayolingana na hali ilivyo yana halalisho la kawaida lakini sio lile la mwisho kabisa. Serikali huhitaji maadili kadhaa ya msingi yajumuishayo ulinzi wa maisha ya mwanadamu. Kwa kupewa msingi huu wa maadili, basi serikali itatunga kanuni zake nyingi na sheria nyingine kutokana na namna jambo lilivyo. Katika kile kinachotokea na kwa haraka kiasi gani, si ufunuo wa Mungu au vitabu vya kiada vya Kikristo vitakavyoamua mwendo au uharaka wake.

Mfano mzuri wa mwingiliano wa maarifa ya kibiblia na sayansi yenye msingi wa kibiblia unaweza kupatikana katika suala la utoaji mimba na uzazi wa mpango.[39] Hadi wanabaiolojia walipogundua mwunganiko wa mbegu za kiume na yai la mwanamke, ndipo tulipotambua ni wakati gani maisha ya mwanadamu huanza. Tangu hapo, Wakristo husisitiza kwamba mtu ni mwanadamu tangu wakati wa utungaji mimba na kwamba kukatiza mimba kwa aina yoyote ile ni uuaji wa binadamu. Wakati ule ule, ilikuwa inawezekana kuidhinisha aina fulani ya uzazi wa mpango, kwa sababu hakuna maisha ya mwanadamu yanayokuwepo kabla ya mimba kutungwa, na kwa sababu, tofauti na mawazo ya hapo mwanzo, kuzuia utungaji mimba hakuharibu uhai wa mwanadamu.

Mfano mwingine ni uleaji wa mtoto. Je, inawezekana kulea watoto kwa kutumia Biblia peke yake? Kwa kweli haiwezekani – Biblia haizungumzii juu ya matatizo ya kiafya, juu ya kiasi cha usingizi watoto wanachohitaji, juu ya mfumo wa heshima, juu ya umri wa watoto shuleni au juu ya posho.

---

[39] Tazama Richard M. Fagley. The Population Explosion and Christian Responsibility. Oxford University Press: New York, 1960, kr. 192-193.

Maandiko hutupatia kusudi la Mungu na kanuni za jumla za kumlea mtoto, ambazo tena hutofautisha jinsi ya kumlea mtoto kibiblia na mifumo mingine. Wazazi wanatakiwa "**kuwalea katika mafunzo na maelekezo ya Bwana**" (Efe. 6:4), kuwafundisha kumpenda Mungu na Neno lake (2 Tim. 3:14-17) na kuwaandaa kuishi maisha ya kujitegemea kulingana na sheria asilia za Mungu na chini ya mamlaka yake. Nje ya miongozo hiyo ya jumla, Biblia ina amri au mapendekezo machache tu kama vile adhabu zinazoumiza mwili au juu ya matumizi ya mifano ya Biblia (kwa mfano kuhusu Sheria: Kumb. 4:9-10; 6:4-9, 20-25; 11:18-21; 31:12-13; 32:7; Yosh. 4:6-7; Zab. 78:5-8; Mith. 22:7; kuhusu Pasaka Kut. 12:26-27; 13:14-16. Tazama pia 13:6-10). Pindi wazazi wanapokuwa wamekubali amri hii ya kisheria ya kibiblia na ya kimsingi, kwa kawaida wataunda njia zao wenyewe kutokana na 'hali ya jambo lilivyo'. Ukuaji binafsi wa mtoto wa kimwili na kiakili utaongoza maamuzi [yetu] mengi na mara nyingi yatahusisha ulinganishaji na yale ya watoto wengine – na ushauri wa wasio Wakristo waweza kuwa na msaada!

Mbali na hayo, wazazi wa Kikristo sharti watafsiri kanuni hizi za jumla katika uhalisia wa maisha ya kila siku. Kwa kufanya hivyo, wanatumia uzoefu wa vizazi vilivyopita (desturi), ushauri wa kisasa, na masomo ya kisayansi, na wanatumia utambuzi wao kutafuta suluhisho bora kwa ajili ya watoto wao, jambo ambalo haliwezekani kwa mtu asiye na uzoefu na hali halisi ya mtoto. Maamuzi ya mwisho huhitaji ufahamu wa usuli wa utamaduni wa mtoto, ukoo wa familia yake na mazingira yake.

Mungu hutarajia na huamuru watu wote kutumia vipawa walivyopokea. Wazazi wanaweza tu kuwatia moyo watoto wao kufanya hivi kwa kuwachunguza ili kutambua uwezo wao na mapendeleo yao, na kwa kutumia akili zao ili kuimarisha mbinu halisi.

Hatari tatu sharti ziepukwe. Ya kwanza ni kuhukumu papo hapo chanzo chochote cha maadili au maelekezo nje ya Biblia, jambo ambalo kiuhalisia humaanisha kwamba mtu huyo hatambui athari ambazo zimeunda mawazo yake mwenyewe. Ya pili ni kulinganisha maamuzi yenye mantiki au uzoefu wa wengine na sheria ya Mungu, kama ambapo waandishi wa Kikristo kimakusudi hutoa maagizo ya maelekezo, ingawa sisi sote tunajua kwamba kila mtoto ni tofauti; wazazi wenye watoto watatu kwa urahisi wanaweza kuandika vitabu vitatu vilivyo tofauti kabisa! Hatari ya tatu ni kuzama kwenye mantiki na uzoefu na kutupilia mbali maelekezo ya kibiblia.

Hivyo, Mungu ametupatia lengo la msingi la uleaji mtoto, na akili na hekima ya kutafuta njia bora kwa ajili ya watoto wetu wenyewe!

56. Tumaini la Kibiblia Dhidi ya Tumaini Danganyifu la Maadili ya Kibwanyenye

Hoja: Biblia haitambui maadili ya kiraia yasiyoegemea upande wowote ambayo huunda kazi, bidii ya kazi, familia, umiliki au utajiri, n.k. kuwa tunu kamilifu, bali ni tunu tu ambazo Mwanadamu, kama sehemu ya Uumbaji, amezipokea kutoka kwa Mungu, na ambazo anazitumia kwa shukrani na kwa kumtegemea Mungu.

Kitabu cha Mhubiri hudhihirisha jambo hili kwa uwazi zaidi. Baadhi wamemlalamikia mwandishi wake kuwa asiyetarajia mema na asiye mcha Mungu. R. B. Y. Scott anahitimisha kwamba ni lazima [Mhubiri] alikuwa mrazini, asiyeamini juu ya Mungu, mtarajia mabaya na mtarajia majaaliwa,[40] na kwamba mfumo wa kimaadili wa Mhubiri hauna msingi katika amri za Mungu, kwa kuwa hauna [amri hizo] hata moja.[41] Kwa kuwa mwandishi anakubali kwa urahisi majaaliwa yake, chote kinachobaki kwake ni starehe. Hata hivyo, mgawanyo bora wa kitabu,[42] unapingana na mtazamo huu kwa uwazi kabisa, kwa kuwa dhamira inayorudiwarudiwa ya kufurahia maisha ya dunia katika 2:24-26; 5:17-19; 8:15-17; 11:7-10 huunda hitimisho la sehemu kuu nne[43] [za Kitabu]. Hivyo basi, kila sehemu moja huishia na usihi wa kufurahia maisha kikamilifu na kuishi katika wakati wa sasa na siyo katika muda kitambo ujao. "Taswira [mifano] hasi huunda mwanzo [wa kila sehemu], taswira au mifano iliyo chanya huunda hitimisho la kila maelezo."[44] Furaha za maisha zinasisitizwa kwa uwazi mara nane (2:24-26; 3:11-14,22; 5:17-19; 8:15; 9:7-10; 11:7-10; tazama pia 12:1). Maneno yaliyotokana na mzizi wa neno la Kiebrania 'smh' (furaha, starehe) hujitokeza mara 17. Furaha ni muhtasari wa kitabu. "**Mwanadamu hawezi kufanya jambo lolote bora kuliko kula na kunywa, na kujipatia ridhiko katika kazi yake. Hili pia, naona linatoka katika**

---

[40] R. B. Y. Scott. Proverbs, Ecclesiastes. Anchor Bible. Doubleday: Garden City (NY), 1965, p. 191. Scott hakusudii maelezo yake kuwa hukumu holela.

[41] Rud., uk. 192.

[42] Tazama Walter C. Kaiser. Ecclesiastes: Total Life. Everyman's Bible Commentary. Moody Press: Chicago, 1979; and Addison G. Wright. „The Riddle of the Sphinx: The Structure of the Book of Qoheleth", kr. 45-66 katika: Roy B. Zuck (Ed.). Reflecting with Solomon. Baker Books: Grand Rapids (MI), 1994 [aus Catholic Biblical Quarterly 30 (1968), kr. 313-334].

[43] Donald R. Glenn. „Der Prediger". pp. 651-696 in: John F. Walvoord, Roy F. Zuck (Ed.). Das Alte Testament erklärt und ausgelegt. Vol. 2: 1. Könige - Hohelied. Hänssler: Neuhausen, 1991. p. 655 (Toleo Asilia la Kiingereza: Bible Knowledge Commentary Old and New Testament, here Ecclesiastes).

[44] Hans Möller. Alttestamentliche Bibelkunde. Lutherische Buchhandlung: Groß Oesingen, 1989. uk. 194.

mkono wa Mungu, kwa kuwa pasipo yeye, ni nani awezaye kula au kujipatia furaha? Kwa mtu anayempendeza yeye, Mungu hutoa hekima, ufahamu na furaha, lakini kwa mwenye dhambi hutoa jukumu ya kukusanya na kuhifadhi utajiri ili kumpatia mwenye kumpendeza Mungu. Hili pia halina maana, ni kuufukuza upepo" (Mhu. 2:24-26).

Kutambua Ubatili wa Maisha Hutuongoza kwenye Furaha

Sehemu	*Kile ambacho niUbatili*	*Usihi wa Furaha*
1:12-2:26	Kazi ya Mwanadamu	2:24-26
3:1-15	Kutojulikana kwa mambo yajayo	3:12 (11-14)
3:16-22	Udhalimu duniani	3:22
5:9-19	Kusumbukia utajiri	5:17 (17-19)
8:10-15	Uovu usioadhibiwa	8:15
9:1-10	Uhakika wa kifo	9:7-9
11:7-12:7	Uzee na kifo	11:9-10; 12:1

Inawezekanaje mhubiri kutoka kwenye mtazamo wa kutarajia mabaya tu na kwenda kwenye furaha kwa ghafla namna hiyo? Je, anakwepa matatizo? Hapana, anamgeukia Mungu na kutambua kwamba mambo yote "hutoka mkononi mwa Mungu" (2:24-26). Hali zinazoonekana kukosa maana na zisizo na matumaini kwa mwanadamu, huwa na maana wakati Mungu, Muumbaji na Mlinzi avutapo usikivu wetu, na wakati tunapoishi maisha ya kumpendeza yeye (2:26).

Kusudi la Mhubiri ni kuonesha ubatili wa kazi, wa bidii ya kazi, wa familia au katika mali zenyewe, pasipo Mungu; na kumtia moyo mwanadamu kuyapokea mambo haya kama zawadi kutoka kwa Mungu, na kuyatumia chini ya usimamizi wake. Kama Donald R. Glenn alivyoliweka hili, Mhubiri anafanya ukosoaji halisi dhidi ya uyumanisti wa kisekyula wa kisasa[45]. Bila Mungu, "ni nani awezaye kula au kujiburudisha?" (2:5), "**Hii ni karama ya Mungu – kila mtu apate kula na kunywa, na kujipatia ridhiko katika kazi yake yote**" (3:13).

[45] Donald R. Glenn. op. cit., uk. 655.

Wazo la maadili ya kiraia yasiyoegemea upande wowote siyo la Kibiblia. Mambo kama kazi, bidii ya kazi, familia, mali au utajiri, yenyewe kama yalivyo si thamani [tunu au amali], bali vina thamani tu kama zawadi kutoka mkononi mwa Mungu, ambazo mwanadamu anaweza kuzitumia kwa shukrani na kwa kumtegemea yeye. Kitabu cha Mhubiri kinavunjavunja mfumo-tunu wa maadili wa kiraia, lakini inaufufua tena chini ya mwumbaji wakati unapokubaliana na maagizo ya Mungu. Wakati watu waijiapo imani hai katika Kristo, kiurahisirahisi tu hawawezi kuendelea na tunu zile zile walizokuwa nazo, bali ni lazima wazijaribu na kuziacha zisafishwe katika moto wa Mhubiri, ili kwamba zijengwe juu ya msingi wa Neno la Mungu na siyo katika mawazo ya kistaarabu ya 'ustahivu'.

Siyo wajibu wetu kuelewa kila kitu, kufikiria matokeo yote yanayowezekana na kufahamu maana ya kila kitu. Wajibu wetu ni kuishi tukiwajibika mbele za Mungu, kufanya kazi, kufurahi na kuitengeneza dunia, kama tulivyoipokea kutoka kwa mwumbaji, kwa kuwa hata mambo yanayoonekana kututaabisha na batili kwetu yametoka kwa Mungu. "Nimeiona taabu ambayo Mungu amewapa wanadamu" (Mhu. 3:10).

Maadili ya kiraia huvunjikavunjika wakati kazi, mali na familia vinaposhindwa. Hata hivyo, kwa maadili ya kibiblia, majanga siyo mwisho wa maisha. Maadili ya kibiblia hutoa tumaini siyo tu katika wakati wa mafanikio na ustawi, kama maadili ya kiraia yafanyavyo, bali ujasiri wake [yaani tumaini] usio na mpaka katika Mwumbaji hutusaidia kukabiliana na mateso pia.

Mhubiri huweka tunu nyingi za kibiblia katika mtazamo; tunu ambazo huwa hatari wakati zinapochukua nafasi ya kwanza katika maisha yetu na kuchukua nafasi ya Mungu. Mhubiri anaonya "**mapato ya ardhi huchukuliwa na wote; mfalme mwenyewe hufaidika kutokana na mashamba. Yeyote apendaye fedha hatakuwa na fedha za kumtosha; yeyote apendaye utajiri hatoshelezwi na mapato yake. Hili pia ni ubatili. Kadri vitu vinavyoongezeka, ndivyo watumiaji wanavyoongezeka pia. Zina faida gani kwa mwenye nazo isipokuwa kuzisherehekea kwa macho? Usingizi wa mtendakazi ni mtamu, iwe anakula sana au kidogo, lakini wingi wa mtu tajiri humkosesha usingizi**" (5:9-12). Utajiri unaweza kuwa chanya na unaweza kufurahiwa, lakini sivyo unapokuwa lengo la maisha, au wa kugandamiza au kuharibu utoshelevu utokanao na kazi. Wakati mambo kama kazi, familia, mali au hekima vinapokuwa malengo pekee, basi na maisha hupoteza mtazamo wake wa milele, maisha hupoteza maana yake. "**Jitihada zote za mwanadamu ni kwa ajili ya kinywa chake, lakini bado hamu yake haitoshelezwi**" (Mhu. 6:7).

57. Tumaini kwa ajili ya Uhifadhi wa Uumbaji[46]

Hoja: Wahifadhi wamefanya uhifadhi wa uumbaji kuwa suala la kisiasa. Wakristo lazima wawakumbushe kwamba hakuwezi kuwa na Uumbaji pasipo Mwumbaji, na ya kwamba tumaini kwa ajili ya Uumbaji humaanisha tumaini katika Mwumbaji.

Utawala wa mwanadamu juu ya Uumbaji kimsingi huwahudumia wanadamu, lakini Mungu aliukusudia pia uhudumie Uumbaji. Tofauti na wasiomcha Mungu, yeyote azitunzaye sheria za Mungu za Uumbaji atahudumia Uumbaji pia. "**Mwenye haki hujali mahitaji ya mnyama wake, lakini matendo mema ya mwovu ni ya kikatili**" (Mith. 12:10). Mungu alimpatia Mwanadamu wajibu wa "kuilima" dunia na "kuitunza", kuibadilisha na kuihifadhi. Mawazo haya mawili huonekana kama yanapingana yenyewe kwa yenyewe, lakini katika maisha ya kila siku hayatenganishwi; yako pamoja kama pande mbili za shilingi.

Katika jamii ambayo imejengwa imara kwa Ukristo, vuguvugu la wahifadhi wa kisasa huvuta hisia kwa matumizi yake ya neno 'Uumbaji' walau katika lugha mbalimbali za Ulaya kama Kijerumani na Kifaransa. Bila kutarajia, hulitumia neno hilo vibaya, kwa sababu hudharau Asili na hukana tofauti kati ya mwanadamu na viumbe vingine, badala ya kufikiri katika dhana ya Mwumbaji. Kwa upande mwingine, Biblia hufundisha kwamba mwanadamu anaweza tu kuihifadhi dunia wakati anapomheshimu Mungu na kutunza sheria za Mungu. Wakati Wakristo wanapofanya kazi ya kuyatunza mazingira, wanaifanya sawasawa na sheria za Mungu, na si kwa sababu Asili yenyewe ina madai fulani ndani yake. Wakristo ni lazima waanze kujaa wazo la uhifadhi wa Uumbaji kwa kufuata maudhui ya kibiblia.

58. Tumaini kwa Jamii

Hoja: Ingawa wokovu binafsi ni lengo muhimu sana na la kwanza la tumaini letu na huduma yetu ya umisheni, tunaweza kuweka malengo mengine pia. Malengo mengine hujipatia umuhimu wake kutokana na tumaini la wokovu binafsi.

Utume Mkuu katika Mathayo 28:18 -20 hujumuisha ushawishi wa kufanya wanafunzi (wajifunzao). Hatua ya kwanza katika mwelekeo huo ni toba binafsi – ni mtu mmoja mmoja pekee wanaoweza kubatizwa – lakini kama mtu mmoja baada ya mwingine watamgeukia Kristo, mataifa yote

[46] Tazama pia Thomas Schirrmacher. Eugen Drewermann und der Buddhismus. Verlag für Theologie und Religionswissenschaft: Nürnberg, 2000[1]; 2001[2], kr. 71-116.

yataamini. Asilimia kubwa ya waumini haipingi dhana ya uamini wa mtu mmoja mmoja.

Aidha, kuamini siyo mwisho wa ufanywaji upya. Mahusiano mapya ya mtu na Mungu ni mwanzo wa ufanywaji upya ndani yake mwenyewe, katika familia, katika kanisa, katika uchumi, katika serikali na katika jamii. Wote wanapaswa kuwa wanafunzi! Kwa kuwa Yesu anawaambia wanafunzi wake "kuwafanya mataifa yote… na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi", Utume Mkuu humaanisha kwamba Wakristo wanapaswa kujifunza mpangilio mzima wa maadili ya Kibiblia, ambayo baadaye yatambadilisha kabisa mtu na mazingira yake, ili kwamba mwishowe, mifumo ya dhambi na udhalimu ionekanayo ishindwe.

Amani ya mtu binafsi na Mungu, wokovu wake binafsi kupitia dhabihu ya neema ya Yesu Msalabani ni lengo la kwanza na lililo muhimu kabisa katika umisheni, ambalo huamua malengo yote ya baadaye. Katika Mathayo 16:26 Yesu anasema kwa uwazi kabisa kwamba wokovu wa nafsi ni wa muhimu zaidi kuliko kitu kingine chochote. "Kwani atafaidiwa nini mtu akiupata ulimwengu wote, na kupata hasara ya nafsi yake? Au mtu atatoa nini badala ya nafsi yake?" Paulo anatumia hoja ile ile kwamba Wayahudi na Wayunani wamepotea katika dhambi zao, na kwamba ni Yesu pekee anayeweza kufanikisha wokovu wao, kabla hajaelezea mada ya maadili ya kijamii, kiutamaduni na kisiasa. "**Kwa hiyo, kwa kuwa tumekwisha kuhesabiwa haki kwa njia ya imani, tuna amani na Mungu kwa njia ya Bwana wetu Yesu, ambaye kwa yeye tumepata njia ya kuifikia neema hii kupitia imani ambayo kwayo tunasimama**" (Rum. 5:1-2a).

Katika Hotuba Mlimani Yesu anawapa changamoto Wakristo kuiangazisha nuru yao na kuwa chumvi ya dunia. Mara baada ya Heri, anatumia mifano hii kuonesha kwamba waumini hawaishi na kufanya kazi kwa ajili yao wenyewe (Mat. 5:13-16). Anatuasa kutenda kazi kabla ya wengine na kwa ajili ya wengine: "Vivyo hivyo nuru yenu na iangaze mbele ya watu, wapate kuyaona matendo yenu mema, wamtukuze Baba yenu aliye mbinguni" (mst. 16).

Katika kushindwa kufuatilia kwa bidii ustawi wa jamii yetu, tunakubaliana na viwango vya mazingira yetu. Hakuna mtu anayeweza kuishi bila viwango na maadili. Kama hatuwezi kujitahidi tuwezavyo kutambulisha maadili ya Kikristo katika dunia yetu, au kama twaamini kwamba viwango vyetu havifanyi kazi na jamii, lazima tutafute maadili yetu sehemu nyingine – yamkini katika jamii yetu. Klaus Bockmühl, profesa wa Elimu-maadili aliwahi kuandika, "Hatari kubwa ya fikra za 'mashua okozi' au 'mahali pa faragha' ni kwamba wafuasi wake huendelea

kushiriki katika maisha ya jamii bila kuuliza na mara zote wakiwa na mafanikio makubwa. Wakikuta suala lile halina mwongozo wa ki-Mungu, hawana uchaguzi mwingine bali kununua na kuuza kwa kulingana na kanuni za kienyeji, na kusalimisha yote chini ya utawala wa 'Mfalme wa dunia hii'".[47]

59. Tumaini kwa Familia

Hoja: Umisheni na ujumbe wa tumaini huanza katika makanisa ya Kikristo na katika familia, ambao hufundisha neno la Mungu kwa ki-zazi kijacho kwa njia ya mifano, nidhamu na elimu.

Hatuwezi kuthubutu kuacha kulihubiri Neno la Mungu kwa wasio Wakristo, lakini familia ya Kikristo isisahauliwe hata kidogo, kwa kuwa familia ya Kikristo yenye siha ni sifa ya uongozi katika Kanisa la Agano Jipya (1 Tim. 3:4-5, 12-13; Tit. 1:6-7). Wakati tunapowaachilia watoto wetu kwa Serikali, tunahitaji kufanya jitihada nyingine zaidi kuathiri makanisa yetu, uchumi wetu, jamii yetu au Serikali yetu, kwa kuwa tumeacha mbinu nzuri zaidi ya kuwabadilisha kwa ajili ya maisha ya baadaye.

Kuwalea watoto wetu ni hatua muhimu sana kuelekea katika kuwapatia tumaini na siasa za kijamii, kwa sababu tunawaandaa binadamu kwa maisha yao yote, tukiwafundisha tunu na kanuni za msingi za mahusiano ya kijamii. Mungu aliumba familia ili kizazi cha watoto kiweze kujifunza viwango vya kibiblia kwa ajili ya ustawi wa jamii nzima kutoka kwenye vielelezo vya majukumu ya wakubwa wao. Ni mahali gani pengine watu hujifunza kuwa wenye kujali, wasio na wivu, kuwasaidia wanyonge au kuwasifu wengine, kama si nyumbani? Hebu tusitupilie mbali nyanja za maisha ambazo Mungu ameziweka mikononi mwetu! Hebu tutumie fursa tulizonazo kuathiri elimu kwa kuanzisha shule za Kikristo na kwa kuwasaidia walimu wa Kikristo katika shule za serikali.

Familia zenye siha na familia za Kikristo zinawezekana tu kama tutahakikisha kwamba nyanja zote zilizoachwa kwetu na jamii na Serikali zinatunzwa salama. Kama tunahitaji kuitunza familia, lazima tusaidie jitihada za Wakristo kuathiri jamii yetu, kwa kuwa jamii yetu huamua kwa kiasi kikubwa kile ambacho familia inaweza kukifanya. Kuharibika kwa familia hutokana na nguvu za kijamii, ambazo zinaweza kuzuiliwa wakati familia zinapoanza kuiathiri jamii kwa manufaa yao. Majaribio ya Ukomunisti kuharibu familia ya Kikristo yanajieleza yenyewe.

---

[47] Klaus Bockmühl. Theologie und Lebensführung: Gesammelte Aufsätze II. TVG. Brunnen: Gießen, 1982, uk. 131.

Familia ya kisasa imepoteza mamlaka yake na kazi zake muhimu sana kwa kutimiza sehemu tu ya majukumu yake ya awali yanayobaki ya uchumi, elimu na ustawi wa jamii. Wakati familia inapotupilia mbali majukumu yake muhimu, nyumbani si mahali pa kazi tena, mahusiano ya kimapenzi ya wasiooana hulinganishwa na ndoa; wazee, wagonjwa na wasiojiweza hutengwa kwenye 'makazi maalum'. Ni pale tu tunu za Kikristo zinapofufuliwa, ndipo maisha ya familia na majukumu ya familia yanapoweza kujengwa tena.

60. Tumaini kwa ajili ya Uchumi

Hoja: Kwa kuwa tuliumbwa na hitaji la tumaini la kutia hamasa jitihada zetu za kikazi na kiuchumi, maono yetu ya siku zijazo kwa sehemu kubwa huamua maadili yetu ya kiuchumi.

Akizungumzia kazi yake ya umishenari, Paulo aliandika: "**(kwa ajili ya hili twajitaabisha na kujitahidi), kwamba tumeliweka tumaini letu kwa Mungu aliye hai, ambaye ni Mwokozi wa watu wote, na hususani wa wale waaminio**" (1 Tim. 4:10) na "**Wakati mkulima atumiaye plau alimapo na apuraye nafaka apurapo, wanapaswa kufanya hivyo kwa tumaini la kushirikiana katika mavuno**" (1 Kor. 9:10). Kwa kuwa umisheni ni mtazamo mmojawapo tu wa kazi, anatumia kanuni ile ile kwa majukumu ya wazee (1 Tim. 5:17-20; 1 Kor. 9:9-18).

Ingawa Wakristo wengi hushindwa kuelewa ukubwa wa matokeo ya kijamii ya baadhi ya amri za kibiblia au Kikristo, wachambuzi wa mambo wa kisekyula hutambua kwamba kanuni za Kibiblia zina matokeo mazuri ya kivitendo katika uchumi. Helmut Schoeck, profesa wa Sosholojia (Elimujamii), akiandika juu ya hukumu ya kibiblia juu ya wivu katika Amri Kumi na katika maneno ya Yesu, anasema, "Agano Jipya daima huzungumza juu ya mtu mwenye wivu, na linamsihi kuvumilia tofauti kati yake mwenyewe na jirani yake katika hali ya ukomavu na kama Mkristo. Katika jamii ya Kimagharibi, maadili ya Kikristo yamelinda na kuchochea nguvu ya ubunifu wa mwanadamu, na yamefanya umbali wa mafanikio yake uwezekane kwa kupinga tamaa."[48] Wale wanaorutubisha wivu hutupilia mbali mafundisho muhimu ya imani ya Kikristo na huigeuza jamii kuwa uwanja wa vita wenye kutisha.

[48] Helmut Schoeck. Der Neid und die Gesellschaft. Ullstein: Frankfurt, 1987[6].

61. Tumaini kwa ajili ya Mfumo wa Kisheria

Hoja: Tumaini la Kikristo kwa ajili ya hukumu ya Mungu iliyo jumuishi na isiyohongeka hutuchochea kutafuta ukweli na haki hapa duniani, ingawa [haki] inaweza kuwa isiyo kamilifu na daima ikikabiliwa na kitisho cha uovu na madhaifu ya kibinadamu.

Daima tumaini hujengwa kwenye matarajio ya haki, lakini pasipo Mungu, tunajifunza kutokana na uzoefu: "**Twatafuta haki, lakini hatupati chochote; ukombozi, lakini u mbali nasi**" (Isa. 59:11). Hata hivyo, mwamini hujua kwamba: "**Lakini kwa imani tunasubiria kwa hamu kwa njia ya Roho haki ambayo tunaitarajia**" (Gal. 5:5). Vyovyote tunavyoyatafsiri mafundisho ya Biblia juu ya Hukumu ya Mwisho, iwe tunaamini kwamba haki itatarajiwa au inaweza kutarajiwa kabla ya hukumu au la, utafutaji wowote wa haki hupata umuhimu wake na hadhi yake mahali hapa.

Mizizi ya serikali ya kikatiba huegemea kwenye aina ya mawazo ya kifalsafa, lakini msingi wake wa awali ni mafundisho ya sheria ya Maandiko (Biblia). Aina yoyote ya ukanaji wa msingi huu huifanya haki kuwa jambo la kubadilikabadilika.

Haki ya msingi ya kiraia ya kujipatia mchakato wa sheria wa haki ni kanuni ya kale inayopatikana katika Agano la Kale na Agano Jipya. Maana ya sheria huhitaji hakimu wa haki, na Mungu ndiye kielelezo (Kwa mfano tazama: Kumb. 10:17-18; Zab. 7:9,12; 9:5; 50:6; 58:2-3; Zab. 75:3,8). Hakimu wa haki daima hutenda chini ya maagizo ya Mungu (2 Nya. 19:6-7). Hakimu lazima atambue kwamba Mungu humtazama yeye na yuko upande wa asiye na hatia: "**Kuzikataa haki za mtu mbele za Aliye Juu, kumnyima mtu haki – je, Bwana hataona mambo hayo?**" (Omb. 3:35).

Hukumu ni lazima ifanywe bila upendeleo (Kumb. 1:17; 2 Nya. 19:7; Mith. 18:5; 24:23; Ayu. 13:10; Kol. 3:25; Efe. 6:9), kwa kuwa Mungu hana upendeleo (kwa mfano Kumb. 19:17-18). Ni mahakimu waovu pekee wafanyao upendeleo (Isa. 3:9). Chuki bila sababu zisiathiri hukumu (1 Tim. 5:21), na kesi sharti ichunguzwe kikamilifu (Kwa mfano tazama, Kumb. 17:4).

Maandiko yanakataa viwango viwili vya kisheria, kama vile sheria moja kwa tabaka la watu wa juu na nyingine kwa wakulima. Hata wageni walifurahia haki zile zile za kisheria kama Waisraeli chini ya sheria ya Agano la Kale (Kut. 12:49). "**Msipotoe hukumu, msioneshe upendeleo kwa maskini au upendeleo kwa mkuu, bali mhukumu jirani yako kwa haki**" (Law. 19:15). Mungu hupigania haki za maskini na mafukara (Mith. 29:7; 31:8). Ki ukweli Biblia hutathmini haki ya taifa kwa namna

linavyowatendea wanyonge. Ustawi wa vyama vinavyoongoza si muhimu kuliko hali ya wasiojiweza. Maandiko hayahukumu kwa kuangalia hali ya matajiri, walio na fedha na nguvu ya kutetea haki zao, bali kwa kuangalia hali ya maskini, wajane na mayatima katika mfumo wa kisheria. "**Sema kwa ajili ya wale wasioweza kusema kwa ajili yao wenyewe, kwa ajili ya haki za wote walio fukara. Sema na hukumu kwa haki; tetea haki za maskini na wahitaji**" (Mith. 31:8-9). Mungu, Mwumbaji na Bwana wa mwanadamu hutaka tutendeane sisi kwa sisi kama taswira za (mifano ya) Mungu na kama viumbe walioumbwa, na siyo kama wanyama.

Haiwezekani kuwa na haki pasipo sheria, na pasipo haki hakuna serikali iwezayo kumpendeza Mungu. Si vinginevyo, hadi zama za sasa [ambazo ni] kipindi cha historia kilichofinyangwa na kanuni za Kikristo na kibiblia, ambapo wenye mamlaka duniani waliwekwa chini ya sheria na haki. Siku ambazo Mfalme angedai, "Mimi ni Serikali!"[49] kwa kutotarajia zimekwisha. Viongozi wa juu wa Serikali, na hata Serikali yenyewe, wako chini ya sheria, ni sharti waitii sheria, na wanaweza kushitakiwa na kuhukumiwa wasipoitii. Kama Wakristo tuna jukumu muhimu la kufanya, kwa kuwa pasipo haki mamlaka huwa udikteta. "Haki huinua taifa; bali dhambi ni aibu ya watu wowote" (Mith. 14:34). Baba wa Kanisa Mtakatifu Augustine aliandika: "Kama hakuna sheria, Serikali ni nini kama si genge la wezi? Magenge ya wezi si chochote bali viserikali vidogo vidogo."[50] Haramia alipoulizwa na Alexander Mkuu ni jinsi alivyothubutu kuifanya bahari kuwa mahali hatari, anaelezea hoja yake kwa mfano wa kueleweka; alimjibu kwa kiburi, "Kwa sababu tu ninatumia meli ndogo unaniita haramia. Unafanya vivyo hivyo kwa manowari na unajiita mwenyewe mfalme."[51]

Kadri tukataavyo kielelezo asilia cha Mungu wetu asiye na upendeleo, ufisadi na rushwa vitaongezeka Afrika. Ni wachache tu wanaotambua kwamba haya ni matokeo ya kimantiki ya kuziacha kanuni zetu za Kikristo. "**Mtu mwovu huikubali rushwa faraghani ili kupotosha njia**

---

[49] Mnamo Sept 7,1891, Kaiser Wilhelm II, kwa upuuzi wake usio na mpaka, alikitilia sahihi kitabu kiitwacho Golden Book of the City of Munich kwa maneno haya, "Suprema lex regis voluntas," ("Sheria kuu kabisa ni mapenzi ya Mfalme). Gerhard Jaeckel. Die deutschen Kaiser. Weltbild Verlag: Augsburg, n. d. (Repr. of Urbes Verlag: Gräfeling), uk. 188. Ingizo linapatikana katika Hans-Michael Körner. "'Na warte Wittelsbach!': Kaiser Wilhelm II. und das Königreich Bayern", kr. 31-42 katika: Hans Wilderotter, Klaus-D. Pohl (Ed.). Der letzte Kaiser: Wilhelm II. im Exil. Bertelsmann Lexikon Verlag: Gütersloh & Deutsches Historisches Museum Berlin, 1991, uk. 37.

[50] Aurelius Augustinus. Vom Gottesstaat. Bd. 1. dtv-klassik. dtv: München, 1988[3]. uk. 173 (Kapitel 4 "Reiche ohne Gerechtigkeit sind große Räuberbanden" in Buch 4).

[51] Rud., uk. 174.

ya haki" (Mith.17:23) Kwa kumgeuzia Mungu mgongo tunatupilia mbali kielelezo asilia cha hakimu wa haki, ambaye haki yake kamilifu na uadilifu wake kamilifu ni msingi wa ukataaji wowote wa upotoshaji wa haki. Je, Agano la Kale daima halimwelezi yeye kama, "**Mungu mkuu, Mwenye uweza na wa ajabu, asiyeonesha upendeleo na asiyekubali kupokea rushwa**" (Kumb. 10:17)? "**Basi sasa hofu ya BWANA iwe juu yenu. Hukumuni kwa uangalifu, kwa kuwa kwa BWANA Mungu wetu hakuna udhalimu au upendeleo au rushwa**" (2 Nya. 19:7).

Alikuwa ni Mkristo wa Makanisa ya Kiinjili, akiwa amevuviwa na tumaini lake la Kikristo, aliyefunua ufisadi ulioenea pote katika Tume ya Ulaya na kuilazimisha tume kujiuzulu. Hapa tunaweza kuona jinsi tunu za kibiblia na uadilifu katika mambo madogo madogo zinavyoweza kuwa na matokeo makubwa. Kitabu chake kwa jambo hili kinaitwa 'Uadilifu kwa ajili ya Ulaya'[52] *Programu nzuri namna gani! Tone la maji kwenye ndoo laweza kuwa mwanzo wa bahari!*

62. Tumaini kwa Wanasiasa

Hoja: Watu wacha Mungu katika Biblia mara zote walishika nafasi muhimu kama maofisa au watawala katika serikali zao – kwa nini isiwe Afrika?

Maandiko hutueleza juu ya mahakimu, wafalme na maofisa wengi wacha Mungu, katika Israeli na pia katika serikali nyingine. Mungu alimfanya Yusufu kuwa mtu mwenye mamlaka ya juu baada ya Farao huko Misri na alimweka Danieli katika cheo cha juu kwenye falme mbalimbali. Kama malkia Esta alivyokuwa maarufu katika ufalme wa Uajemi ndivyo Nehemia alivyotumika kama gavana chini ya mtawala mpagani. Nebukadreza, mfalme wa Babeli, aliongoka; Mfalme wa Ninawi alitubu baada ya kusikia ujumbe wa Yona. Naamani, jemadari aliyekuwa [sawa na] mkono wa kulia wa Mfalme wa Shamu (Syria) alioongoka kupitia mtumishi wa kike wa Kiisraeli na nabii Elisha. Watu hawa wote waliendelea kushikilia nafasi zao baada ya uongofu wao. Agano Jipya hutueleza juu ya askari na maofisa wengi wa Kirumi (kwa mfano Mat. 8:5-13; 15:39; 27:54; Luk. 7:2-9; 23:47; Mdo. 10:1-48) na kuhusu Dionisio (Mdo 17:34), meya wa Athene, ambao wote waliamini na kuwa Wakristo, lakini hawakuhitaji kuacha ofisi zao kama matokeo ya kuamini kwao.

---

[52] Paul van Buitenen. Blowing the Whistle: Fraud in the European Commission. Politico's Publ.: London, 2000; German: Paul van Buitenen. Unbestechlich für Europa: Ein EU-Beamter kämpft gegen Mißwirtschaft und Korruption. Brunnen: Gießen, 1999.

Agano Jipya hutaja kwa uwazi maofisa wa Kikristo wa siku zile, likitoa mwongozo tu wa majukumu yao kama wakusanyaji kodi, askari au polisi. Kwa mfano, Yohana Mbatizaji anawashauri maofisa wa Kirumi: "**Wakusanyaji kodi nao wakaja kubatizwa, wakamwuliza, "Mwalimu, tunapaswa kufanya nini? Akawaambia; "Msikusanye zaidi kuliko mnavyopaswa" Kisha baadhi ya askari wakamwuliza, "Na sisi tunapaswa kufanya nini?" Akawajibu, "Msitoze fedha kwa nguvu na msiwashtaki watu kwa uongo – mtosheke na malipo yenu**" (Luk. 3:12-14; Tazama pia Luk. 7:29). Baada ya kuamini kwake, Zakayo, yule mkusanyaji kodi, aliwarejeshea watu aliokuwa amewadanganya (Luk. 19:1-10): "Zakayo akasimama, akamwambia Bwana, Tazama, Bwana, nusu ya mali yangu nawapa maskini, na ikiwa nimemnyang'anya mtu kitu kwa hila namrudishia mara nne" (Luk. 19:8; Tazama pia Kut. 22:1).

Wakristo wengi, kimaana, huichukulia siasa kama kitu kiovu, lakini kwa nini tushangae kwamba siasa ni biashara "chafu' wakati tunashindwa kushiriki. Kwa nini wanasiasa wavutiwe na vipimo vya Mungu wakati Kanisa linawachochea kuvitupilia mbali? Basi kwa ukweli huo, hata sera nzuri ni biashara 'chafu', kwa sababu wajibu muhimu sana wa siasa ni kupambana na makosa ya jinai na udhalimu. Ikiwa Mungu ameipa serikali mamlaka, kimsingi haiwezekani kuwa ni makosa, kama vile yalivyo mamlaka ya wazazi kimsingi yasivyokuwa ni makosa, hata kama wazazi wasiomcha Mungu wametumia vibaya mamlaka yao. Siasa haziharibu tabia, bali huzifunua. Kama watu wote wacha Mungu wakijiondoa kwenye maisha ya kisiasa tunaweza kutegemea tu wasiomcha Mungu kuchukua nafasi zao.

Sharti tujifunze hilo, hata kama Mungu alikusudia Kanisa na Serikali kuwa taasisi mbili zilizotengana, zote zina wajibu uliowekwa na Mungu, na tunu zihubiriwazo na Kanisa na zilizowekwa wakfu na Mungu ni halali kwa Uumbaji wote. Wakristo kama mtu mmoja mmoja hawawezi kutengeneza sera kama wawakilishi wa Kanisa, bali kama raia. Jukumu la Kanisa ni kuifundisha serikali kanuni za ki-Mungu pasipo kulazimisha mawazo yake kwa Serikali au kuchukua mahali pa Serikali.

63. Tumaini kwa ajili ya Amani

Hoja: Tumaini kwa ajili ya amani inayoonekana katika mambo madogo na katika mambo makubwa hutokana na amani yetu isiyoonekana kwa Mungu, kwa kuwa mapenzi ya Mungu ni siku zijazo zenye amani. "Kwa kuwa najua mipango niliyonayo kwa ajili yako,"

asema BWANA, "mipango ya kufanikiwa na si ya kukudhuru, mipango ya kukupa tumaini na siku zijazo" (Yer. 29:11).

Mahusiano ya mtu kwa Mungu huamua uadilifu wake binafsi na pia maadili yake ya kijamii. Katika Warumi Paulo anadhihirisha wazi hali ya kupotea ya Wayahudi na Wayunani (Wagriki) na haja ya wokovu katika Kristo. Katika sura ya 5 anaandika: "**Kwa hiyo, kwa kuwa tumekwisha kuhesabiwa haki kwa njia ya imani, tuna amani na Mungu kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye kwa kupitia yeye tumepata, kwa imani, njia ya kuifikia neema hii ambayo ndani yake tunasimama. Na twafurahi katika tumaini la utukufu wa Mungu**" (Rum. 5:1-2). Ndipo sasa anaanza kuzungumzia maadili ya mtu binafsi (Rum. 6-8), ya kutamaduni (14-15) na ya kisiasa (13:1-7). Kitabu cha Warumi huonesha kwamba imani yetu wenyewe ina matokeo kwa masuala halisi ya maisha ya kila siku kama vile kazi, taifa na Serikali. Hatuwezi kuiwekea mpaka imani iwe ya mahusiano yetu binafsi na Mungu, na Kanisa pasipo kuondoa sehemu kubwa ya Kitabu cha Warumi!

Kwa sababu "vita na mapigano" ukijumuisha na migongano baina ya waamini hutoka katika tamaa zetu (Yak. 4:1), yaani hutoka katika utu wetu wa ndani; ulinzi wetu pekee dhidi ya hayo sharti utoke ndani, kwa kuwa na amani na Mungu na wenzetu wapendwa. Amani hii, inayoanzia katika mioyo yetu, sharti ifurike katika maisha yetu na kuyajaza kikamilifu.

64. Tumaini Huhitaji Mazungumzo na siyo Vurugu

Hoja: Tumaini hutupatia amani kujadili masuala na wale wanaotetea misimamo mingine.

Mazungumzo, majadiliano ya amani, uvumilivu na usikilizaji na kujifunza kiungwana kutoka kwa wengine ni tunu ya Kikristo, lakini hatuwezi kuacha madai haya makuu ya Ukristo kuwa wenyewe ndio wenye kumiliki ukweli au wajibu wake wa kufanya umisheni wa kiulimwengu bila kuichanganua imani yetu kwa pamoja.

Mazungumzo kati ya Wakristo na wafuasi wa dini nyingine na wafuasi wenye mtazamo-dunia mwingine yanawezekana pale tunapoweza kujadili imani yetu kwa njia ya amani ("**Mwe tayari daima kutoa jibu kwa yeyote awatakaye mtoe sababu kwa ajili ya tumaini mlilonalo. Lakini fanyeni hivi kwa wema na heshima**" (1 Pet. 3:15-16)), tuwasikilize wengine (Yak. 1:9) na tuwe tayari kujifunza kutokana na uzoefu wa wengine katika nyanja nyingi za maisha (Tazama Mithali), na kwamba daima tuwe tayari kujichunguza sisi wenyewe na tabia zetu.

Mazungumzo ambayo kwa muda fulani au kinadharia hukana ukweli mkamilifu wa dai kuu la Yesu Kristo, (Yoh. 14:6), wa Injili (Rum. 1:16-17; 2:16), au wa Neno la Mungu (2 Tim. 3:16 -17; Ebr. 4:12-13; Yoh. 17:17), au ulinganifu wa ufunuo wa Maandiko [Biblia] na Maandiko ya dini nyingine, hayapatani kabisa na huduma ya umisheni ya Kikristo na asili yenyewe ya Ukristo. Madai ya Biblia ya mamlaka kamilifu yameelezwa vizuri sana katika mafundisho ya Hukumu ya Mwisho na Uzima wa Milele. Waebrania 6:1-2 huorodhesha "ufufuo wa wafu, na hukumu ya milele," katika misingi sita muhimu ya imani yetu. Kanisa limekuwa likishikilia dhana hizi katika historia yake yote kama Imani ya Mitume inavyotukumbusha: *"kutoka huko atakuja kuwahukumu walio hai na wafu."*

65. Tumaini kwa Kanisa

Hoja: Ni makanisa pekee yenye tumaini ndiyo yanayoweza kutoa tumaini kwa Afrika. Tunahitaji viongozi wanaotenda na kufundisha tumaini.

Lazima tukumbuke kwamba Mungu hupenda ukuaji wa kanisa, wa aina zote mbili za kupandikiza makanisa ya nje, na ule wa ukomavu wa ndani; yaani ukuaji wa idadi na ukuaji wa kina wa kiroho, upendo wa mtu binafsi kwa Mungu, na kwa Neno lake na katika tumaini lililojengwa juu ya fursa zake zisizo na mipaka.

Hivyo, makanisa mengi ya Afrika yamejiondoa yenyewe katika kufuata mambo ya kiulimwengu na mambo ya ndani yanayohusu jamii yetu. Viongozi wengi wa makanisa huendelea kujitoa mhanga katika huduma, lakini hawana mtazamo wa wakati ujao. Wanasimamia masuala waliyoyarithi, lakini hawana ujumbe kwa ajili ya wakati ujao na hawana maono ya fursa za Mungu.

Afrika inahitaji viongozi wenye tumaini. Tunahitaji kuachilia mbali mifumo yetu ya mafunzo ya kitheolojia ya kiakili, kifalsafa na kinadharia na kuanzisha programu mpya za mafunzo za kusisimua kama zile zilizotumiwa na Yesu na Paulo. Tunahitaji maandalizi yenye kubadilisha utendaji kwa kugeuza mawazo na maandalizi yenye kukabiliana ana kwa ana na masuala yanayohusu wakati wetu. Ni wale tu wenye matumaini ya kweli wanaoweza kuyafundisha kwa viongozi wa kizazi kipya.[53]

---

[53] Tazama Thomas Schirrmacher. "Jesus as Master Educator and Trainer". Training for Crosscultural Ministries (World Evangelical Fellowship) 2/2000: uk 1-4; „Paul and His Colleagues". Training for Crosscultural Ministries (World Evangelical Fellowship) 3/2000: pp 6-8; "Ausbilden wie Jesus und Paulus", kr. 7-43 katika: Klaus W. Müller, Thomas Schirrmacher (Hg.). Ausbildung als missionarischer Auftrag. Referate der Jahres-

66. Kuna Tumaini kwa masuala ya Kisiasa wakati Kanisa Linapotubu

Hoja: Tukianza na uamsho wa kimatengenezo wa kibiblia wa mtu binafsi, na kuendelea mbele hadi kwenye ujenzi wa familia; Kanisa la Kikristo ni lazima kwanza lianze kuyajenga upya Matengenezo.

"**Kwa mana ni wakati wa hukumu kuanza na familia ya Mungu**" (1 Pet. 4:17)[54], kwa kuwa maoni ya Paulo kuhusu Wayahudi, yanayokubaliana na Agano la Kale, ni halisi kabisa kwa Kanisa: "**Kama ilivyoandikwa: 'jina la Mungu linakufuriwa miongoni mwa Mataifa kwa sababu yenu**'" (Rum. 2:24). Dhambi za Wakristo na za Kanisa ni mbaya sana kuliko zile za 'dunia': "**Ikiwa wameepa ufisadi wa dunia kwa kumjua Bwana na Mwokozi wetu Yesu Kristo na kisha tena kujizongomeza ndani yake na kushindwa, ni wabaya sana mwishoni kuliko walivyokuwa hapo awali. Ingelikuwa bora kwao kutoijua njia ya haki, kuliko kuijua na kisha kuigeuzia mgongo amri takatifu ambayo walipewa**" (2 Pet. 2:20-21).

Ngoja turudie: kuna njia moja tu ya kuijenga upya siasa na jamii yetu. Kama ilivyo muhimu kuichunguza Sheria ya Mungu ili kutambua ni nini kilichoenda mrama, na kugundua njia ya Mungu ya kufanya mambo, sharti tujianzie sisi wenyewe: "Ikiwa watu wangu, walioitwa kwa jina langu, watajinyenyekesha, na kuomba, na kunitafuta uso, na kuziacha njia zao mbaya; basi, nitasikia toka mbinguni, na kuwasamehe dhambi yao, na kuiponya nchi yao" (2 Nya. 7:14). Ndipo tunaweza kuanza kuomba kwa dhati kwa ajili ya jamii yetu na serikali zetu. Basi tutumaini kwamba Mungu hatatuambia sisi jambo lile lile kama alivyowaambia Israeli: "Nilimtafuta mtu miongoni mwao ambaye angejenga kuta na kusimama mbele zangu … kwa niaba ya nchi ili kwamba nisije kuiharibu, lakini sikumwona yeyote." (Eze. 22:30). "Injili ya kweli lazima ionekane katika maisha ya wanaume na wanawake waliobadilishwa. Kadri tunavyotangaza upendo wa Mungu ni lazima tushiriki katika huduma za upendo, kadri tunavyohubiri Ufalme wa Mungu sharti tujitoe kikamilifu kwenye matakwa yake ya haki na amani."[55]

---

tagung 1999 des afem. edition afem - mission reports 7. Verlag für Kultur und Wissenschaft: Bonn, 1999.

[54] John Calvin kipekee husisitiza wazo hili. Tazama Heinrich Berger. Calvins Geschichtsauffassung. Studien zur Dogmengeschichte und Systematischen Theologie 6. Zwingli Verlag: Zürich, 1956, uk. 229.

[55] Das Manifest von Manila. Lausanner Bewegung - Deutscher Zweig: Stuttgart, 1996, uk. 14 (paragraph 4); English text: www.gospelcom.net/lcwe/statements/manila.html (26.11.2001).

Basi Mungu wa tumaini awajaze ninyi furaha na amani yote kadri mnavyomtumaini yeye, ili kwamba mweze kufurika tumaini kwa nguvu za Roho Mtakatifu. *(Warumi 15:13)*

VISAWE NA MAELEZO YA MANENO

Anuwai (diversity): aina mbalimbali.
Amali (values): mambo yenye kuthaminiwa sana katika jamii.
Aedeolojia (ideology): mfumo wa kiitikadi.
Baba wa Kanisa (Church Father): Kiongozi wa Kanisa katika karne za mwanzo waliotoa mchango uliotukuka kwa kanisa.
Bwanyenye (Burgeois): Mtu ambaye ana mali nyingi, hasa mashamba na majengo makubwa; mwinyi; tajiri mwenye ardhi au majumba ya kupangisha mjini; kabaila; mtu anayependa starehe lakini hapendi kufanya kazi.
Chapeo (Helmut): kofia ngumu yenye kulinda kichwa iliyotumiwa na askari wa Kirumi.
Dhamira (Theme): wazo au mada zinazojitokeza, au mambo muhimu yanayozungumziwa.
Dhana (Concept): Wazo.
Elimu-Maadili (Ethics): Mfumo wa Elimu unaojishughulisha na maadili au kujua mema na mabaya.
Epa (escape): kukwepa jambo
Eskatolojia (eschatology): Elimu ya dini inayohusu mambo ya siku zijazo.
Falsafa (Philisophy): 1. Elimu ya mambo au vitu inayohusu asili, maana na sababu za kuwepo kwao 2. Mfumo wa mawazo unaotawala mtindo wa maisha.
Famasi (Pharmacy): duka la dawa baridi.
Fasili (Interpretation): Eleza maana ya neno kwa undani zaidi, fafanua, pambanua.
Fursa (Opportunity): Nafasi; wasaa.
Ghushi (Forge): Iga, danganya.
Jozi (Pair): Vitu viwili vinavyofanana ambavyo hukaa pamoja k.v. viatu n.k.
Kinzani (Opposite, Contrary): enye kupinganishwa na nyingine, enye kulinganishwa na nyingine kwa kutumia tofauti.
Lahaja (Dialect): Tofauti katika matamshi, maumbo na matumizi ya maneno mbalimbali kwa lugha yenye asili moja.
Kita (base): weka msingi katika jambo fulani.
Kitenzi (Verb): aina mojawapo ya maneno ambayo huelezea kitendo, au hali ya nomino (jina).
Maadili (Morality, Morals): 1. Mfumo wa mwenendo wa tabia. 2. Tabia au mienendo iongozayo jamii wa mtu mmoja mmoja.

Majaaliwa (fate): mambo yanayotupata yaliyo nje ya uelewa na uwezo wetu.

Mambo au wakati a baadaye/wa usoni (Future): wakati ujao

Manifesto (Manifesto): Ilani

Mantiki (Logic/Reason): uwezo bora wa kufikiri; kufikiri katika mtiririko au mpangilio unaokubalika kiakili.

Mashua okozi (Lifeboat) - Mashua ya kuokolea watu au inayochukuliwa kutoka melini.

Matengenezo (Reformation): Wakati wa kihistoria katika kanisa ambapo mageuzi makubwa katika mafundisho ya Kanisa yalitokea, wahusika muhimu ni pamoja na Martin Luther, John Calvin n.k.

Mkamilishano (complementarity): vitu au hali zenye kukamilishana; au vinavyotokea katika uwili.

Mrazini (Rationalist): mwenye akili timamu; mwenye uwezo wa kufikiria, au mwenye kuwaza kimantiki.

Msongo (Suffocation): Tendo la kusonga kitu; namna ya kusonga; mbinyo

Mtazamo-dunia (Worldview): mfumo au mtazamo unaoongoza jinsi mtu anavyoutazama ulimwengu.

Mzizi (Root): Kiini au kipande cha msingi cha neno

Siha (health): afya njema.

Sekyula (secular): -a kidunia.

Sheria Asilia (Natural Law): Sheria inayotokana na asili au maumbile.

Tafsiri (Translate): badili lugha moja kwenda lugha nyingine.

Tasnifu (Thesis): Maandiko ya kitaaluma yanayochanganua mada maalumu aghalabu kwa ajili ya kupata shahada ya juu.

Theolojia (Theology): Taaluma ya dini inayohusu tabia na sifa za Mungu na misingi ya imani za dini.

Tunu (Values): mambo yenye kuthaminiwa na jamii husika.

Uadilifu (Righteous): Hali ya kutenda haki bila kupendelea upande wowote.

Uajemi (Persia): nchi au dola iliyojulikana sana wakati wa kale.

Uamsho (Revival): Ufufuaji, uhuishaji, uamshaji, au urudishaji (hali ya zamani).

Udhalimu (Injustice): Tendo la kufanya mambo yaliyo kinyume cha haki; uonevu, hiana, ukatili.

Udogma (Dogmatism): mfumo wa mafundisho ya kidini unaoshikilia imani za kimsingi za dini husika bila kubadilikabadilika na unaoaminiwa na wafuasi bila kupingwa.

Ufisadi (Corruption): Mambo machafu, yasiyofaa au kukubalika katika jamii.

Uhalifu/Ukosa-sheria (Lawlessness): Tendo la kuvunja sheria za jamii

Ujamaa wa Kitaifa (National Socialism): Mfumo wa Kisiasa uliofuatwa na Manazi huko Ujerumani.

Ukokotoaji (Calculation): hali ya kuchambua jambo kutoka hatua moja hadi nyingine kwa mujibu wa mfuatano unaokubalika mf. Kukokotoa hesabu.

Ungamo/Ukiri (Confession): tamko la kiimani

Umaksi (Marxism): Itikadi ya kisiasa na kiuchumi iliyobuniwa na Mjerumani, Karl Marx, ambayo inataka njia kuu za uchumi zimilikiwe na umma.

Umanikaisimu (Manichaeism): Mfumo wa imani uliofundisha kuwa roho ya mwanadamu itokayo katika ufalme mwema (wa Mungu) hutafuta kujiondoa au kuuepa mwili ambao hutokana na ufalme mwovu (wa Shetani), yaani roho ni kitu chema na kisafi na mwili ni kitu kiovu na kichafu.

Uongofu (conversion): Kugeukia imani nyingine; uamini mf. Kumwamini Yesu.

Upayatisti (Pietism): mwako, au mfumo wa kiimani wenye kuzingatia au kuyatazama zaidi mambo kiroho.

Usuli (Background): Chanzo, asili au msingi wa kitu, hali au jambo

Uumbaji (Creation): jumla ya vyote vilivyoumbwa; viumbe.

Uyumanisti (Humanism): Mtazamo wa maisha unaomwona binadamu kuwa kiini cha kila jambo.

Vuguvugu (Movement): Mwamko au wimbi lenye mvuto mkubwa kwa kundi fulani la watu wenye kufuata mawazo au mtazamo fulani.

Wanatheolojia kinzani (critical theologians): wanatheolojia wenye kupinga mafundisho msingi ya kidini.

Zama Mpya (New age): Mfumo au itikadi inayoaminiwa na baadhi ya watu katika nyakati hizi.

Zongomeza (entangle): Ingiza matatizoni, mtegoni n.k.

VIFUPISHO VYA MANENO

mst. (v.) – mstari wa Biblia
n.k. (etc.)– na kadhalika
k.v. – kama vile
Dk. (Dr.) – Daktari
uk. (p.) – ukurasa
kr. (pp.) – kurasa (nyingi)
Rud. (Ibid.). Rudia nukuu iliyoko hapo juu.